# MAUDHUI YA MAPINDUZI KATIKA RIWAYA ZA VISIWANI ZANZIBAR:

NA

SIMON KIMANI NJOGU

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya 'Master of Arts' katika Chuo Kikuu cha Nairobi."

1987

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0146948 5

UNGAMO:

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika Chuo Kikuu kingine."

SIMON KIMANI NJOGU
(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu."

18/6/87

DKT. JAY KITSAO

18.6.87

BW. KITHAKA WA MBERIA

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu Geoffrey Njogu Kariuki na Martha Njeeri Njogu.

# YALIYOMO


Yaliyomo .............................. i

Shukrani.............................. iii

Muhtasari.............................. v

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi wa Utafiti...........

1.1 Utangulizi...................... 1

1.2 Somo la Utafiti................ 1

1.3 Madhumuni ya Utafiti............ 3

1.4 Upeo wa Tasnifu................. 4

1.5 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili.. 6

1.6 Sababu za kulichagua somo hili.. 14

1.7 Msingi wa Nadharia.............. 21

1.8 Njia ya Utafiti.................. 31

1.9 Tanbihi ......................... 34

SURA YA PILI

2.0 Muundo wa Mfumo wa Uzalishai Mali

2.1 Utangulizi ........................ 37

2.2 Nyenzo za uzalishaji mali ........ 38

2.3 Ukoloni Visiwani Zanzibar......... 43

2.4 Muundo wa Kijamii................. 47

2.5 Elimu na Nafasi za kazi........... 53

2.6 Pupa.............................. 64

2.7 Hitimisho......................... 75

2.8 Tanbihi........................... 77

SURA YA TATU

3.0 Nafasi ya Mikinzano ya Kitabaka

3.1 Utangulizi........................... 78

3.2 Mikinzano na mapinduzi.............. 79

3.3 Mikinzano baina ya matabaka......... 83

3.4 Urazini wa Kitabaka.................. 110

3.5 Taasisi za Kitawala.................. 124

3.6 Hitimisho........................... 128

3.7 Tanbihi.............................. 129

SURA YA NNE

4.0 Mapinduzi na Baadaye

4.1 Utangulizi........................... 132

4.2 Siasa za vyama...................... 133

4.3 Kulipuka kwa mapinduzi.............. 141

4.4 Uimarishaji wa mapinduzi............ 147

4.5 Hitimisho........................... 158

4.6 Tanbihi.............................. 161

SURA YA TANO

5.0 Himitisho...........................

5.1 Utangulizi........................... 163

5.2 Kazi kwa jumla...................... 163

5.3 Ilhamu.............................. 166

5.4 Matatizo na mafanikio............... 168

5.5 Mapendekezo......................... 168

Marejeleo........................... 170

## SHUKRANI

Natoa shukrani nyingi kwa wasimamizi wa kazi hii Dkt. Jay Kitsao na Bw. Kithaka wa Mberia kwa kuniongoza na kunipa mashauri yaliyonifaa na kunitanzua kififikra.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika kwa kunihimiza na kunitia shime katika masomo yangu. Miongoni mwa hawa sina budi kuwataja wafuatao: Profesa Karega Mutahi (Mudiri wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika) Profesa Mohammed Abdulaziz, Dkt. Mohamed Bakari, Bw. Kazungu Kadenge na Bw. Ali Wasi Mwabaya.

Nina masahibu wengi ambao tangu mwanzo wamenishajiisha kwa kujihusisha kwa dhati katika masomo yangu. Baadhi yao ni: Dkt. Al'amin Mazrui, Dkt. Chacha Nyaigotti, Rocha Chimerah, Zakayo Ole Nchoe, na Kariri Ngotho. Ahsanteni.

Kazi hii haingefaulu japo sikupata ushirikiano wa wanafunzi wenzangu: Mukuriah, Maringah, Marwa, Mwove na Onditi. Nawapa shukrani zangu za dhati.

Aidha, nawashukuru wazazi wangu wapenzi Geoffrey Njogu Kariuki na Martha Njeeri Njogu. Mlinifunza unyenyekevu, uvumilivu na subira. Tena, mkajitolea na kujinyima mambo mengi ya lazima ili nipate elimu. Mlinielekeza katika ulimwengu wenye giza na kuniibusha nilipotaka kukata tamaa. Mliniinua nilipoteleza. Sina maneno niyajuayo yanayoweza

kuelezea shukrani zangu kwenu.

Tena, nawashukuru ndugu zangu kwa kuniunga mkono katika safari hii. Tangu mwanzo tumevushana kama ndugu.

Masomo yangu ya digrii ya uzamili yamegharamiwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta. Natoa shukrani kwa Chuo hicho na hasa kwa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kuniteua niendelee na masomo ya uzamili.

Nakushukuruni mke wangu mpenzi Joyce Njooki na watoto wangu Njogu, Njeeri na Wanjiru. Mmevumilia upweke mwingi nikiwa masomoni.

Mwisho, ahsante Jane W. Mutharia kwa kunipigia chapa kazi hii.

## MUHTASARI

Tasnifu hii inajadili maudhui ya mapinduzi katika riwaya za visiwani Zanzibar. Tunachunguza vile maudhui haya yalivyosawiriwa katika riwaya za Mohamed Suleiman Mohamed, Said Ahmed Mohamed na Shafi Adam Shafi. Kazi hii inajaribu kuonyesha kwamba fasihi huathiriwa na matukio ya kihistoria na huweza kuyahifadhi kisanaa. Aidha, inajaribu kubainisha kwamba kitovu cha mapinduzi kinapatikana katika mfumo wa uzalishaji mali.

Sura ya kwanza ni Utangulizi wa Utafiti. Hapa ndipo tunapojadili somo letu, madhumuni na upeo wa utafiti huu. Fauka ya hayo, tunasema machache kuhusu nadharia tunayoitumia kama kigezo cha kipimia waandishi hawa kwa mujibu wa usawiri wa maudhui ya mapinduzi. Vile vile, tunajadili baadhi ya kazi zingine zilizowahi kuandikwa na ambazo, kwa namna fulani, zinahusiana na utafiti wetu. Sababu zilizotuelekeza katika kulichagua somo hili zinatajwa katika sura hii.

Sura ya pili inauhakiki mfumo wa uzalishaji mali kama msingi wa mapinduzi ya visiwani. Inaonyeshwa kwamba nyenzo za uzalishaji mali zilimilikiwa na tabaka dogo ambalo zaidi lilipewa nguvu na utawala wa kikoloni. Fauka ya hayo, mfumo wa uzalishaji mali unaonyeshwa kwamba uliendeleza pupa iliyofurutu na

ulikuwa na ubaguzi katika kutoa nafasi za elimu na kazi.

Katika sura ya tatu tunaonyesha kwamba mikinzano ya kitabaka ina nafasi kubwa katika kuwepo kwa mapinduzi ya kijamii. Lakini mikinzano hiyo haina budi kuongozwa kiurazini. Nafasi ya taasisi za kitawala katika migogoro ya kitabaka inajadiliwa hapa.

Sura ya nne inahusu mapinduzi na baadaye. Katika sura hii siasa za vyama zinaonyeshwa kuwa na nafasi muhimu miongoni mwa matabaka yanayokinzana. Baada ya kuzijadili siasa hizo, tunaonyesha vile kulipuka kwa mapinduzi kulivyosawiriwa katika riwaya tunazozihakiki. Mwisho, tunajadili uimarishaji wa mapinduzi.

Katika sura ya hitimisho, tumetoa muhtasari wa kazi tuliyoifanya na tukaonyesha matumaini yetu kuwa waandishi hawa wa visiwani watawahamasisha waandishi wengine wa visiwani na kwingineko. Aidha, tunatoa mapendekezo kuhusu utafiti zaidi wa fasihi ya visiwani, Zanzibar.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI WA UTAFITI

### 1. 1 UTANGULIZI

Mnamo Januari 12, 1964 kulitokea mapinduzi visiwani Zanzibar ambayo yaliondolea mbali utawala wa Kisultani. Mapinduzi haya yalibadili kwa kiasi kikubwa mfumo wa uzalishaji mali visiwani kwa sababu Waafrika ambao kazi yao zaidi ilikuwa kuwahudumia mamwinyi na mabepari, walianza kupata hadhi ambayo ilikuwa stahiki yao.

Baina ya 1970 na 1980 waandishi fulani wa riwaya visiwani waliyashughulikia mapinduzi haya katika kazi zao kwa kuyahuisha kisanaa.

### 1.2 SOMO LA UTAFITI

Katika tasnifu hii tunanuia kujishughulisha na uhakiki wa maudhui ya mapinduzi katika riwaya za visiwani Zanzibar. Waandishi wa visiwani tuwajuao wanaobainisha maudhui ya mapinduzi ni Shafi Adam Shafi (1978, 1979), Said Ahmed Mohamed (1978, 1980(a), 1980(b) na Mohamed Suleiman Mohamed (1972, 1976).

Riwaya zao zinabainisha mapinduzi katika viwango viwili. Kwanza, zinabainisha mapinduzi kwa kukiuka kaida iliyowekwa na watangulizi wao kama Mohamed Said Abdalla na Mohamed Saleh Farsy kwa kujiepusha na masuala ya upelelezi na utamaduni. Pili, riwaya

hizi zimejaribu kuonyesha hali za kiuchumi na kijamii zilizosababisha kuwepo kwa mapinduzi ya visiwani mnamo Januari, 1964. Tutajishughulisha na kiwango cha pili cha mapinduzi.

Riwaya tutakazozihakiki katika kiwango cha maudhui ya mapinduzi ni Kasri ya Mwinyi Fuad (1978) Kuli (1979); Asali Chungu (1978), Dunia Mti Mkavu (1980(a) Utengano (1980 (b); Kiu (1972) na Nyota ya Rehema (1976) Ingawa Said Ahmed Mohamed ana maudhui haya katika Sikate Tamaa na Kina cha Maisha, kazi hizi hazitahakikiwa kwa sababu ni kazi za ushairi. Tutachunguza hali za kisiasa, kiuchumi, na kijamii zilizoyaleta mapinduzi ya 1964 kama zilivyowasilishwa kwa ubunifu. Kwa hivyo, tutauchunguza mfumo wa uzalishaji mali kama unavyojitokeza katika riwaya hizi. Tutachunguza mikinzano ya kitabaka ambayo huenda ilizushwa na mfumo huo. Aidha, tutachunguza kuandaliwa, kuhitimishwa na kutekelezwa kwa mapinduzi kama kujitokezavyo katika riwaya tunazozishughulikia.

Kazi ya fasihi inayozingatia uyakinifu wa kijamii ina kiwango cha ubunifu na kiwango cha uhalisi wa maisha. Kulingana na nadharia ya ki-marx, uyakinifu wa kweli ni ule unaoukaribia ukweli wa kihistoria kama iwezekanavyo. Endapo kazi hiyo itazungumzia

matukio ya jamii basi msanii hatakuwa na budi kuonyesha misingi yake katika historia.

Engels (katika Bisztray 1978:17) amesema hivi kuhusu uyakinifu:

> Uyakinifu, kwa maoni yangu, humaanisha licha ya ukweli wa maelezo, ukweli katika usawiri wa wahusika halisi, katika hali halisi.

Kwa hivyo uyakinifu una vipengee vitatu: kusimulia hadithi kikweli, kuwa na wahusika halisi na kuwasawiri wahusika hawa katika hali halisi. Hali halisi hiyo ni ya kihistoria.

Kama vile ambavyo mwandishi myakinifu hapaswi kuipuuza historia naye mhakiki hana budi kuizingatia katika utanzuaji wa vitushi. Katika uhakiki wetu tutaizingatia historia ya visiwani hasa kufungamana na maudhui ya mapinduzi. Msingi huu wa kihistoria utatusaidia katika kutufahamisha hali za kisiasa, kiuchumi na kijamii zilizowazaa waandishi tunaoshughulika nao.

## 1.3. MADHUMUNI YA TASNIFU

Mwandishi hawezi kujitenga na hali za kihistoria zilizomkuza au zilizoikumba jamii aizungumziayo endapo kazi zake zitakuwa na uyakinifu. Madhumuni ya uchunguzi wetu ni kubainisha kwamba fasihi

huathiriwa na matukio ya kihistoria. Tutachunguza, kama tulivyotangulia kusema, hali za kiuchumi, kisiasa na kijamii zilizoyafanya mapinduzi ya visiwani Zanzibar mnamo Januari 12, 1964 kuwa jambo la lazima kulingana na riwaya tulizozichagua. Haya tutayafungamanisha na uhalisi wa kihistoria.

Aidha, tutachunguza ni kwa namna gani maudhui ya mapinduzi yameendelezwa na kuhitimishwa na Waandishi wa visiwani tutakaowahakiki. Madhumuni yetu yatakuwa ni kuwalinganisha ili tubainishe mshabaha walio nao au tofauti zinazojitokeza. Uyakinifu wa kihistoria utazingatiwa katika ulinganishi huu.

1.4 UPEO WA TASNIFU

Mhakiki yeyote wa kazi ya fasihi anaweza kujikita katika uchunguzi wa utanzu wowote wa fasihi uwe riwaya, tamthilia, ushairi au fasihi simulizi. Baada ya kuuchagua utanzu autakao, anaweza kuzama katika uhakiki wa kimaudhui au wa kifani.

Katika tasnifu hii tumehitari kuzichunguza riwaya za visiwani Zanzibar ambazo zina maudhui maalum - maudhui ya mapinduzi. Yaani riwaya zinazohakikiwa ni zile zinazosimulia mfumo wa uzalishaji mali uliokuwepo kabla ya mapinduzi na ambao ulikuwa msingi wa mapinduzi hayo. Pili,

riwaya zinazosimulia hali iliyoletwa na mapinduzi ili kuyatekeleza na kuyaimarisha.

Kama tulivyotangulia kusema kazi hii itahakiki riwaya za Shafi Adam Shafi, Said Ahmed Mohamed na Mohamed Suleiman Mohamed. Ingawa Mohamed Said Abdalla ni mwandishi mashuhuri visiwani Zanzibar, amejishughulisha na maandishi ya upelelezi. Naye M.S. Farsy (1960) amezama katika masimulizi ya utamaduni wa Waswahili hasa ulivyofungamana na Uislamu. Kazi za waandishi hawa hazitajadiliwa kwa sababu maudhui yake ni tofauti na yale tunayoyachunguza.

Uchambuzi tunaoufanya ni wa kifasihi. Lakini suala tunalolichunguza linahitaji msingi wa historia, siasa na uchumi wa Zanzibar kabla na baada ya mapinduzi ya 1964. Katika uhakiki wetu tutalazimika kuigusia historia ya Zanzibar, siasa na uchumi wake hasa kabla ya mapinduzi. Msingi huu utatusaidia katika ulinganishaji wa yale yanayotukia katika riwaya na matukio halisi ya kihistoria. Tunafahamu kuwa kazi ya sanaa huwa na kipengee cha ubunifu na cha uhalisi. Hali hiyo halisi hufahamika inapolinganishwa na uyakinifu wa kihistoria.

Madhali tunajadili maudhui ya mapinduzi hatuna budi kuifahamu dhana hii katika muktadha wa mahusiko

yetu. Kwa vile huu ni uchambuzi wa kifasihi na wala si wa kisiasa hatutajiingiza katika dhana hii kwa mapana na marefu yake.

## 1.5 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Leon Trotskii (1971) ameonyesha kuwa Mapinduzi ya Urusi yalifurika katika sanaa na hasa fasihi. Fasihi ya mamwinyi ikaipisha fasihi ya wafanyakazi na mafalahi. Amechambua mkondo wa sanaa kabla ya mapinduzi ya 1917 kisha akaonyesha mkondo uliopasa kuchukuliwa na sanaa baada ya mapinduzi hayo. Trotskii (1971: 228 - 256) ametoa maoni yake kuhusu sanaa ya kimapinduzi na kijamaa. Anatutahadharisha kuwa:

> Fasihi inayotakikana wakati wa enzi ya mapinduzi, ni fasihi ya kimaendeleo inayowaimarisha wafanyakazi dhidi ya wanyonyaji. Fasihi ya kimapinduzi haina budi kupata moyo wa uhasama wa kijamii, ambalo ni jambo la ubunifu na la kihistoria wakati wa enzi ya 'uimla' wa wafanyakazi.[1]

Madhumuni ya uchunguzi wa Trotskii yalikuwa ni kubainisha mkondo wa fasihi ya Kirusi kabla na baada ya mapinduzi ya 1917. Utafiti tunaoufanya unahusu fasihi ya Zanzibar katika muktadha wa maudhui ya

mapinduzi. Fikra za Trotskii zitatufaa kwa kiasi fulani kwa sababu utafiti wake umegusia mambo tunayojishughulisha nayo ingawa ni katika muktadha tofauti.

Makala ya Mao Tse Tung (1893-1977) '<u>On Literature and Art</u>'yanazungumzia kuhusu uhusiano baina ya kazi ya fasihi na kazi ya kimapinduzi kwa jumla. Lengo la makala hayo yaliyotolewa Yenan, Mei 1942 ni kuhakikisha kwamba fasihi ya kimapinduzi imefuata mkondo wa maendeleo na inatoa mchango wake katika kulikomboa taifa la Uchina. Mao Tse Tung (Katika Lang na Williams 1972: 116-117) anatoa mwito kuwe na wiano wa siasa na sanaa katika fasihi. Kwa hivyo, kazi ya kimapinduzi haina budi kutathminiwa kwa kutumia vigezo vyote viwili.

Hotuba hii iliyotolewa kabla ya mapinduzi ya Uchina ya 1949 inatupa mwelekeo mzuri kuhusu dhima ya fasihi katika harakati za ukombozi na baada ya ukombozi.

Kuna maandishi mengine mengi ambayo yamejishughulisha na suala la fasihi na jamii kama vile ya Baxandall (1972), Vasquez (1973), Bisztray (1978) na Ngugi wa Thiong'o (1981, 1986). Kwa kiasi fulani waandishi hawa wameonyesha kuwa fasihi ni kielelezo cha hali halisi za kijamii na haiwezi kattu kujitenga

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

na masuala ya kijamii. Licha ya kuzichangamsha nafsi za hadhira yake, fasihi ya kimapinduzi ina jukumu la kumwondoa binadamu kutoka hali dhaifu aliyo nayo hadi hali nzuri ya kiutu. Utafiti tuufanyao unahusu mabadiliko ya kiuchumi na vile mabadiliko hayo yalivyohifadhiwa kisanaa. Waandishi hawa wameujadili uhusiano wa fasihi na jamii kwa ujumla ilhali sisi tumejikita katika maudhui na muktadha maalum wa kijiografia na kisanaa.

Lofchie (1965) ameonyesha mambo kadhaa:vile visiwa vya Zanzibar vilivyowapokea wageni waliochagua kulowela huko baada ya shughuli zao za kibiashara; vile Waarabu walivyojikita na kutamakani visiwani humo; vile mitafaruku ya kiuchumi na kisiasa iliyozidishwa na ubaguzi wa rangi na uchaguzi wa 1963 na vile mapinduzi ya 1964 yalivyotokea. Lengo la Lofchie lilikuwa kuonyesha msingi wa mapinduzi ya 1964 huku akitumia mkabala wa kihistoria. Katika uhakiki wa maudhui ya mapinduzi tutauhitaji msingi huu.

Tasnifu ya M.A. ya M.H. Jabir (1977) inachunguza muundo wa kiuchumi hasa kuhusiana na mashamba makubwa ya karafuu visiwani Zanzibar baina ya 1890 na 1964. Aidha, Jabir (1977: 184-212) amejadili vile ukulima huo wa mashamba makubwa ulivyosababisha mapinduzi

ya 1964. Suala la mashamba makubwa ya karafuu ni muhimu katika utafiti wetu. Hatuwezi kulijadili kwa kirefu kama alivyofanya Jabir bali tutachunguza lilivyowasilishwa katika riwaya tunazozihakiki na vile lilivyochangiza katika kuyaleta mapinduzi ya 1964.

John Okello (1967) ameonyesha kuwa rangi ya mtu ilikuwa kigezo muhimu katika ugawaji wa rasilmali za taifa la Zanzibar. Waarabu walikuwa wakwasi kwa kila hali ilhali Waafrika walikuwa wakata kwa sababu Waarabu ndio walioshika nyenzo kuu ya uzalishaji mali - ardhi. Tofauti hii ya kitabaka iliendelezwa na Uingereza ilipochukua "Ulinzi" wa visiwa hivi mnamo 1890. Waarabu wakapewa hadhi kubwa serikalini na nafasi nzuri ya kwenda masomoni ng'ambo. Mwafrika akakengeushwa na ardhi ambayo tangu hapo ilikuwa yake. Okello anatueleza kuwa hali hii, pamoja na uchaguzi wa 1963 uliowapendelea Waarabu, ni baadhi ya mambo yaliyosababisha mapinduzi ya 1964. Maandishi kama hayo ya Okello yanatupa msingi mzuri wa kihistoria utakaotusaidia katika utafiti tunaoufanya.

Dhana ya mapinduzi imejadiliwa na maulama wengi wa taaluma ya uchumi na siasa. Jack Woddis katika kitabu chake New Theories of Revolution amehakiki

nadharia mbalimbali za mapinduzi hasa kuhusiana na nafasi ya matabaka katika kuyafanikisha mapinduzi. Amewachunguza Frantz Fanon, Regis Debray na Herbert Marcuse. Fikra za Woddis ni tofauti na za wasomi hawa wengine kwa sababu anasisitiza kwamba tabaka linaloongoza mapinduzi ya kijamii ni la wafanyakazi ambao 'wametayarishwa' na mfumo wa uzalishaji mali kutekeleza jukumu hili. Frantz Fanon kwa upande wake anachukulia mafalahi ndio wanaoongoza mapinduzi katika bara la Afrika. Woddis anatoa mifano mbalimbali kupinga dhana hiyo. Debray katika <u>Strategy for Revolution</u> anaamini kuwa ni kundi dogo la watu waliojitolea analoliita'foco' linaloweza kuongoza vita dhidi ya wanyonyaji. Wafanyakazi wa mijini hawapewi dhima yoyote na Debray na Marcuse.

Naye Ben Turok katika <u>Revolutionary Thought in the 20th Century</u> amezikusanya fikra mbalimbali kuhusu mapinduzi. Baadhi ya fikra hizi ni za Marx na Engels katika <u>The Communist Manifesto</u> ambapo wafanyakazi wa mijini wanapewa dhima ya kuyaunganisha matabaka yanayonyanyaswa ili kuyafanya mapinduzi yafaulu. Makala mbalimbali kama ya Lenin, Machel, Le Duan na Cabral yamekusanywa humu. Katika makala yake <u>On the Weapon of Theory</u>, Amilcar Cabral amesisitiza umuhimu wa nadharia ya kimapinduzi katika jitihada za ukombozi.

Theda Skocpol katika State and Social Revolution amesema kwamba mapinduzi ya kijamii ni matukio ya ghafla ambayo yanalifanya tabaka moja kuchukua uongozi wa kisiasa na kuleta mabadiliko katika mfumo wa uzalishaji mali (1979:4). Ili kubainisha kwamba muundo wa mfumo wa uzalishaji mali ndio kitovu cha mapinduzi, Skocpol amejadili mapinduzi ya Ufaransa, Urusi na Uchina.

Ingawa wataalamu hawa wanazungumzia muktadha tofauti na ule tunaouhakiki fikra zao ni nzuri. Hali zinazoivisha mapinduzi na nguvu zinazoyaleta mapinduzi haya hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Lakini tuchunguzapo kwa undani tutaona kuwa kuna hali za kijumla na hali za kibinafsi. Fikra za kijumla zilizotajwa na baadhi ya magunge zitatufaa kwa kadri zitakavyotumulikia maudhui ya mapinduzi katika riwaya tunazozihakiki.

Tasnifu ya Kamunde, M.E (1983) ya M.A. imejadili 'unyonge' wa kiuchumi uliopo katika tabaka la chini na 'unyonge' wa tabia katika tabaka la juu kama ujitokezavyo katika Utengano (1980), Asali Chungu (1978) na Dunia Mti Mkavu (1980). Madhumuni ya Kamunde yalikuwa kuwajadili wahusika mbalimbali kwa kadri wanavyobainisha 'unyonge' wao. Kauli ya Kamunde ni kwamba Said Ahmed Mohamed :

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

> ameeleza kinagaubaga juu ya mifumo itumiwayo kuwadhalilisha wanyonge; mifumo hiyo ikiwa ni siasa, uchumi na mas-ala ya jamii.[2]

Usemi huu ni wa kijumla mno kwa sababu Said Ahmed anajadili mfumo maalum wa kiuchumi. Katika kuyajadili maudhui ya mapinduzi tutauweka 'unyonge' huu katika muktadha wa kiuchumi na kijamii ili tubainishe nafasi yake katika kuyaleta mapinduzi ya 1964. Kamunde amehakiki riwaya tatu za Said Ahmed ilhali sisi tutawahakiki waandishi watatu wa visiwani Zanzibar.

Mazrui, A. (1984) ameitumia nadharia ya Ki-Marx katika uhakiki wake wa Dunia Mti Mkavu. Amesema kuwa:

> Dunia Mti Mkavu (1980) ya S.A. Mohamed kufikia sasa inawakilisha kilele cha maendeleo ya riwaya ya Kiswahili katika uchanganuzi wake wa kisiasa na kijamii kuhusu mabadiliko na upembuzi wa jamii za Kiafrika chini ya utawala wa kiistiimari.[3]

Makala haya yatatufaa kwa sababu yamegusia suala la mapinduzi tunalolihakiki. Aidha, mwandishi huyu

ameonyesha kuwa nadharia ya Ki-Marx inaweza kutumiwa katika uhakiki wa maandishi ya Said Ahmed.

Tasnifu ya Kitsao, J. (1982) ya Ph.D. imejadili maudhui mbalimbali yapatikanayo katika fasihi ya Kiswahili. Amezihakiki riwaya fulani akitumia uchambuzi wa kitarakimu. Ameonyesha kuwa kila mwandishi huwa na mtindo ambao aweza kunasibishwa nao. Kitsao amesema kwamba:

> ..... Ingawa Utengano, Asali Chungu, na Dunia Mti Mkavu zapendeza hasa kuhusiana na matumizi ya lugha, zimechukua mfano wake katika Nyota ya Rehema hivi kwamba hatimaye kazi hizi zaonekana kana kwamba ni ..... miigo, hasa kimaudhui na kifani.[4]

Kauli hii itajadiliwa kwa kadri inavyohusu maudhui ya mapinduzi.

Mapitio ya Khatib, M.S. (1983) kuhusu Kuli na ya Senkoro, F.E.M.K. (1984) kuhusu Kasri ya Mwinyi Fuad yatazingatiwa katika utafiti wetu. Hali kadhalika makala ya Mlacha, S.A.K. (1984) yanayozungumzia kwa kifupi riwaya za visiwani (1970 - 1980) na ujenzi wa jamii mpya yatatiliwa maanani kwa sababu amegusia riwaya zinazohakikiwa.

Maughan - Brown (1985) amejadili maudhui ya vita vya Mau Mau kama yajitokezavyo katika kazi za historia na za fasihi. Ameonyesha vile tukio la kihistoria linavyoweza kuhuishwa kifasihi na kwa kufungamanishwa na itikadi maalum. Amejishughulisha na kazi za kifasili zinazohusu vita vya Mau Mau ilhali sisi tunachunguza riwaya za Zanzibar zenye maudhui ya mapinduzi. Utafiti wa Maughan - Brown madhali umejikita katika uhusiano wa historia na fasihi utatufaa kwa sababu uchunguzi wetu vile vile unajaribu kubainisha uhusiano wa aina hiyo.

## 1.6 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO HILI

Sababu yetu kubwa ya kulichagua somo hili inatokana na imani yetu kwamba kuna uhusiano mkubwa baina ya sanaa na matukio ya kijamii. Kwanza, msanii ni mmoja katika jamii ya binadamu wenye ubunifu na uwezo wa kuufurahia ubunifu huo. Hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake kwa sababu ana maslahi katika jamii hiyo. Pili, kazi yake ni kiungo chake na jamii anayoilenga. Msanii hutarajia kwamba atakuwa pamoja na hadhira yake kihisia na kwa hivyo hujitahidi kuufanya umbuji wake uziteke hisi za hadhiria yake. Tatu, kazi ya sanaa ina taathira kwa wana jamii - hutilia nguvu au hudhoofisha mawazo yao, matarajio yao na hofu zao (Vasquez, A.S. 1973: 112-113). Jamii ndiyo impayo ilhamu msanii

akasanifu hasa ikiwa inaonyesha mguso iupatao kutokana na sanaa yake. Vasquez ameligusia jambo hili asemapo:

> Kwa namna fulani kila jamii hupata sanaa inayoistahiki kwa sababu ya sanaa iipendeleayo au iivumiliayo na kwa sababu wasanii wakiwa watu katika jamii huumba kutegemea uhusiano walionao na jamii hiyo.[5]

Tungeweza kuongeza kuwa wasanii aghalabu huumba vile vile kutegemea hali halisi ipatikanayo katika jamii waizungumziayo. Hali hizi zinamhusu binadamu na mazingira yake. Binadamu anapozifinyanga na kuzielewa hali hizi huku akiwa anakinzana nazo basi huwa yuaiandaa historia. Kwa hivyo, basi, matukio ya kihistoria hutokana na jitihada za binadamu apambanapo na mazingira yake pamoja na binadamu wenzake.

Ernest Fischer (1959) ameonyesha vile taathira za kijamii na kihistoria zinavyoielekeza fasihi kwa kuwa anazingatia kwamba fasihi ina uhai na hutoa mdundo wenye misingi yake katika jamii. Kwa hivyo, kadri jamii inavyopiga hatua ndivyo fasihi inavyochukua mkondo unaoafikiana kwa kiasi fulani na yale yatukiayo katika jamii. Ngugi - wa - Thiong'o

(1981:6) amesema:

> Kwa sababu ya hali yake ya kijamii, fasihi ..... inaelekezwa na nguvu na msukumo wa historia ya jamii, haiwezi kujiepusha ..... na uchumi, siasa, tabaka, rangi au kile akiitacho Achebe 'masuala muhimu zaidi ya wakati huo' kwa sababu masuala hayo muhimu inayojishughulisha nayo hutokea katika muktadha wa kiuchumi, kisiasa, kitabaka na rangi.[6]

Hali hii huwa bayana zaidi pale ambapo, katika maendeleo ya jamii, pametokea jambo kubwa linaloyabadilisha, kwa kiasi fulani, maisha ya jamii ihusikayo. Kwa mfano, huku Kenya vita vya Mau Mau viliotesha na kushamirisha fasihi iliyofichua hali za kisiasa, kiuchumi na kijamii zilizovifanya vita hivyo kuwa jambo la lazima. Aidha, fasihi hiyo imejaribu kuitanabahisha hadhira yake kuhusu matumaini ya wapigania ukombozi na ni kwa namna gani matumaini hayo yalifikiwa au yalisalitiwa.

Mapinduzi ya Urusi ya Oktoba 1917 yalikuza kizazi kipya cha wana-fasihi na yakatoa mwelekeo fulani katika fasihi ya Kirusi. Mapinduzi ya kisiasa na kiuchumi yakazua mapinduzi katika fasihi.

Maandishi ya Nikolai Ostrovsky (1904-1936) How the Steel was Tempered na ya Maxim Gorky (1949) Mother yakawa ni baadhi ya yale yakubalikayo na yastahiwayo. Fasihi 'ikashauriwa' ijikite katika uyakinifu wa kijamii ili isadie katika uendelezaji wa mapinduzi hayo. Jarida la 'Soviet Literature' latwambia:

> Mapinduzi makuu ya kijamaa yaliyofaulu Urusi Oktoba 1917 yaliipa fasihi kongwe nguvu mpya, yakamwaya damu ya uhai katika fasihi ambazo zilikuwa ndio mwanzo zinachipuka wakati huo na yakazipa uhai nyingine mpya.[7]

Fasihi ilipewa nafasi kubwa katika uendelezaji wa mapinduzi.

Huko Cuba mapinduzi ya 1959 yaliimarisha aina fulani ya fasihi kiasi cha kumfanya Fidel Castro (1961) awashauri maulama hivi:

> Nanyi mna fursa ya kuwa zaidi ya hadhira, muwe waumbaji katika mapinduzi, mwandike kuyahusu, mjieleze kwayo.[8]

Mujaradi wa Tanzania kutangaza Azimio la Arusha (1967) kulizuka fasihi iliyozama katika maudhui ya ujamaa uliopendekezwa na azimio hilo. Euphrase Kezilahabi akausaili ujamaa katika Kichwa Maji (1974),

Dunia Uwanja wa Fujo (1975), Gamba la Nyoka (1979). Ebrahim Hussein katika Mashetani(1971) na Arusi (1980) ameonyesha mikinzano ya kiuchumi, kijamii na kisaikolojia iliyoletwa na mfumo huo mpya.

Al'muradi pindi patokeapo jambo muhimu la kihistoria fasihi hulihifadhi kwa kulihuisha kisanaa. Vasquez, A.S. amelisisitiza jambo hili:

> Sanaa na jamii kwa hivyo bila shaka zimeungana: hakuna sanaa isiyoathiriwa na taathira za kijamii na hakuna sanaa ambayo kwa upande wake, imekosa kuiathiri jamii.[9]

Matukio ya kijamii huwa hayana mpango wowote bali yameingiliana, huku mengine yakiwa ghafi na mengine safi. Inambidi msanii ayatazame na kisha akate kauli kuhusu yale yafaayo kuwasilishiwa hadhira yake. Uchaguzi atakaoufanya utaelekezwa na falsafa yake ya maisha ambayo ndiyo msingi wa itikadi yake. Chambilecho Ngugi-wa-Thiong'o (1986:78):

> Jinsi mwandishi anavyouchora uhalisi wa maisha huathiriwa na falsafa yake ya kimsingi kuhusu maumbile na jamii na mbinu yake ya kupeleleza maumbile na jamii hiyo ....[10]

Jambo hili ndilo litakalomwelekeza msanii katika ubainishaji wa matukio kiuhusisho au kiutengano; katika utuvu au yakibadilika na kadhalika. Said Ahmed Mohamed amelisisitiza jambo hili asemapo:

> Mwandishi lazima awe na sifa na tabia ya upembuzi baina ya uzima na uoza. Mwandishi hawezi kuandika kinachomjia tu. Mwandishi anayekosa sifa hii ni 'mbuku' asiyechagua vya kutafuna au vya kumeza: yeye hufakamia tu, madhali ajua soko liko tayari kupokea uoza wake.[11]

Mwandishi atajiepusha vipi na tabia ya kufakamia? Uchaguzi na upembuzi utawezekana endapo atakuwa na itikadi itakayompambanulia mema na mabaya. Itikadi hii ndiyo itakayomsaidia kumaizi yale yenye tija na yenye upotovu.

Waandishi wa visiwani Zanzibar tuliowachagua wamehitari kuyasawiri maudhui ya mapinduzi ya 1964. Kitendo hiki bila shaka kimetokana na itikadi kuwa fasihi ina dhima ya kuyaendeleza mapinduzi yenye manufaa kwa umma.

Ingawa tunayajadili mapinduzi ya visiwani Zanzibar tunaamini kuwa fasihi ina mapana na marefu yake. S.A. Mohamed (1980:xvii) amelitaja hili:

> Tungo zangu zinaibuka na hali halisi
> ya jamii lakini si jamii fulani finyu;
> ila zinagubika jamii pana ya dunia
> yenye madhila na mateso kwa wanyonge na
> kibri kwa watukufu.[12]

Lakini, aghlabu, kabla msanii hajazama katika uhalisi wa kilimwengu, chanzo chake kuwa ni jamii fulani finyu. Hali zilizoikumba jamii hiyo hupewa muktadha mpana ili zizigubike jamii pana. Hili ni kwa sababu msanii ni mja wa wakati wake, jamii yake, utamaduni maalum na tabaka maalum. Aidha, sanaa yote nzuri huibuka katika hali fulani mahsusi lakini ina matokeo ya kilimwengu (Vasques, A.S. 1973:114). Waandishi tutakaowahakiki huenda wameyatumia mapinduzi ya 1964 kama kielelezo cha yale yawezayo kutokea kokote kwenye madhila.

Kwa kadiri tujuavyo sisi hakuna utafiti uliofanywa kuhakiki kizazi hiki kipya cha waandishi kinachowakilishwa na Shafi Adam Shafi, Said Ahmed Mohamed na Mohamed Suleiman Mohamed. Kizazi hiki kimejitenga na watangulizi wao kama M.S. Abdalla na M.S. Farsy kwa kuifinyanga historia kisanaa. Tumewachagua ili tuwape nafasi wanayoistahiki katika fasihi ya Kiswahili.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Nadharia ni kigezo kinachotumiwa katika kutathmini jambo na aghalabu hubadilika kutegemea yule anayetathmini na yale anayotathmini.

Kuna nadharia mbalimbali ambazo hutumiwa na wahakiki katika uhakiki na unakidi wa kazi ya sanaa. Kwa mfano, kuna nadharia inayoihakiki kazi ya sanaa kwa kuzingatia kuwa sanaa ni umithilishaji wa hali fulani ulimwenguni. Nadharia hii ya umithilishaji ndiyo iliyotumiwa na Plato katika kuelezea nafasi ya wasanii katika taifa lake la kidhahania. Plato (katika Lodge 1972:6; Aristotle, Horace,Longinus 1965:11-12) alisema kuwa sanaa inamithilisha kile kinachoonekana na msanii na wala si kile ambacho ndicho cha asili, yaani Dhana ya daima dawamu isiyobadilika. Plato alisema sanaa imetengwa mara dufu kutoka hali ya asili na kwa hivyo haina manufaa makubwa. Katika Aristotle, Horace, Longinus (1965:13) alisisitiza kwamba msanii husanifu ikiwa amepandwa na jadhiba na kuwa hawezi kutunga akiwa na akili zake razini.

Aidha, kuna tahakiki zinazozingatia mtindo wa kazi ya sanaa. Tahakiki hizi hazijishughulishi na maudhui bali hujikita katika uchambuzi wa kitarakimu. Huchunguza miundo ya maneno, sarufi na

maana. Uchunguzi wa aina hii unatokana na imani kwamba kitovu cha kazi ya sanaa ni mtindo - kuwa mtindo ndio unaosheheni maudhui (Trotskii 1971:164). Jukumu la mhakiki anayetumia nadharia hii ni uchambuzi wa kimaelezo na kitarakimu juu ya msamiati, sentensi, kuhesabu takriri za vokali na konsonanti, mizani na kadhalika. Uhakiki wa aina hii una manufaa yake katika ufichuaji wa ujumi wa kazi ya sanaa. Hata hivyo, sanaa imethibitishwa kuwa chimbuko lake si Neno ni Kitendo (Fischer 1959,Vasquez 1973). Uhakiki wa kimtindo basi kwa kawaida hupuuza kipengee muhimu sana cha sanaa nacho ni maudhui.

Nadharia inayofungamanisha fasihi na jamii ndiyo iliyoshika sana, hasa katika 'Ulimwengu wa Tatu.' Hii ni kwa sababu inaonyesha kuwa fasihi ni kielelezo cha hali halisi na inachukuliwa kama zana mojawapo ya kujihami dhidi ya mazingira makali. Nadharia hii iliyonidhamishwa na Hippolyte Taine (1828-1893) inasisitiza kuwa fasihi ni taasisi ya jamii. Msanii anachukuliwa kama mmoja katika jamii na mwenye nafasi yake katika jamii hiyo. Huwa ameilenga hadhira fulani (hata ingawa nyakati nyingine hadhira hiyo iko katika kiwango cha mawazo tu). Fasihi, kufuatana na nadharia hii ya kijamii, yasemekana kuwa ina jukumu kwa jamii (Wellek na Warren 1956:94).

Jukumu hili liko katika viwango viwili. Kiwango cha kwanza ni cha mtu binafsi na kiwango cha pili ni cha jamii kwa jumla. Kazi nzuri ya sanaa huiathiri nafsi ya hadhira yake na kuziteka hisi zake. Mara nyingi tumepata kuwaona watu wakitabasamu, wakipiga vifijo, wakicheka na kulia wanaposhuhudia kazi ya sanaa. Hii ni kwa sababu umbuji wa msanii mzuri huzishambulia nafsi za hadhira yake na ikazitekenya ili hadhira hiyo iwe pamoja na msanii kihisia.

Katika kiwango kingine fasihi inachukuliwa kama chombo kimojawapo kinachomsaidia binadamu kujielewa na kuyaelewa mazingira yake. Fasihi inakuwa ni zana muhimu ya kumkomboa mja kutokana na madhila yaliyosababishwa na waja wenziwe au na maumbile makali.

Uhakiki tunaoufanya unahusiana na suala la 'fasihi na jamii.' Nadharia zinazozingatia fasihi kama 'umithilishaji' wa 'Dhana' iliyotengwa mara dufu kutoka kwa msanii au 'mtindo' haziwezi kuwa na manufaa katika utafiti wetu. Kwa hivyo, msingi wa kinadharia unaotufaa zaidi ni ule unaojikita katika uhakiki kijamii.

Uhakiki wa fasihi kijamii una mielekeo tofauti tofauti. Katika tasnifu hii tunatarajia kuitumia nadharia ya uhakiki kijamii inayoelemea katika

mtazamo wa Ki-Marx. Uchaguzi wetu unatokana na sababu tatu. Mtazamo wa fasihi Ki-Marx unaonyesha uhusiano wa fasihi na uzalishaji mali. Hili ni jambo linaloingiliana vema na utafiti wetu. Mapinduzi ya kijamii yatokeapo na kufaulu, mfumo wa uzalishaji mali aghalabu hubadilika na taasisi za kitamaduni - fasihi ikiwemo huchukua mkondo mwingine. Yaani, kadiri mfumo wa uzalishaji mali unavyobadilika ndivyo fasihi nayo idhihirishavyo mabadiliko hayo katika tanzu zake zote. Mabadiliko hayo yanaelezwa vema na mtazamo wa Ki-Marx. Katika dibaji ya A contribution to the Critique of Political Economy, Karl Marx amesema:

> Mfumo wa uzalishaji mali katika hali halisi ya maisha ndio unaozielekeza hali za kijamii, kisiasa, na kiulama kwa jumla.... Si urazini wa watu unaozielekeza hali zao, bali, kinyume na hili, hali zao katika jamii ndizo zinazouelekeza urazini wao... Mabadiliko ya msingi wa kiuchumi yatokeapo, muundo mzima wa taasisi za jamii hubadilika.[13]

Tasnifu yetu inachunguza maudhui ya mapinduzi katika riwaya za visiwani Zanzibar. Kusudi letu ni kubainisha kuwa mfumo wa uzalishaji mali ulipobadilika

visiwani Zanzibar fasihi ilichukua mkondo mwingine na ilijaribu kuelezea hali iliyokuwepo kabla ya mabadiliko hayo. Hakuna nadharia nyingine inayoelezea vema uhusiano huu baina ya mfumo wa kiuchumi na fasihi isipokuwa ile iliyojikita katika mtazamo wa Ki-Marx.

Pili, suala la jamii kubadilika kwa njia ya mapinduzi na sababu za hatima hiyo limeelezwa kutegemea nadharia hii. Kulingana na mtazamo huu jamii za kilimwengu zimepitia hatua mbalimbali za kihistoria kwa wakati tofauti. Hatua hizi zinahusiana na njia za uzalishaji mali. Hatua ya kwanza ilikuwa ni mfumo wa ishitiraki. Katika mfumo huu binadamu aliishi kwa ushirika huku kila mtu akifanya kazi itakayoifaidi jamii. Jamii zilipoendelea, zikaanza biashara ndogondogo na mataifa jirani. Mara uzalishaji mali ukalenga katika mahitaji ya jamii na biashara. Mali yakatengwa na wale walioshiriki katika kuyazalisha. Kabla ya biashara hizi kuanza, mateka wa kivita waliuawa. Lakini mahitaji ya kibiashara yalilazimisha kuwepo kwa wafanya-kazi wa ziada ili kutosheleza mahitaji ya uzalishaji mali. Mateka wakafanywa watumwa - wakazalisha mali kwa ajili ya uhai wao na kwa manufaa ya bwana zao (Babu, A.M.

1981:21). Lakini mfumo huu ulianza kujikinza wenyewe. Ikawa ghali kuendelea kuwa na watumwa kwa ajili ya ghasia na fujo za mara kwa mara. Mfumo wa uzalishaji mali ukabadilika ukawa wa kibwanyenye. Mfumo wa kibwanyenye ulijitambulisha kwa ubadhirifu na ufujaji miongoni mwa tabaka-tawala. Kaida ya tabaka hili ikawa ni kustaladhi katika ubozi. Maisha ya tabaka hili yakawa ni maisha ya matumizi tu bila kushiriki katika uzalishaji mali. Jambo hili lilizuia maendeleo ya tabaka la kibepari lililokuwa limepamba moto na lililotamani kujitanua. Tabaka hili la kibepari lilikuwa la kimapinduzi. Tumeliita hivi kwa sababu lilileta mfumo mpya wa kiuchumi - mfumo wa kibepari. Hili ni jambo la kawaida kwa sababu:

> Ni jambo la kihistoria lisiloepukika kwamba nguvu za kisiasa, hata zikiwa na uwezo mkubwa wa kukandamiza, endapo zitakuwa kizuizi cha maendeleo ya kawaida ya kiuchumi, huondolewa na nguvu mpya zinazowakilisha maendeleo zikachukua hatamu.[14]

Mfumo wa kibepari umefikia kilele chake katika uistiiimari. Nayo mataifa ya Kiafrika yakajikuta katika mkondo huu wa ubepari wa kilimwengu. Lakini

kama mifumo hiyo mingine iliyotangulia, mfumo wa kibepari unajikinza wenyewe. Umesababisha kuwepo kwa wafanya-kazi wengi wanaolitumia jasho lao kwa manufaa ya mabepari. Hali hii imeleta mikinzano mikali sana ya kitabaka na hatima yake imekuwa ni mapinduzi na mfumo mpya wa kijamaa. Ni mataifa machache sana yaliyoifikia hali hii.

Itabainika kuwa mtazamo wa Ki-Marx ndio unaofaa zaidi kuelezea mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi kwa njia ya mapinduzi katika taifa la Zanzibar.

Sababu ya tatu iliyotuelekeza katika kuuchagua mtazamo huu ni kwamba waandishi wa riwaya tunazozihakiki wameandika wakati nchi yao ikiwa imefuata mfumo wa kijamaa. Katika uchunguzi wetu tunanuia kuhakiki hali iliyoletwa na mapinduzi kama ijitokezavyo katika riwaya tunazozichambua. Mtazamo wa Ki-Marx utakuwa kigezo kizuri cha kuipimia hali hiyo na kuwalinganisha waandishi hawa.

Glicksberg (1976:70) amesema hivi kuhusu uchambuzi wa Ki-Marx:

> Uhakiki wa fasihi Ki-Marx huchunguza athari za kiuchumi katika wakati fulani kihistoria na husisitiza mtafaruku wa kitabaka ambao hujitokeza kutokana na siasa hizo za kiuchumi.[15]

Msimamo wa mtazamo huu ni kuwa hali zozote katika jamii (fasihi ikiwemo) hutokana na mfumo wa kiuchumi ingawa kama Engels alivyomwambia Heinz Starkenburg (katika Marx-Tarehe haikutolewa(a):392) hali hizo "haziketi" zikisubiri msukumo wa mfumo wa kiuchumi bali daima ziko katika kuathiriana na kujiendeleza.

Kulingana na ujumi wa Ki-Marx fasihi ni kielelezo cha matukio halisi katika jamii na inapaswa ijikite katika uyakinifu. Uyakinifu katika fasihi ni masimulizi ya kweli na ya wazi, yenye wahusika wanaokubalika, na waliomo katika hali halisi (Ngara 1985:14). Kwa hivyo, ili msanii awe na uyakinifu katika kazi zake hana budi kuielewa historia ya jamii yake na muundo wa jamii hiyo. Hii ni kwa sababu wahusika hawaumbwi katika ombwe bali hutokana na hali halisi za maisha. Hali hizi nazo ni matokeo ya kihistoria.

Uyakinifu unaosisitizwa na mkabala wa Ki-Marx ni ule wa kijamaa. Dhana ya uyakinifu wa kijamaa iliundwa na Kongamano la waandishi wa Taifa la Urusi. Uyakinifu huu unamtarajia msanii auwasilishe uhalisi wa maisha katika hali yake ya kimaendeleo na kimapinduzi kikweli na kwa kuzingatia historia (katika Baxandall 1972:241). Nayo historia

yatufundisha kwamba jamii za kilimwengu daima ziko mbioni kuiacha hali dhaifu na kujaribu kuukaribia utu kamili. Mikinzano yoyote ya kijamii huchangiza katika kuyaleta mabadiliko hayo. Fasihi yakinifu ya kijamaa itazingatia hili. Kama asemavyo Fadeyev:

> Kwa mujibu wa mkabala wa Ki-Marx na Ki-Lenin, uyakinifu wa kweli wa sanaa ni kazi ya ubunifu inayoukaribia ukweli wa kihistoria kama iwezekanavyo na iwezayo kuwakilisha mielekeo ya kweli ya maendeleo katika mapambano dhidi ya nguvu zilizozeeka.[16]

Msingi wa nadharia ya Ki-Marx kuhusu uyakinifu ni kwamba sanaa yakinifu ni ile imulikayo ukweli wa maisha katika upana na utatanishi wake. Naye mwandishi azingatiaye uyakinifu wa kijamaa hudhihirisha kuafikiana kwake na matakwa ya wafanya-kazi katika jitihada zao za kujikomboa na kuunda taifa la kijamaa. Kwa hivyo uyakinifu wa kijamaa umelenga wakati ujao (Fischer 1959:108-113; Lukacs 1963:99; Bisztray 1978:55). Kiwakati, basi, uyakinifu wa kijamaa husisitiza uhusiano wa jana, leo na kesho. Ili kuifikia hiyo kesho yenye utu, mkabala huu huonyesha mikinzano ya kijamii na asili

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

yake na hujitokeza katika uteteaji wa wafanya-kazi na mafalahi.

Ni bayana kwamba uyakinifu wa kijamaa ni wa kimapinduzi kwa sababu huipa fasihi jukumu la kushiriki katika kuutayarisha umma kwa minajili ya kujikomboa na kuanzisha taifa la kijamaa. Mhakiki aliyejitwika wajibu wa kuichambua na kuinakidi kazi ya sanaa kwa kuzingatia mtazamo wa Ki-Marx hana budi kuihakiki kazi hiyo kwa mujibu wa uyakinifu wa kijamaa.

Fauka ya hayo, hana budi kujitoma katika elimu jamii na historia. Hii ni kwa sababu, kama tulivyotangulia kusema, kazi za sanaa zina uhusiano na jamii fulani na historia yake. Dhima ya mhakiki, kwa hivyo, haiishii katika uchambuzi wa kazi anazozihakiki bali humlazimu aielewe jamii iliyoikuza kazi ile na iliyompa ilhamu msanii aweze kubuni. Lowenthal (1957:x) anatwambia:

> Ni jukumu la mhakiki wa fasihi kijamii kuzihusisha tajiriba za wahusika wa mwandishi na hali za kihistoria walimoibuka.[17]

Hali kadhalika, Kohn Bramstedt naye anatutahadharisha kwamba:

> Ni mtu yule ... aliye na utambuzi wa muundo wa jamii kutoka asilia nyingine mbali na ile ya kifasihi tu awezaye kugundua kama ... hali fulani za kijamii na tabia zake zimehuishwa katika riwaya.[18]

Kwa hivyo, tutaitumia nadharia tuliyoichagua siyo katika uhakiki wa riwaya tu bali pia katika kuielezea historia ya Zanzibar kabla na baada ya mapinduzi ya 1964. Msingi huu wa kihistoria ni muhimu sana katika utafiti wetu kwa sababu unaziweka riwaya tunazozihakiki katika muktadha maalum Ki-mahali na Ki-wakati. Utatusaidia katika kuzitathmini kwa mujibu wa uyakinifu wake. Chambilecho Ngara (1985: 29):

> Ikiwa tutaelewa na kutathmini chimbuko, maendeleo, shughuli na mitindo ya fasihi ya taifa hatuna budi kuitazama fasihi hiyo katika muktadha wa historia na mikinzano ya jamii hiyo na katika muktadha wa itikadi zilizoko....[19]

## 1.8. NJIA YA UTAFITI

Huu ni uhakiki wa kifasihi na kwa hivyo tutasoma maandishi mbalimbali yanayohusiana na uhakiki wa

fasihi. Tutaitumia nadharia ya kijamii na, kama tulivyotangulia kusema, tutajikita katika mtazamo wa Ki-Marx. Itatubidi tusome makala na vitabu vinavyohusiana na nadharia ya fasihi kijamii na mtazamo wa fasihi kufungamana na ujumi wa Ki-Marx.

Tumewachagua waandishi maalum tutakaowahakiki. Tutavisoma vitabu vyao kwa kituo. Mbali na Shafi Adam Shafi, Said Ahmed Mohamed na Mohamed Suleiman Mohamed, tutawasoma waandishi wengine wa visiwani Zanzibar. Tunatarajia kuyachanganua mawazo ya wasanii hawa na kuyalinganisha na uhalisi wa maisha ambamo sanaa hiyo imeota. Hatuna budi basi kuisoma historia ya Zanzibar na muundo wake wa kiuchumi na kijamii kabla ya mapinduzi. Kwa vile tunayahakiki maudhui ya mapinduzi itatupasa tusome nadharia ya mapinduzi kama ilivyoelezewa na baadhi ya wataalamu wa siasa na uchumi.

Haitakuwa muhimu kwetu kuwafahamu waandishi tunaowahakiki kwa kuwa kama asemavyo Plekhanov (katika Arvon 1973:12):

> Kwa sababu kazi ya sanaa ni ....
> matokeo ya uhusiano wa kijamii,
> inawezekana kuifasiri kutoka lugha
> ya kisanii hadi lugha ya elimu-jamii.
> Kumfahamu msanii au mwandishi mwenyewe

> si muhimu katika kuielewa kamili
> kazi ya sanaa au fasihi kama
> ilivyo muhimu saikolojia ya jamii
> anayoifuata pamoja na wenzake.

Jambo muhimu si kuzifahamu tabia za waandishi tunaowahakiki bali kuufahamu mfumo wanaouzungumzia katika kazi zao.

## 1.9. TANBIHI

1. Trotskii, L. (1971) Literature and Revolution. The University of Michigan Press, U.S.A. uk. 230.

2. Kamunde, M.E. (1983) "Kilio cha Wanyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi, uk. 124.

3. Mazrui, A (1984) 'Dunia Mti Mkavu: A Literary Treatise on Marxism.' Makala katika Jarida la 'Kiswahili' Juzuu la 51/1, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam uk. 198.

4. Kitsao, J. (1982) 'An Investigation of Themes in Swahili Literature and an application of Stylostatistics to Chosen Texts.' Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Nairobi. uk. 117-118.

5. Vasquez, A.S.(1973) Art and Society. Monthly Press Review. New York uk. 112.

6. Ngugi wa Thiong'o (1981) Writers in Politics
Heinemann Publishers
Nairobi. uk. 6

7. 'Soviet Literature' Sehemu ya 1 (1968)
Jarida lililochapishwa na
Union of Writers of the
USSR. uk. 150.

8. Baxandall, L. (Mhariri) (1972) Radical
Perspectives in the Arts.
Penguin Books. Middlesex.
uk. 276.

9. Vasquez, A.S. Kama hapo juu uk. 113

10. Ngugi-wa-Thiong'o (1986) Decolonising the mind:
The Politics of Language
in African Literature
James Currey Ltd. London.
uk. 78.

11. Mohamed, S.A. (1983) 'Kupatana na riwaya zangu'
Mwamko 2. Jarida la Chakina,
Chuo Kikuu cha Nairobi.
uk. 42.

12. ----------------- (1980) 'Sikate Tamaa' Longman
Nairobi. uk. xvii.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

13. Marx, K. (Tarehe Haikutolewa(a) Selected Works Vol. I. International Publishers. New York. uk. 356.

14. Babu, A.M. (1981) African Socialism or Socialist Africa. Tanzania Publishing House. Dar-es-Salaam. uk. 23

15. Glicksberg, C.I. (1976) The Literature of Commitment. Associated University Press. London uk. 70.

16. Baxandall, L. Kama hapo juu. uk. 241

17. Lowenthal, L. (1957) Literature and the Image of Man. Beacon Press Boston uk. x.

18. Imenukuliwa na Rene Wellek na Austin Warren (1956) Theory of Literature. Penguin Harcourt uk. 104.

19. Ngara, E. (1985) Art and Ideology in the African Novel. Heinemann. London. uk. 29

# SURA YA PILI

## 2.0 MUUNDO WA MFUMO WA UZALISHAJI MALI

### 2.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tunanuia kujadili muundo wa mfumo wa uzalishaji mali uliokuwepo visiwani Zanzibar kabla ya mapinduzi kama unavyojitokeza katika riwaya tunazozihakiki. Tusemapo mfumo wa uzalishaji mali tunamaanisha nyenzo za uzalishaji mali na uhusiano wa watu katika uzalishaji mali.[1] Tutazijadili nyenzo hizo na vile zilivyomilikiwa huku tukionyesha nafasi ya historia ya ukoloni katika umilikaji huo. Tutachunguza muundo wa kijamii katika riwaya hizi. Baada ya kuzungumzia nafasi za elimu na kazi miongoni mwa wenyeji wa visiwani kama vielelezo vya muundo wa mfumo wa uzalishaji mali, tutajadili pupa kama kipengee muhimu cha mfumo wa uzalishaji mali.

Lengo la sura hii ni kubainisha kwamba muundo wa mfumo wa uzalishaji mali ulikuwa ndio msingi wa mapinduzi ya visiwani. Tunadhamiria kuonyesha kwamba kitovu cha mapinduzi hakimo akilini mwa wahusika wa riwaya tunazozihakiki bali kitapatikana katika mfumo mzima wa uzalishaji mali.[2]

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

## 2.2. NYENZO ZA UZALISHAJI MALI

Waandishi wote wa visiwani wanaonekana kukubaliana kwamba nyenzo za uzalishaji mali kama ardhi na viwanda zilimilikiwa na mamwinyi na mabepari wa kigeni. Waliokuwa na ardhi walipata malighafi maridhawa na mtaji uliowawezesha kupata thamani ya ziada. Hali kadhalika waliokuwa na viwanda walipata thamani ya ziada iliyotumiwa katika upanuzi wa viwanda hivyo au kuanzisha vingine. Kulingana na nadharia ya Ki-Marx ya uchumi, kiasili ardhi na mtaji hazina thamani. Nyenzo hizi hupewa thamani na nguvu za binadamu. Kwa hivyo, ingawa mamwinyi na mabepari walikuwa na mashamba na mtaji, palihitajika watu wangaliotumia nguvu zao ili matajiri wapate thamani ya ziada.

Katika riwaya hizi tunayaona mashamba makubwa ambako wafanyakazi wameajiriwa au kukodi vikataa. Hali kadhalika, viwandani na bandarini wafanyakazi wameenea wakiuza nguvu zao kwa mnunuzi anayezitaka. Riwaya ya <u>Nyota ya Rehema</u> inapoanza, tunatangaziwa kwamba wakulima wamefika kuleta magunia na vipeto vya mazao yao kama zawadi kwa mwenye shamba Fuad. Wanatahadharishwa wasichelewe kuleta kodi ya vikataa walivyokodi (uk. 1). Inavyobainika hapa ni kwamba Fuad anatarajia alipwe kodi na kisha apewe mazao

kutokana na vikataa alivyokodisha.

Dunia Mti Mkavu inatuonyesha kuwa Hamoud, babake Fauz, anamiliki ardhi kubwa ambayo wahusika kama Fumu, Simai, Hassani na kadhalika wanaihitaji kwa uhai wao. Hawa mafalahi[3] wamekodi vikataa shambani humo. Kwa vile Fauz anajua vikataa hivi ni uti wa mgongo wa Fumu haoni ugumu kujaribu kumfunga shemere Fumu kwa vitisho ili ampate Masika (mpenzi wa Fumu). Fumu anaonywa:

> Tokea leo, vipando hivi unavyovipanda ardhini petu si vyako. Na kuanzia sasa, huruhusiwi kulima katika shamba hili la Hamoud bin Said. Huruhusiwi kulima wala kupanda chochote. (uk. 9).

Tukimgeukia Shafi katika Kasri ya Mwinyi Fuad, tunakumbana na shamba kubwa lenye fahari la Malik. Shamba hili lenye mikarafuu, matunda, na mpunga linaweza kuwekwa sambamba na lile la Fuad tulilolitaja hapo juu. Shamba la Fuad la Mbiju lilikuwa na mtelemko wa mabonde yaliyojaa mibuni, mpunga na mbayaya. Isitoshe, "Minazi iliumana kadri ya maili tatu mpaka ikafika karibu na baraste iliyoelekea mjini" Mwandishi anatutahadharisha kwamba ingawa shamba hili ni kubwa, ni sehemu ndogo

tu ya milki ya Fuad kwa sababu mzee Salim, babake Fuad, alikuwa na tamaa kubwa ya kulundika mali. Tamaa hii inabainishwa anapowatoza riba masikini na anapolifilisi shamba la Ramwe ambalo ni la babake Aziza.

Hata katika Asali Chungu, tumechorewa Zuberi, Mkuu wa Wilaya aliyeisahau dhima yake kwa wananchi. Zuberi amewakodisha masikini shamba lake kubwa. Katika kila hali, waliokodi wanatozwa malipo fulani ambayo yanapelekewa mamwinyi. Aidha wanawapelekea vyakula na kisha kufanya kazi mashambani mwao. Kodi hii inakusanywa na manokoa[4] ambao wanajiona kijonzi kana kwamba wamekaribiana kitabaka na mabwana wenye mashamba. Ujeuri wa manokoa unaweza kudhihirika katika maneno yafuatayo yaliyotolewa kwa bibi mmoja aliyeliliwa muhogo na migomba yake na wanyama wa Zuberi.

> Ondoka hapa! muhogo, muhogo; una muhogo na mgomba hapa wewe? Ng'ombe ni wa bwana, shamba ni la bwana. Pana hasara gani ng'ombe wake kula migomba iliyomo shambani mwake? (uk. 2-3).

Mantiki hii inadhamiriwa kuonyesha kuwa mafalahi kwa kila hali huwategemea mabwana wenye shamba. Jasho lao linawafaidi mamwinyi kwa sababu wanapata thuluthi

moja tu ya mazao. Zuberi anamwambia mzee Omari:

> Mara ngapi nimekwambia kuwa
> chochote unachopanda ardhini
> mwangu thuluthi mbili zangu...? (uk.21)

Kutokana na ukorofi na usafihi[5] wa aina hii tunaona kuwa uhusiano baina ya wale wanaomiliki ardhi unakinzana moja kwa moja na mafalahi wanaolazimika kuzitumia nguvu zao kwa manufaa ya mwamwinyi ili waendelee kuwa na vikataa walivyokodi. Si ajabu, basi, kuwasikia baadhi yao kama Sulubu katika Nyota ya Rehema wakikaidi kulipa kodi. Sulubu anadai kulifaidi jasho lake. Hata hivyo, unyonge wake unamlazimisha kuhamahama kutoka shamba moja hadi jingine.

Viwandani, Waafrika hawakupata nafuu. Katika riwaya ya Kuli, Shafi Adam Shafi anatusimulia hali ya wafanyakazi katika kampuni ya Smith Mackenzie. Smith Mackenzie ni kampuni ya mabepari wa kiingereza iliyomiliki gati ya Unguja, chini ya usimamizi wa Mr. (sic) George. Hali kadhalika, kampuni ya Kiingereza ya wakuza karafuu chini ya usimamizi wa Morarji ndiyo iliyowaajiri wachukuzi kama mzee Tindo. Katika Dunia Mti Mkavu tunaambiwa kwamba mabepari wa Kiingereza ndio wanaomiliki Bandari ya Unguja chini ya usimamizi wa Mr. (sic) Barnes. Unyanyasaji wa

wafanyakazi bandarini ndio chimbuko la mgomo tunaosimuliwa katika Dunia Mti Mkavu. Bandari hii inatekeleza wajibu wa kutengeneza thamani ya ziada kwa manufaa ya utawala na kampuni za kigeni kwa sababu kama asemavyo Mr. Barnes:

> Sio rahisi Mr. David (kuyaangalia maslahi ya wapagazi na makuli) hakutakuwa na faida kwa matajiri na wenye mali zao, nje na ndani ya nchi; tena, na hili ndilo jambo muhimu, kutakuwa hakuna maslahi kwa serikali ya Kiingereza, hasa kwa tatizo la kiuchumi linalokabili dola la kiengereza. (uk. 109).

Kwa hivyo umilikaji wa ardhi na viwanda ni sehemu muhimu ya uendelezaji wa ubepari wa kilimwengu. Utawala wa Kiingereza ulilinda hali hiyo ili ufaidike kiuchumi. Riwaya hizi zinatusimulia umwinyi wa Kiarabu ukienda sambamba na ukisaidiana na ubepari wa kimagharibi katika uporaji wa mtaji kutoka visiwani Zanzibar. Wenyeji wakawa watoa jasho ili kutengeneza thamani ya ziada kwa manufaa ya tawala za kigeni. Kimsingi, basi, umilikaji wa nyenzo kuu za uzalishaji mali kabla ya mapinduzi

umefungamana na ukoloni. Kwa vyovyote vile, hatuna budi kuchunguza asili ya ukoloni Zanzibar kwa sababu ndio kitovu cha migogoro mingi tunayokumbana nayo katika riwaya za visiwani.

## 2.3 UKOLONI VISIWANI ZANZIBAR

Waandishi mbalimbali wameujadili ukoloni. Brett (1972:vii) amesema kwamba ukoloni ni mfumo wa utawala ambao unapora haki na kuwakandamiza watu wengine. Hatimaye, watawaliwa hushindwa kujitegemea kiuchumi na kisiasa. Katika maelezo yake kuhusu maenezi ya ukoloni, Woddis (1972 (a):14) amesema kwamba ukoloni ni mfumo ambao kwao nchi moja huikandamiza nchi nyingine na kutwaa madaraka ya kutawala ili iwanyonye wenyeji kikamilifu. Utawala wa kikoloni huhakikisha kwamba maadili yake ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ndiyo yanayokubaliwa na kuenezwa. Kwa jumla, basi, tunaweza kusema kwamba ukoloni ni nchi moja kuivamia na kuimiliki nchi nyingine kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Kabla ya kuwasili kwa ukoloni visiwani Zanzibar, mataifa ya Kiafrika yalikuwa yameishi humo tangu zama za zama. Makazi ya mwanzo kabisa yalitokana na uhamiaji wa makundi mbalimbali ya watu wa kutoka bara karne nyingi zilizopita. Makundi haya yalingia humo nyakati tofautitofauti na kwa hivyo hayakuwa na umoja

wa kisiasa ambao ungeyawezesha kuyakabili mataifa ya kigeni (Lofchie 1965:24).

Takriban 500 BC, wageni wengi kama vile Waajemi, Wachina, Wafoeniki, Wayahudi na Waarabu walikuwa wakifanya biashara na mataifa ya Kiafrika. ambayo yalikuwa yakiishi mwambao wa Afrika ya Mashariki. Kufikia karne ya kumi na moja, kundi la Waajemi lilikata alaka na makao yao ya jadi huko Shiraz, Uajemi. Waajemi hawa walikuja na utamaduni wao ambao baadhi yake ulikubaliwa na wenyeji wa Unguja na Pemba. Baadaye kundi hili la Waajemi likawa haliwezi tena kutofautishwa na Waafrika kwa vile wote walivyofungamana kiutamaduni.

Taifa la kigeni lililoathiri sana historia ya visiwani Zanzibar baada ya kuimarisha ukoloni wake kwa mapana na marefu ni la Waarabu.[9]

Ukoloni wa Kiarabu visiwani Zanzibar wapaswa kutazamwa huku ukifungamanishwa na matukio ya Bara Ulaya hasa baada ya "Mapinduzi ya Viwanda." Huu ndio wakati ambapo watumwa walinunuliwa na kusafirishwa na vile vile malighafi nyingi ikahitajika katika utengenezaji wa bidhaa viwandani. Ingawaje Zanzibar yenyewe haikuwa na idadi kubwa sana ya watu ambao wangefanywa watumwa, palikuwa pahali pazuri pa kufanyia biashara kwa sababu ya bandari zake nzuri

zenye maji safi. Zanzibar vile vile ilipendeza kwa sababu ya kukaribiana kwake na mwambao wa Afrika Mashariki na usalama iliotoa dhidi ya makabila makali ya bara. Aidha, mikarafuu na minazi ilikua vema sana katika sehemu hiyo.

Mnamo 1741 aila ya Mazrui iliyokuwa ikitawala Mombasa ilikata alaka na utawala wa Omani. Muhammad Uthman Al-Mazrui, aliyeteuliwa na utawala wa Yarubi wa Omani ili awe wakala wao Mombasa, alikataa kuukubali utawala mpya wa Busaidi ukiongozwa na Ahmad Said al-Busaidi. Utawala wa Busaidi uliposhindwa kuichukua Mombasa kutoka kwa Wamazrui ukajiimarisha Zanzibar na kupafanya kituo muhimu kwa ajili ya biashara. Utawala wa Kisultani Zanzibar ukazama katika biashara ya watumwa na karafuu. Ikumbukwe kuwa ukuzaji wa karafuu kama anavyoeleza Jabir (1977:2-10) umefungamana na mahitaji ya enzi hii huko Ulaya na Bara Hindi. Mashamba makubwa ya karafuu yaliyotolewa kwa Waarabu yalihitaji wafanyakazi ambao waliletwa kwa nguvu kutoka visiwani na bara. Waafrika wenyeji wakatengwa pembezoni mwa ardhi yenye rutuba na wengine wakabaki katika mashamba ya Waarabu kama watwana na watumwa. Nao Waarabu wakajilimbikizia rasilmali nyingi hata wakajitokeza kama tabaka la matajiri.

Wahindi wengi walihamia Zanzibar biashara ya karafuu ilipoumana. Hawakujishughulisha sana na umilikaji wa mashamba hapo mwanzoni bali walizama katika usafirishaji wa karafuu kutoka visiwani hadi Bara Hindi.

Waingereza walijikita visiwani baada ya mataifa ya Ulaya kukutana katika kongamano la Berlin la 1884-1885 lililoigawa Afrika ili kuuhami utawala wa kibepari. Lenin (1939) ameonyesha kwamba ubeberu hautamani maeneo ya malighafi yanayojulikana tu bali hupania kunyakua ardhi kubwa kadri itakavyowezekana katika sehemu yoyote na kwa njia yoyote. Tumaini la ubeberu lilikuwa kwamba patapatikana malighafi na ardhi ambayo bado haijavamiwa.

Ni wazi kwamba ukoloni unatokana na kukua na kupanuka kwa ubepari ambao hufikia hatua ya kulazimika kuvuka mipaka ya nchi yake. Kinachoustawisha ukoloni ni uporaji wa thamani ya ziada. Thamani ya ziada hii hutokana na kunyanyaswa na kupewa mishahara midogo wafanyakazi, malighafi ipatikanayo kwa usahili na masoko yaliyo wazi na tayari kupokea vifaa kwa bei nafuu. Mambo haya ndiyo yaliyovifanya visiwa vya Zanzibar kinyang'anyiro kikubwa cha ukoloni wa Kiarabu

ukiungwa mkono na Waingereza.

Kujikita kwa Waingereza visiwani humu kulitokana na mkataba wa Julai 1, 1890. Katika mkataba huu Uingereza ilipewa 'haki' ya kuiweka Zanzibar chini ya himaya yake kwa kisingizio cha kuilinda dhidi ya mataifa mengine ya kigeni. Waingereza walivihitaji vituo hivi kwa vile wangeweza kutumia bandari zake kuegeshea vyombo vyao katika safari zao za Bara Hindi na Mashariki ya Mbali.

Ukoloni ulivuruga muundo wa kijamii visiwani na ukasababisha kujiimarisha kwa muundo wa kitabaka. Hii ni kwa sababu kundi fulani dogo lilimiliki nyenzo za uzalishaji mali na kundi kubwa la wenyeji likalazimika kulitumikia kundi hili dogo. Waandishi wa visiwani wamehusisha kuwepo na kujiimarisha kwa makundi haya na suala la mapinduzi katika kazi zao.

## 2.4 MUUNDO WA KIJAMII

Tumesema kwamba muundo wa kijamii visiwani ulikuwa wa kitabaka. V.1 Lenin alipokuwa akieleza maana ya neno tabaka alisema:

> Matabaka ya kijamii ni makundi
> makubwa ya watu waliotofautiana
> kwa sababu ya nafasi waliyoishika
> katika mfumo wa kihistoria wa

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

> uzalishaji mali; katika uhusiano wao (ambao wakati mwingine umewekwa na kudumishwa na sheria) na njia za uzalishaji mali; katika jukumu lao katika unidhamishaji wa ufanyakazi na vile vile katika mkondo na njia ya kupokea rasilmali za jamii wanazozitumia.[6]

Katika riwaya za visiwani tunakumbana na makundi yafuatayo: watamba-na-njia, mafalahi, watumishi, wafanyakazi wa mashamba na mijini, mamwinyi na mabepari. Idadi kubwa ya mafalahi, watumishi, wafanya kazi na watamba - na - njia wana asili ya Waafrika waliowekwa pembezoni mwa ardhi yenye rutuba. Wengine wana asili ya utumwa.

Mnamo Aprili 5, 1897 Sultani wa Zanzibar alitia sahihi mkataba ambao uliwapa watumwa haki na uhuru wa kupeleka mahakamani maombi ya kupewa uhuru. Hata hivyo, kulikuwa na vikwazo. Kwa mfano, mtumwa yeyote aliyepewa uhuru alipaswa kulipa kodi kama watu wengine waliokuwa huru. Aidha, kabla mtumwa huyu hajapewa uhuru alibidika kuonyesha ithibati kwamba ana mahali atakapoishi na ana njia ya kujiruzuku. Watumwa wengi walipewa kipande cha ardhi kilichoitwa 'panga ya mtumwa' ambacho

walikifanyia kazi kwa siku chache na kwa muda wa siku tatu au nne kwa juma walimfanyia kazi mwinyi mwenye - shamba. Fauka ya hayo, mamwinyi waliafikiana kuwa Waafrika waliotoka utumwani wapewe nafasi ya kukodisha ardhi ya makazi kutoka kwa mamwinyi hao na kufanya kazi kwa malipo (Jabir 1977:69). Kwa hivyo, uhuru wa watumwa ulikuwa wa bandia kwa sababu uliwatia watumwa katika haja ya kuuza nguvu zao na jasho lao kwa mamwinyi na mabepari ili waendelee kuishi. Wale ambao hawakupata mnunuzi wa nguvu zao waliishia katika utambaji - na - njia .... wengine wakawa wezi na wengine wakaingilia ukahaba. Duru hii ilijirejelea-rejelea kadri miaka ilivyoendelea.

Mpango wa utawala wa kiingereza ulidhamiria kwamba hatua zozote za kiuchumi na kisiasa zichukuliwapo ziwe zawapendelea Waarabu. Hii ni kwa sababu waliamini kuwa Zanzibar ni taifa la Kiarabu. Mrina na Mattoke wamesema:

> Mamwinyi waliotokana na mfumo wa watumwa ndio pia waliopewa nafasi na upendeleo katika mambo ya siasa, uchumi na maendeleo ya jamii.[7]

Uingereza ikawa yawapa Waarabu nafasi kubwa kakika tanzu zote za maisha na kwa hivyo kuwa Mwarabu

kukanasibishwa na ukwasi, heba na hadhi.

Ulinzi wa utawala wa Kiingereza kwa Waarabu ulibainika vema wakati wa mgogoro wa uwiwaji. Mgogoro huu ulifikia kilele chake miaka ya 1930 wakati Waarabu walipokuwa wakidaiwa na Wahindi baada ya kudhoofika kwa uchumi visiwani.

Ni jambo la kawaida kuwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya bidhaa katika taifa linalotegemea aina moja ya bidhaa. Hali hii iliikumba biashara ya karafuu. Jambo hili liliathiri sana biashara ya mamwinyi nao wakaanza kukopa fedha kutoka kwa wala-riba wa Kihindi ili kutosheleza ufujaji, ubadhirifu na 'ukarimu' wao kutegemea imani yao ya _kadri_ na _takrima_ (Lofchie 1965:108). Zaidi ya hayo, mamwinyi waliwiwa na Wahindi kwa sababu walishindwa kulipa mikopo yao iliyokuwa ikitozwa riba kubwa.

Shafi Adam Shafi katika _Kasri ya Mwinyi Fuad_ imeidokezea hali hii anaposimulia maisha ya babake Nassor. Anatwambia:

> Baba yake Nassor pia alikuwa Bwana Shamba lakini alikufa ghafla baada ya shamba lake kufilisishwa _ba_ bepari wa Kihindi aliposhindwa kulipa deni la pesa alizokopa kuchumia karafuu (uk. 34)

Suala hili la uwiwaji liliathiri sana muundo wa kijamii kwa vile Wahindi walianza kushiriki kilimo kwa kutwaa mashamba yaliyowekwa rehani au kununua mashamba ya karafuu kutoka kwa Waarabu. Baadhi ya Waarabu, kama Nassor hapo juu, wakalazimika kwenda mijini kutafuta kazi. Hata hivyo, kwa jumla, Waarabu walikuwa wamejikita katika kilimo na Wahindi katika biashara.

Wakati huu wa mvutano ulifikia kilele Waingereza walipojitokeza waziwazi kuwatetea Waarabu dhidi ya Wahindi. Jambo hili liliwafanya Wahindi kususia karafuu yote ya Zanzibar na pia wakakiomba chama cha kupigania uhuru cha India kiwahimize Wahindi wagomee karafuu iliyotoka Zanzibar (Mrina na Mattoke 1980:41).

Kwa hivyo, kuna makundi manne yaliyotofautiana kitaifa na yaliyochukua nafasi maalum za kitabaka kutegemea uhusiano wao na nyenzo kuu za uzalishaji mali na ugawaji wa bidhaa. Waingereza na Wahindi walikuwepo katika shughuli za viwandani na biashara, Waarabu wakashughulika zaidi na umilikaji wa mashamba na Waafrika wakawa ndio wafanyakazi. Baadhi ya Waafrika walipalilia na kuchuma karafuu, wengine wakawa wakwezi wa kuangua nazi, wengine makuli na wachukuzi bandarini na wengine watumishi viwandani.

Katika muundo wa kijamii visiwani rangi ya mtu ilimwelekeza katika tabaka maalum la kijamii. Rangi na tabaka vikaandamana. Chambilecho Nkrumah (1970:27):

> Katika dunia ya sasa, mapambano ya rangi yamekuwa mamoja na ya kitabaka. Yaani isibupo kuwa mna taklifu ya rangi, taklifu hii imehusishwa na mapambano ya kitabaka.

Mohamed Suleiman Mohamed katika Nyota ya Rehema anatusimulia vile Rehema anavyobaguliwa kwa sababu ya weusi wake usiochukuana na weupe wa wazazi wake. Ingawa mwandishi huyu angetaka kuonyesha, kwa upande mmoja, ukweli wa kimaumbile kuwa mtoto si lazima awalande wazazi wake, kwa upande mwingine, amethibitisha ukweli wa kihistoria kwamba rangi na utaifa wa mtu vilimwelekeza katika tabaka maalum la kijamii. Katika Dunia Mti Mkavu Bwana Suleiman anamkataza bintiye Lulua asiolewe na Farouk Hilal kwa sababu Hilal ni mweusi. Baadaye Bw. Suleiman anapoona atafilisiwa na kupigwa tanji na Lalji anasalimu amri na kuikubali hiyo ndoa mradi tu Farouk aibatilishe haki kwa manufaa ya Bw. Suleiman.

Itakumbukwa kwamba Farouk Hilal (Kibwana Jaku) ananunuliwa na Bi. Wa Minarani (Bi. Nafisa).

Mwafrika ananunuliwa na Mwarabu na anastaarabishwa. Kununuliwa huku ni jazanda ya Mwafrika kujikuta kisadfa katika tabaka tawala. Hili litokeapo, yeye hulisaliti tabaka lililomzaa na kulibusu kwa mikono miwili tabaka hilo jipya. Uzawa unakuwa jambo duni chini ya kivuli cha nafasi mpya ya kiuchumi iliyopatikana. Kibwana Jaku anapomfanya babake afungwe jela na kuamuru nduguze Bakari, Pandu na Fumu wauawe (japo hakujua ni ndugu zake), alikuwa akiutii wito wa tabaka lake jipya. Kutokana na maelezo tuliyoyatoa hapo juu, jamii ya visiwani Zanzibar kama ijitokezavyo katika riwaya hizi ni jamii yenye muundo wa kitabaka. Aghalabu, tabaka la mtu lilitegemea rangi yake kwa sababu nafasi za kujiendeleza zilifuata rangi. Said Ahmed katika Dunia Mti Mkavu ametuonyesha kwamba endapo rangi na tabaka havikuandamana, kama ilivyotokea kumhusu Farouk Hilal, basi tabaka lilivuvia rangi na likawa na nguvu zaidi.

## 2.5 ELIMU NA NAFASI ZA KAZI

Nafasi kubwa za elimu ya juu zilitolewa kwa Waarabu, Wahindi na Waingereza. Hii inamaanisha kwamba Waafrika walilazimika kufanya kazi za Sulubu za kutumikia na kuhudumia. Wengi wao walilazimika

kufanya kazi za kijungu-jiko ambazo hazikuwa na simile bali zilijaa hatari. Mijini kazi zilizokuwa maarufu ni za ukuli na uchukuzi. Duru hii ilirithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Katika Dunia Mti Mkavu tunafahamishwa kwamba mzee Gae alisoma hadi darasa la sita. Kwa hivyo urazini wake wa kisiasa haukutokana na elimu ya shule bali na uhalisi wa maisha visiwani, "vita vya mpakani alivyoshiriki," na safari nyingi za nchi mbalimbali alipokuwa baharia. Shomari amejua kuandika ukubwani na Bakari "amejifunza kusoma na kuandika kutokana na Hababuu mtoto wa tajiri wake, Khalfan, alipokuwa akifanya kazi ya uboi kwao" (uk. 42). Aidha, katika riwaya hii tunakumbana na watoto wadogo ambao wanapaswa kuwa shuleni lakini badala yake wanakokota susu la samaki kwa sababu ya ukosefu wa karo ya shule.

Said Ahmed katika Asali Chungu anatueleza kuwa Dude, kama vile Mzee Gae hapo juu,alimalizia shule darasa la sita. Alikuwa hodari shuleni lakini mahudhurio yake yalikuwa mabaya kwa sababu ya ulitima uliomkumba yeye na mamake Semeni.

Tukiigeukia riwaya ya Kuli tunaona kwamba Rashidi anarithi kazi ya babake ya ukuli kwa

sababu hakupata elimu wala ujuzi. Hakuwa na jingine ila kuzitegemea nguvu za mikono yake ili kujiruzuku. Tunafahamishwa kwamba ilimpasa asomewe na Faki makaratasi ya kuwatetea wafanyakazi. Baadaye, akiwa bado ni mtu mzima, alihudhuria elimu ya watu wazima baada ya kutoka kazini.

Wasichana wengi tunaokumbana nao katika riwaya hizi hawakusoma. Mohamed Suleiman Mohamed katika Nyota ya Rehema anatuonyesha kwamba Rehema hajui kusoma wala kuandika. Rehema, ambaye hasa ni mtoto wa Mwinyi Fuad, anabaguliwa kielimu kwa sababu ni mweusi. Ndugu zake, Samir na Salma, waliochukua rangi ya baba yao wanapewa elimu nzuri. Bahati katika Kiu amesoma hadi darasa la kumi na mbili lakini hakupata kazi. Maisha yake ya ukata yanamfanya aghilibike kwa urahisi na mapenzi ya kinafiki ya Idi.

Kwa upande mwingine, watoto wa mamwinyi na mabepari walipata elimu nzuri. Katika Kiu tunafahamishwa kwamba Rehema wa mzee Mwinyi anasomea elimu ya juu Ulaya. Hali ni hiyo hiyo katika Nyota ya Rehema. Samir, mtoto wa Adila na Fuad, anasomea Ulaya na fedha zinatumiwa kumwingiza Salma katika 'Royal School' ingawa kama tunavyoambiwa, shule

yenyewe imejaa. Haya yanawezekana kwa sababu 'mkurufunzi pesa' chambilecho Fuad. Wenye elimu nzuri na ya fahari ni wale waliopendelewa na mfumo wa uzalishaji mali.

Mfumo wa aina hii ya uzalishaji mali huwaelekeza watu kuuza kile walicho nacho-mradi tu kuwe na mtu aliyejitayarisha kukinunua. Kwa kuwa Waafrika hawakupata elimu ya juu ilikuwa muhali kwao kupata kazi zenye heba na hadhi. Badala yake waliishia katika kazi za kijungu-jiko zenye dharubu na Sulubu. Baadhi walikuwa wakulima wa vikataa, wengine wafugaji, wapagazi, wachukuzi na watumishi na wengine makuli wa bandarini. Wengine walifanya kazi za rejareja za kuuza supu, uji na maandazi na wengine wakawa watamba-na-njia. Hawa watamba-na-njia wakalazimishwa na uhitaji kuuweka kando utu wao. Wakaingilia na kuzama katika ukahaba, ulevi na wizi.

Ingawa udhaifu wa kimaumbile unaweza kumwelekeza mtu katika ukahaba, wahusika wengi katika riwaya hizi wanajikuta mijini wakiuza miili yao kwa sababu ya uhitaji. Katika <u>Dunia Mti Mkavu</u>, Sakina anautoa mwili wake kwa Farouk ili apate kazi. Anaambiwa:

> Kupeana ni kikoa, toa nawe upewe. Bila ya hivyo hakuna kazi. (uk. 84).

Katika Asali Chungu, Semeni anakataa njama za mwajiri wake Zuberi kwa sababu anajiheshimu. Hata hivyo ananusishwa dawa akiwa usingizini na ananajisiwa. Maisha yake yanabadilishwaa na anakuwa fundi wa ulevi na ukahaba. Tunaambiwa:

> Haja ndiyo iliyombadilisha. Moyo wake mgumu ukalainika. Akakubali yale ambayo kwake yalikuwa magumu kutendeka. Akasalimu amri na kutoa lile ambalo watu wakilichimba (uk.55)

Baadaye akakinaiwa, akapuuzwa na akaporomoka. Mwajiri wake Mwinyi Zuberi ndiye aliyemvua utu pale alipomnajisi. Maisha yake mapya yakawa ya kinyama. Hata kile alichokizaa (Dude) kikawa hakina msingi madhubuti wa maisha. Semeni amekengeushwa na ulimwengu hivi kwamba miiko kwake haipo. Pili anatwambia:

> Tazama alivyokondeana vile, fupa la uso limemparama. Hayumo mule Semeni wa mwaka jana, hayumo;

> amebak debe bovu. Lo, masalale! Mimi nilidhani atakuwa na akili zake ajisikie mambo, wapi! Akitoka chakari, akirudi chordo. Huu ulevi ndio unaozidi kumuuwa; ulevi moto mmoja. Na hayo mambo ameyafanya ibada; akiingia huyu, anaingia huyu.... ndiyo kazi; amejigeuza ardhi, hatosheki na viumbe (uk. 48)

Na wala si yeye peke yake, bali ni wasichana wengi wanaoishi Ng'ambo- mtaa wa Waafrika.

Katika Nyota ya Rehema, Rehema anabaguliwa na kupuuzwa na babake na mamake wa kambo (Adila) kwa sababu ya weusi wake. Kwa hivyo, anachagua kwenda mjini kuliko kutukanwa na kufedheheshwa. Huko anakumbana na akina Mansuri walio tayari kununua mapenzi. Tena, majaribu ya wenzake kama Kidawa, Ruzuna na Chiku yanabadilisha mkabala wake kuhusu maisha na anazama katika uasherati.

Miriam Mapozi katika Dunia Mti Mkavu anautumia urembo na ujana wake kumwendeshea maisha. Tunapokumbana naye kwa mara ya kwanza, 'amewekwa' kama kimada na Ramadhani 'karani njaa.' Ndoto yao ni kuwa hapo baadaye watatoka mtaa wanamoishi

ili waepukane na maisha ya zogo na zahama za watu wa tabaka la chini. Lakini uhalisi wa maisha ni kwamba hawawezi kujitanua kiuchumi kwa sababu mshahara wa Ramadhani ni mdogo. Naye Mashaka anaiba viakiba vya mkewe, Mtumwa, ili aende ulevini kwa minajili ya kujisahaulisha idhilali iliyomkusa. Wakati wa vita visivyokoma, Mashaka anamlalamikia mkewe:

> Unafi... unafikiri na ... nayataka
> Mimi ha...haya, miimi niku....
> nikutegemee wewe! Unafi... kiiri
> mi nalewa kwa niini? Nipe kazi
> bas , nipe ka...zi wewe bas ,
> unafikiri rahisi? (uk. 30)

Si rahisi kwa sababu yeye ni MUME na ana jukumu la kuitafutia riziki aila yake. Lakini mfumo haumruhusu na kwa hivyo anatafuta sitara katika ulevi. Mashaka ni mmoja katika kundi kubwa lililonyimwa haki ya kuishi kama inavyomstahiki binadamu.

Katika Asali Chungu, Said Ahmed anatwambia:

> Miongoni mwa maelfu ya vijana
> waliokuwa wakitafuta kazi na
> hatimaye kuzurura ovyo majiani

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

> na kuhunika, mmoja alikuwa
> Dude. (uk. 76).

Uhitaji ulimtumbukiza jela na baadaye ukamfanya atekwe na amtumikie Amina, mke wa Zuberi. Amina aliutumia utajiri wake kuwanasa vijana shababi na mabarubaru ili wazime utashi na ashiki zake. Wala si Dude peke yake. Bushiri, hali kadhalika, alielekezwa kwenye uhalifu na mfumo wa uzalishaji mali. Kabla hajapata kazi ya kumtafutia Amina vijana wa kiume aliowatamani. Bushiri na jela walikuwa chanda na pete. Anatwambia:

> Niliona bora utumwa wa kuwa mfungwa kuliko kuwa na uhuru katika ulimwengu ambao hauwezi hata kunipa chakula. Nilihisi kutoka jela ni kubadilisha namna ya mateso; na pengine akhasi. Nje kuna maonevu, unyonge na utumwa.... (uk. 97)

Bushiri akastahabu kukaa jela ambako angaa angepata chakula cha bure.

Ni bayana kufikia sasa kwamba katika riwaya za visiwani Waafrika walikoseshwa kazi na walibaguliwa. Said Ahmed katika <u>Asali Chungu</u> anatwambia kwamba

Afisa wa Leba Mukri aghalabu aliwatia kazini jamaa zake wa Kihindi.

> Kazi ya Baniani huyo ilikuwa kutia watu kazini. Mara nyingi aliwatia kazini jamaa zake wa Kihindi au yeyote aliyeweza kumpa tonge. Kazi njema zikawa za mabwana na matajiri; kina Dude mara nyingi wakaingia utopasi. (uk. 77).

Mfano mzuri ni Subhash ambaye kitabaka hakutofautiana na Dude. Subhash alikuwa mmoja miongoni mwa wale waliojikuta katika mkumbo wa kufukuzwa kwa ajili ya ukosefu wa karo. Ingawa alifika darasa la sita kama Dude na wala hakuwa hodari shuleni, alipewa kazi na Mukri. Jambo hili likamwudhi Dude na kwa hivyo akaanza kutafuta tatuzi la kibinafsi. Akamhujumu Mukri na hili likamfungisha miaka miwili.

Utawala wa kikoloni haukutosheka kuwakosesha Waafrika kazi bali uliwafuata kokote walikokuwa wakijitafutia njia za kujiruzuku. Bi Zaina katika Dunia Mti Mkavu (uk. 47) ameanzisha kioski awe akiwauzia wafanya kazi chakula kwa bei nafuu. Hata hivyo, anapewa notisi afunge kioski yake eti kwa sababu anatia mji uchafu. Njia za kihalali za kujitafutia riziki zinajazwa taklifu nyingi katika

mfumo huu wa uzalishaji mali.

Shida hizi zimesimuliwa vile vile katika Kiu kuhusiana na maisha ya Bahati na Cheusi. Ulemavu uliosababishwa na umaskini ndio uliomfanya Jaku, babake Bahati, ayoyomee hadi Kongo akajiingize katika biashara ya magendo. Ulemavu huu unamfanya Bahati aghilibiwe na Idi na atumiwe kama chambo cha kuunasia utajiri wa Mwinyi.

Elimu ilikuwa na nafasi kubwa sana katika kuwaelekeza watu kwenye kazi za kitaaluma.

Jedwali lifuatalo linatuonyesha kwamba Waafrika walipata elimu duni. Ithibati hii ya kihistoria inaunga mkono hisia za Waandishi wa riwaya visiwani kuhusu elimu ya Waafrika.

Wanafunzi mashuleni mwaka wa 1948

| DARASA | Waarabu | | Wahindi | | Waafrika | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi: | asilimia | Idadi: | asilimia | Idadi: | asilimia |
| 1-6 | 3715 | 29.2 | 955 | 7.5 | 4905 | 38.5 |
| 7-9 | 430 | 25.7 | 595 | 35.5 | 185 | 11.0 |
| 10-12 | 225 | 32.1 | 290 | 41.4 | 20 | 2.9 |

kutoka Lofchie (1965:92)

Jedwali hili linatuonyesha kwamba Waarabu na Wahindi walipata elimu nzuri. Hii, bila shaka, iliwahakikishia kazi nzuri na zenye hadhi. Ukweli huu unathibitishwa na Mukri katika Asali Chungu (uk.77) asemapo:

> Iko wenjenu shoma shana.
> veve hata darsha pili kuna
> fika; tampo vapi kazyi.

Hao waliosoma sana bila shaka ni wale wa tabaka la juu waliopewa nafasi nzuri ya kuteka elimu.

Katika Nyota ya Rehema tunampata Karim, mume wa Salma. Karim ni Mudir wa mjini na ana hadhi kubwa serikalini. Mkuu wa Polisi ni nduguye kwa baba na mama. Mwenyekiti wa sheria ni baba yake mdogo. Naye Jaji Mkuu ni mtani wake (uk. 125). Katika Asali Chungu, Zuberi ni Mkuu wa Wilaya na Mukri ni afisa wa Leba Shafi Adam Shafi katika Kuli anatwambia kwamba Brek na Ramju ndio wanaotoa kazi. Na katika Dunia Mti Mkavu, tunakumbana na Farouk Hilal ambaye, japo ni mweusi, ameinuliwa kitabaka na wazazi wake walezi. Akapelekwa masomoni Ulaya na akapata Uinspekta wa polisi. Mkuu wa Polisi ni Mzungu. Mr. David.

Hali hii inatuonyesha kwamba tabaka linalomiliki nyenzo za uzalishaji mali ndilo tabaka tawala.

Tabaka hili linashikilia nafasi za kazi kubwa kubwa kwa sababu limepata elimu nzuri. Utengano huu wa kikazi na kielimu bila shaka ulichangisha katika kuyachochea mapinduzi.

## 2.6 PUPA

Kuna fikra za kidhanifu zinazochukulia pupa kuwa ni jambo linalotokana na maumbile ya binadamu na kwamba binadamu hawezi kujitanzua kutoka katika hali hiyo.[8] Jambo hili halikubaliki kulingana na mkabala wa Ki-Marx. Mtazamo wa Ki-Marx huchukulia kwamba tusemapo 'maumbile' katika muktadha huo tunamaanisha hali ya binadamu aliyekengeuka. Hali ya mkengeuko ni ile ambayo hupatikana wakati falsafa au mtazamo wa mtu unapopingana na kanuni, mwenendo na msingi wa jamii. Elimu na fedha wakati mwingi hukengeusha kwa sababu humtenga mtu na jamii. Wakati mwingine binadamu aliyekengeuka huwa na ubinafsi na pupa iliyokithiri ambayo husababishwa na juhudi zilizofurutu za kutosheleza nafsi. Juhudi hizi humwelekeza mtu katika kukengeuka zaidi na zaidi na hatimaye tabia zake huwa ni za kinyama.

Ni katika muktadha huo ambapo twapaswa kuitazama pupa kama sehemu ya mfumo wa uzalishaji mali kabla ya mapinduzi.

Katika mfumo wa uzalishaji mali ambapo walio wengi hawana njia nzuri za kujiruzuku, inatarajiwa kwamba kutakuwa na tamaa kubwa na upapiaji wa mali miongoni mwa wale wenye nguvu za kisiasa na kiuchumi. Ufisadi utakuwa na nafasi kubwa katika maisha. Pupa hiyo, aidha, itazidisha ubinafsi na uzandiki kwa sababu mtu atayafikiria maslahi yake mwenyewe na si mno kuyajali maslahi ya wengine. Licha ya pupa ya mali, kutakuwa na upapiaji wa miili ya binadamu kwa lengo la kutosheleza ashiki na utashi. Kwa vile pupa hii zaidi hupatikana miongoni mwa tabaka - tawala lenye nguvu, walio wengi hujikuta katika dhuluma na hiana. Hali hii husababisha kuweko kwa kundi kubwa la watu wenye hasira na ghamidha, japo za kibinafsi, dhidi ya tabaka tawala. Hili baadaye husahilisha kuweko kwa mlipuko wa kisiasa hasa baada ya wenye ghamidha kupevuka kiurazini.

Kwa hivyo pupa, kama ilivyosawiriwa katika riwaya za visiwani, haina budi kuchunguzwa kama kichocheo cha mapinduzi. Pupa hii ni ya mali na mwili.

Ingawa katika <u>Dunia Mti Mkavu</u> Fumu amekasirishwa na mfumo mzima wa uzalishaji mali unaomdhulumu, ana hasira za kibinafsi dhidi ya Fauz. Fauz anamtaka

Masika, mpenzi wa Fumu. Kwa hivyo, anamtisha Fumu kusudi Fumu akiache kile ambacho Fauz anakitamani. Fumu anazuiliwa kulima na kulisha ng'ombe katika shamba 'alilolikodi'. Fauz anamtesa kisaikolojia kwa mbwa na bunduki. Baadaye mimea yake inatiwa moto na Fauz. Tamaa ya kumpata Masika inampofusha Fauz asijali hisia za Fumu na Masika. Shehe, Hamoud (babake Fauz)na babake Masika wanamwana Masika aweke dole katika cheti cha ndoa. Masika, kwa upande wake, anaradua kuoa fukara anayempenda.

Ndoa yapasa kuwa kitu cha kufurahia na kushangiliwa. Lakini ndoa iliyojikita katika ubinafsi na pupa inaleta majonzi na kilio. Katika mfumo wa uzalishaji mali uliokuwepo kabla ya mapinduzi, ndoa ilitumiwa kama chombo cha kuvunjia utu sio kama jambo la kuendelezea kizazi. Babake Masika anamwuza bintiye kwa sababu ana tamaa ya mali na Fauz anatumia hiyana kumpata Masika kwa sababu ana tamaa za kimwili ambazo angetaka zizimuliwe. Tamaa ya babake Masika inabainika anapomwambia bintiye:

> Masika, sisi tu masikini
> Mimi ni nokoa tu wa mabwana hawa;
> huoni kwamba ndoa hii itatufungulia
> milango ya kheri. Mimi sikubali
> mwanangu aolewe na masikini maadamu

imemwangukia nyota ya jaha (uk.21)

Ingawa usemi huu unaweza kuonyesha kama kwamba babake Masika anajali maslahi ya bintiye hili si kweli hata chembe. Gurudumu linalomsukuma ni pupa na matumaini ya utajiri Masika akiolewa na Fauz. Fikra hii inapata nguvu tunaposhuhudia Masika akibingirishana na babake, Shehe na Hamoud. Hatimaye anasalimu amri baada ya kuzidiwa nguvu. Siku ya kuingia ndani, ilibidi Masika afungwe miguu na mikono kusudi Fauz atosheleze ashiki zake. Baadaye, Masika anamwua Fauz. Kutofaulu kwa ndoa ya Masika na Fauz ni kielelezo cha ugumu wa ushirikiano baina ya matabaka mawili yanayokinzana. Ushirikiano kama huo unapolazimishwa huangukia patupu kwa sababu hauna msingi imara. Jambo hili limejadiliwa vema na Ebrahim Hussein katika <u>Arusi</u>.

Katika tamthilia hii, Bukini (nchi ya kibepari) anataka kumwoa Mwanaheri (nchi ya kijamaa) lakini bila kumfichulia matakwa yake yote. Bukini anamvisha pete Mwanaheri wakati Mwanaheri amefumba macho. Lakini Mwanaheri anapofumbua macho, anaivua pete kukataa pendekezo la arusi la Bukini mpaka 'hapo hapo baadaye'. Hii ni kwa sababu baina ya kufumba na kufumbua macho aliweza kuona kwamba

itakuwa kinyume na maslahi yake kujiwacha aghilibiwe na 'Shetani wa mahaba' akaingia katika ndoa yenye hadaa na ubinafsi. Yaonekana kana kwamba Hussein yuasema kwamba 'ndoa' baina ya mataifa mawili yanayofuata mifumo na mitazamo tofauti haiwezi kufaulu. Inspekta Farouk Hilal katika Dunia Mti Mkavu anahongwa na wasichana kwa miili yao kusudi awape kazi. Vile vile yuko tayari kuibatilisha sheria ili ampate Lulua, binti wa Bw. Suleiman. Anasema:

> Kwa ajili yake nitafanya lolote;
> nitasimama kuibatilisha haki ingawa
> haki ya batili maana yeye Bwan
> Suleiman na Lalji sijui nani pwaguzi.
> Kamwambie Bwan Suleiman kafuzu.
> (uk. 80)

Kinachomwongoza ni pupa ya kumpata Lulua.

Ufisadi, kwa Inspekta Farouk Hilal, ni jambo la mazoea na kaida. Anachukua mirungula kutoka kwa watu mbalimbali ili afifilishe kesi zao. Tunafahamishwa kuwa mezani alikuwa na kiasi cha faili derizeni moja za watu waliomhonga. Wenye fedha wakapata nafuu katika sheria na wanyonge wakazama katika maonevu. Mfano mzuri ni yale yaliyompata Mwanaali binti Hamadi. Huyu bibi alikuwa na

kikataa cha Kibopa Chewa karibu na Bwana Khelef, mpaka na Bwana Subhash, Akamkopa Subhash shilingi mia tano lakini baadaye akashindwa kuzilipa. Subhash akamwendea Inspekta Farouk ili kikataa cha Mwanaali kufidie fedha hizo. Mwanaali akatilishwa dole kwamba amekubali kikataa chake kitwaliwe. Anasema:

> Kwa nguvu nitatia, hata wewe Supekita ukizidiwa nguvu kama mimi, utafanya lolote... (uk. 88)

Pupa ya Farouk Hilal na Subhash ikawafanya wamdhulumu Mwanaali. Subhash akaongeza kikataa hiki kwenye fahari kubwa ya mashamba yake. Mfumo wa uzalishaji mali wa namna hii haumpi nafasi mnyonge kujitanua bali huendelea kumminya hadi tone lake la mwisho la uhai. Kikataa cha huyo mama ni uti wa mgongo wa maisha yake lakini anahiniwa na wawakilishi wa sheria ili apewe Mwinyi mwenye mashamba mengi.

Pupa kama hii ndiyo imfanyayo Shomari katika Dunia Mti Mkavu (uk. 39) kusema:

> Katika ulimwengu huu mwanadamu kila kitu amekifanya chake. Hata hewa wangaliweza kuitenga na kuidhibiti wangalinganyana, kila mmoja akidai

> ni yake. Na hiyo labda ndiyo
> nusura yetu sisi masikini;
> angalau tuko huru kuvuta hewa;
> ingawa sisi huvuta chafu, wao
> wakavuta safi.

Ngugi wa Thiong'o ameizungumzia pupa ya namna hii katika Shetani Msalabani na Nitaolewa Nikipenda.

Katika Asali Chungu hali kama hiyo inajitokeza. Zuberi, ambaye ni Mkuu wa Wilaya, anafanya mapenzi afisini badala ya kuwahudumia wananchi. Tamaa imemkengeusha Zuberi hadi tabia zake zikawa za kinyama. Kwa mfano, anamtarajia Mzee Omari amletee bintiye mboga ili afanye mapenzi naye. Akimletea, Zuberi anasema, ataepukana na kutoa thuluthi mbili za mavuno yake. Pupa ya Zuberi vile vile inadhihirika anapofunga matambara miguuni na kumvamia na kumnajisi Semeni baada ya kumnusisha dawa. Hivi ni vitendo vya kinyama vilivyotokana na ukengeushi wa mfumo uliowapa wachache uwezo wa kudhibiti kila kitu.

Wakati Zuberi akifukuzana na wasichana wabichiwabichi Mkewe naye anafukuzana na wavulana. Amina anautumia utajiri kama chambo na ulimbo wa kuwanasa wavulana wampe kile alichokitamani. Lengo

la Amina ni kudhibiti nafsi, vitendo na fikra za yule amnasaye kama vile Katu anavyomdhibiti Juma katika Buriani. Amina anamwambia mpenzi wake Dude:

> Dude siwachi kukuhimiza; nisije nikakukutia, au hata kusikia, una mwanamke mwingine; moyo wangu hauchukui joto hilo. Nataka uwe wangu, mali yangu, pasi na mtu kuweza kuniingilia; umesikia hivyo? (uk. 140).

Amina hajali hisia za Dude bali anachokijali ni utashi wake mwenyewe.

Katika Nyota ya Rehema pupa ndiyo inayoipeleka mrama ndoa ya Salma na Karim. Karim ni mpenda raha, starehe na pesa. Kwa vile anajua apendwa sana na Salma anamfanya kutenda lile asilolitaka. Salma anaiba, anadanganya na anakopa ili kumkidhisha Karim. Lakini Karim hajui kukinai. Anatamani shamba la Ramwe ambako Sulubu na Rehema wanaishi kwa furaha, utu na utulivu wakitaraji kufaidi jasho lao. Tunaambiwa vile Sulubu anavyoisarifu ardhi:

> Sasa hakuwa na hofu kama alivyokuwa nayo pale alipokuwa akipanda mimea yake katika ardhi za kukodi, ambazo wenyewe wangeweza kupandisha kodi

> wakati walipopenda na kumpa - kwa mujibu wa sheria - ilani ya 'saa - ishirini-na nne' achague baina ya shubiri ya kupokea fidia waliyoikisi wao wenyewe, au mrututu wa kungoa mimea yake katika ardhi yao. Sasa alijua jasho lake litatua ardhini. (uk. 105)

Lakini halikutua. Pupa ya mamwinyi ilimwandama hadi Ramwe ikawa Sulubu ametoka kikaangoni akaingia jikoni. Karim alishirikiana na wenzake ki-tabaka ili kulipata shamba la Ramwe. Ikasemekana Rehema alizaliwa nje ya ndoa na kwa hivyo hakuwa mrithi wa mali ya Fuad. Madole ya bandia yalitumiwa kuubatilisha ukweli huu. Sulubu, Rehema na Mzee Pongwa wakaihama Ramwe. Wakaanzisha makao mapya. Karim hakukinai kuipata Ramwe. Akatamani makao hayo mapya yaliyotokana na kunadhifishwa na misuli ya wanyonge. Lakini wavyele wamenena 'mwenye pupa halitamu.' Karim akauawa na Sulubu (kama vile mbwa Simba) kwa kufurutu pupa na kuparamia kile ambacho kimsingi ni cha wengine. Kitendo hiki cha Sulubu ni kilele cha uvumilivu wa miaka mingi.

Katika <u>Kiu</u> tunakumbana na Mwinyi, Idi na Bahati ambao wote wana pupa. Pupa ya Mwinyi ni kumpata

Bahati kwa vyovyote. Anaamini kwamba utajiri wake unaweza kuilaza milima. Japo ni mzee ki-umri na Bahati ni kijana hana wasiwasi kuwa atampata kwa sababu katika mfumo huu 'mkurufunzi ni pesa.' Imani hii inamfanya amtegemee sana Idi, dereva wake. Anakosa nathari asijue kuwa Idi anamcheza shere kusudi atwae mali yake. Lengo la Idi ni kutegemea nundu. Inapombainikia Mwinyi kuwa hampati Bahati, maradhi yanamzidia na kumharakisha kaburini.

Pupa ya Bahati ni mapenzi kwa Idi. Anapofushwa na mapenzi haya mpaka anaridhia kufanya lolote aambiwalo na Idi ingawa haliamini. Anakubali kuwa mshiriki wa Idi katika kumghuri na kumlaghai Mwinyi. Pupa ya pili ya Bahati ni mali. Bahati ni msichana aliyekulia katika ukata na ingawa amefika darasa la kumi na mbili, hana kazi. Mwanzoni, haamini kuwa mali yana nafasi kubwa katika maisha ya binadamu lakini baadaye anazuzuliwa na Idi na kuonyeshwa kuwa fedha ni tatuzi la umasikini na ni njia inayomweleke za binadamu katika furaha, anasa na starehe. Anakumbana na ukweli baada ya kuolewa na Idi, kuteswa na kutalikiwa. Anapodai haki yake ya ngawira walizoteka kutoka kwa Mwinyi, anauawa.

Idi ana pupa ya pesa na anasa. Pupa hii inakithiri hivi kwamba yuko tayari kuua ili akipate

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

kile anachokienzi. Anamlaghai Bahati na kumtumia kama ulimbo wa kunasia mali ya Mwinyi. Pupa inamvua utu. Anapokipata kile akitakacho anawatema Mwinyi na Bahati. Idi amebadilishwa na kukengeushwa na mfumo wa kiuchumi hivi kwamba hajui mhisani wake ni nani.

Hata katika riwaya za Shafi Adam Shafi tunaona baadhi ya wahusika wakidhihirisha pupa za kimwili na mali. Katika Kuli tunakumbana na Mzee Tindo. Huyu ni kiongozi wa kundi la wachukuzi wa karafuu katika ghala la CGA. Badala ya mzee Tindo kuwakilisha maslahi ya wachukuzi wenzake, anawakilisha maslahi ya mabepari. Ndiye anayemfahamisha Morarji kuhusu mipango ya wachukuzi ya kuwasilisha matatizo yao. Anajipendekeza kwa waajiri wake kusudi apewe tonge. Ni wazi kwamba usaliti kama huo unaorudisha nyuma jitihada za wanyonge za kujikomboa unatokana na ubinafsi wenye misingi yake katika pupa ya kujifaidi wakati wengine wakiteseka.

Pupa ya kuzimua ashiki za kimwili inadhihirika katika Kasri ya Mwinyi Fuad wakati Fuad anapojaribu kuwavamia Mariam na Mkongwe. Wasichana hawa wa-kifanya kazi hawampi nafasi. Tabia yao ni kama ya Waringa katika Shetani Msalabani. Baada ya Fuad kukataliwa na Mariam, ari yake ya ubwana

inateketea. Anajiuliza:

> Vipi, Vipi, kijakazi kama kile
> kimkatae bwana wake....?
> Kilithubutuje kusema 'sitaki'!
> Kupiga kelele, kumtia aibu...
> ..... ah! (uk. 22)

Hakuelewa kwa sababu alijiona yeye ndiye mtu na wengine ni 'vitu'. Hivi ndivyo mtu aliyekengeushwa na 'ubwana' anavyofikiri. Haoni uwezekano wa kukataliwa au kupuuzwa na mtu wa tabaka la chini kiuchumi. Amezoea kumiliki na kwa hivyo anatamani kumiliki hata nafsi za binadamu wenzake. Na pindi akutanapo na mtu aliyejikita kuitetea nafsi na utu wake, basi hupigwa na butaa. Azindukapo, hujikakamua kutumia mabavu kusudi fahari yake isiteketee. Haya ndiyo yaliyotokea baina ya Zuberi na Semeni katika Asali Chungu, Fauz na Masika katika Dunia Mti Mkavu, Mwinyi na Bahati katika Kiu na Fuaz na Mkongwe katika Kasri ya Mwinyi Fuad.

## 2.7. HITIMISHO

Katika sura hii tumeona kwamba mfumo wa uzalishaji mali visiwani Zanzibar uliwapendelea wachache na kuwakandamiza walio wengi. Tumeona kuwa hawa wachache ndio waliomiliki nyenzo za uzalishaji

mali. Hili linajitokeza katika riwaya zote tunazozihakiki. Ukweli huu una misingi yake katika ukoloni wa Kiarabu na Kiingereza ambao ulipojikita uliimarisha jamii yenye muundo wa kitabaka. Tumeona kwamba nafasi za elimu nzuri na kazi zilikuwa wazi kwa watu wa tabaka la mamwinyi na mabepari ambao aghalabu walikuwa Waarabu, Wahindi na Waingereza. Waafrika kazi yao ikawa ya kuwahudumia na kuwatengenezea thamani ya ziada mashambani na viwandani. Mfumo huu vile vile ulisababisha kuwepo kwa watamba-na-njia walioishia kuwa wezi na makahaba. Aidha, pupa kama sehemu ya mfumo ilijiimarisha katika kiwango cha mwili na mali.

Kutokana na hali kama hiyo kuzuka kwa mikinzano ya kitabaka kulikuwa jambo la lazima. Katika sura ifuatayo tutaichunguza mikinzano hiyo.

## 2.8 TANBIHI

1. Katika shughuli za uzalishaji mali binadamu huingia katika uhusiano fulani na wenzake. Uhusiano huu hubainika katika ugawanyaji wa kile kitokanacho na shughuli hizo.

2. Mabadiliko ya kijamii hayapasi kuchunguzwa katika falsafa ya enzi inayohusika bali katika hali ya kiuchumi. Kwa maelezo zaidi tazama Karl Marx Selected Works Vol. 1 International Publishers.New York

3. Neno hili linatumiwa katika tasnifu hii kwa maana ya wakulima wadogo wa vikataa.

4. Hawa walikuwa wasimamizi wa mashamba makubwa ya Mamwinyi. Aghalabu nokoa alikuwa chini ya 'mkadamu'.

5. Hii ni hali ya ujeuri na ufyozi

6. Lenin, V.1 Selected Works Vol. 9 Progress Publishers. Moscow, uk. 432-433

7. Mrina na Mattoke (1980) Mapambano ya ukombozi Zanzibar. T.P.H. Dar-es-Salaam uk. 28

8. Tazama Babu, A. katika Debate on Class, State and mperialism kilichohaririwa na Tandon, Y.(1982) Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. (Uk. 1)

# SURA YA TATU

## 3.0 NAFASI YA MIKINZANO YA KITABAKA

### 3.1 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita tumejaribu kuonyesha msingi wa mapinduzi visiwani Zanzibar kama ujitokezavyo katika riwaya tunazozihakiki. Huku tukitumia ithibati za kihistoria, tumesema kwamba nyenzo za uzalishaji mali zilimilikiwa na tabaka dogo ambalo lilikuwa la Waarabu, Wahindi na Waingereza. Tumetoa kauli kwamba aghalabu tabaka na rangi viliandamana na kwamba Waafrika hawakupata nafasi nzuri za elimu. Hii iliwanyima wengi wao kazi za kitaaluma. Tumetoa mifano kutoka riwaya za visiwani kuonyesha kuwa pupa ya kila aina ilikuwa sehemu ya maisha. Kutokana na hali hizo, mikinzano ya kitabaka ilijitokeza kama zao la mfumo mzima wa maisha.

Sura hii inanuia kuchunguza mikinzano ya kitabaka kama ijitokezavyo katika riwaya tunazozihakiki. Lengo letu ni kubainisha kwamba hakuna mapinduzi ya kijamii yatokeayo bila kuwepo mwanzoni mivutano ya kitabaka. Tutachunguza nafasi ya mikinzano katika mapinduzi. Kisha tutajadili mikinzano yenyewe na urazini wa kitabaka, kama hali muhimu katika mapinduzi. Aidha, tutajadili nafasi ya taasisi za utawala katika mikinzano ya kitabaka.

3.2 MIKINZANO NA MAPINDUZI

Hatuwezi kusema kwamba mapinduzi visiwani Zanzibar yalitokea kwa sababu ya kuzorota kwa hali ya maisha. Riwaya zote za visiwani zinatusimulia kuhusu ukwasi miongoni mwa tabaka fulani visiwani. Tabaka hili linamiliki mashamba na nyumba za kukodisha. Wengi wao wana magari. Katika Kasri ya Mwinyi Fuad, Fuad anaendesha gari aina ya Rambler. Amina wa Asali Chungu ana Vauxhall, Mwinyi wa Kiu ana Benz, na Fuad wa Nyota ya Rehema ana Land Rover. Wote wana majumba makubwa yanayostahiki kuitwa 'makasri'. Al'muradi kabla ya mapinduzi tabaka fulani lilikuwa na maisha yenye anasa na yaliyojaa pomoni kwa hali na mali.

Wasomi fulani kama Chalmers Johnson[1] wamejaribu kuonyesha kwamba mapinduzi hutokea endapo hatua fulani za kitawala zimekosa kuchukulia. Johnson (1968) ameshauri tawala zitafute hali zinazosababisha mapinduzi kusudi zididimizwe kabla hazijalipuka. Lengo la Johnson ni uzuiaji wa mapinduzi ili tawala zilizoko ziendelee kuwepo. Utafiti wake ni mpungufu. Kama ijulikanavyo hatua za kuzuia mapinduzi wakati mwingine hujikinza zenyewe.[2] Hatua zilizopendekezwa zikakosa kufaulu bali zikaliongezea kasi gurudumu la mapinduzi.

Kwa maoni yetu utawala huenda ukajua udhaifu na upungufu wa uongozi wake lakini ukashindwa kujitanzua kutoka kwa makucha ya mikinzano ya kisiasa, kiuchumi na kijamii iliyosababishwa na utawala huo huo. Utawala hapo hujikuta umejikinza wenyewe kwa sababu, katika hatua zake za kimaendeleo, huacha vitanzi ambavyo baadaye huukaba koo na kuuzuia usiendelee kuwepo. Pendekezo la Johnson kwa hivyo huenda lisitufaidi sana kwa sababu hata tukijua hatua ipasayo kuchukuliwa huenda tukashindwa kuichukua.

Mkabala wa uzuiaji vile vile unapuuza hali zingine zilizoko mbali na jamii hiyo maalum lakini ambazo huenda zimekuwa na nafasi kubwa katika kuyalipua mapinduzi.[3] Kwa mfano, uwezekano wa mawasiliano baina ya nchi moja na nyingine huleta maenezi na nadharia ya kimapinduzi. Aidha, kufaulu kwa mapinduzi katika taifa moja huweza kulipa taifa jingine ilhamu na mwamko wa kisiasa kusudi nalo liweze kujikomboa. Kwa mfano, vuguvugu la kimapinduzi katika mataifa ya Cuba na Vietnam lilitoa ndimi na miale na liliamsha hisia za kimabadiliko katika mataifa mengine ya kilimwengu.

Nadharia ya Ki-marx imeipa mikinzano ya kitabaka nafasi kubwa na pevu katika usababishaji na uimarishaji wa mapinduzi.[4] Mkabala huu unashikilia kwamba historia

ya mataifa ya kilimwengu ina ithibati maridhawa za mivutano baina ya tabaka linalomiliki nyenzo kuu za uzalishaji mali na lile linatotumia nguvu za mwili kujitarazaki. Uhasama uibukao kwa sura ya mikinzano, kwa hivyo, una misingi ya kiuchumi. Wale wanaomiliki nyenzo kuu za uzalishaji mali hung'ang'ania thamani ya ziada kubwa iwezekanavyo il hali wale wanaokandamizwa hutaka kujihami kwa kuzuia nguvu na jasho lao visitumiwe sana kwa manufaa ya wachache. Kwa hivyo, huwa kuna vita vya kila wakati; wafanyakazi huunda vyama vyao nao waajiri wakishirikiana na utawala hujitahidi kupunguza nguvu za vyama hivyo kwa kuviingilia na kuwahasi viongozi wake. Al'muradi makundi haya mawili hutazamana na kukabiliana kwa uhasama. Mikinzano yake mara huwa wazi ikabainika lakini mara nyingine hujisetiri na baadaye hujitokeza kwa kishindo.[5]

Lenin (1939:25) ameonyesha mkinzano ulio muhimu zaidi katika enzi ya kimwinyi na kibepari. Mkinzano huu ni kuwa uzalishaji mali hufanywa na jamii kwa ushirika, lakini katika matumizi ya kitu hicho kilichoundwa kwa nguvu za pamoja, ni kundi dogo tu linalofaidi. Uzalishaji unakuwa wa kijamii lakini matumizi yanakuwa ya kibinafsi. Fauka ya hayo, thamani ya ziada ipatikanayo haitumiwi kuinulia wala kustawishia hali ya maisha ya umma kwa jumla bali

inatumiwa kuwafaidi wale wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Kwa mfano, katika Asali Chungu taswira ya mzee Uledi, mwangalizi wa bustani ya Zuberi, inatuthibitishia jambo hili:

> Yeye, tokea ujana wake mpaka leo, ametumikia katika jumba hili. Hana hata tambara la kuvaa, zikwambii akiba ya haja. Nguvu zake za ujana zilimfaa babu-mtu; za utu uzima baba-mtu; za uzee alimmalizia mwana-mtu, Zuberi. Hana alichobakiwa nacho ila mifupa na ngozi. (uk. 11).

Hali kama hiyo, kwa vyovyote, husababisha migogoro ya kitabaka ambayo ikielekezwa kinadharia huenda ikaleta mapinduzi.

Mivutano haipatikani baina ya tabaka moja na lingine peke yake bali pia hupatikana hata humo mwenye tabaka moja.[6] Aghalabu kiini cha mivutano katika tabaka moja ni mashindano miongoni mwa watu wa tabaka hilo. Katika tabaka lisilokuwa na nguvu za kiuchumi, mivutano hii hutokana na kutomfahamu vyema adui anayesababisha udhaifu wao. Mivutano huwa ni baina ya wao kwa wao na kwa namna hiyo wanahisi kama kwamba wamemwahi adui. Aidha, mivutano huweza kutokea kwa sababu ya uhaba wa mtaji miongoni mwao.

Mivutano ya kila siku miongoni mwa wafanyakazi kuhusu mishahara, usalama kazini, hali ya kazi, mavazi ya kazini na kadhalika yapasa ichukuliwe kama mikinzano ya kisiasa hata ingawa haikujitokeza moja kwa moja kama sehemu mojawapo ya mapambano ya kisiasa.[7] Katika undani wake mivutano hii huwa imelenga katika mabadiliko ya kimsingi lakini haipati mwelekeo mpaka pale itakapoelekezwa na itikadi na nadharia mufti.

## 3.3 MIKINZANO BAINA YA MATABAKA

Migomo inayojadiliwa na Adam Shafi katika Kuli na Said Ahmed katika Dunia Mti Mkavu ilikuwa ni hatua muhimu katika siasa za visiwani kabla ya mapinduzi na ilikuwa kichocheo kizuri cha fikra za kimapinduzi zilizolipuka mnamo 1964. Ilhamu yao ni mgomo wa wafanyakazi bandarini mnamo 1948. Aidha, yumkinika Said Ahmed vile vile amehamasishwa na mgomo wa mafalahi na wafugaji wa 1951.

M.S Khatib (1983:17) amesema hivi kuhusu riwaya ya Kuli:

> Kuli ni riwaya ya kimaendeleo kama inavyojinasibisha na harakati za kitabaka zilizochomekwa Zanzibar mwaka 1948, kati ya kambi ya maproletari na ile ya mabepari wanaotetea uchumi wa

> makampuni yao. Uchumi huo hauwafaidi tu mabepari wachache wanaowakilisha mfumo mzima wa ubeberu, bali pia, daula za kibepari zinazoonekana kufai ika. Meli kadha wa kadha huegesha bandarini tayari kuhaulisha malighafi.

Nayo Dunia Mti Mkavu imeutumia mgomo wa makuli bandarini Zanzibar dhidi ya kampuni ya Smith Mackenzie na ule wa mafalahi dhidi ya serikali ya kikoloni kuelezea mikinzano mikali iliyokuwepo kabla ya mapinduzi.

Maandishi ya kihistoria[8] yanatwambia kuwa mnamo 20/8/1948 kulitokea mgomo wa makuli bandarini Zanzibar. Mgomo huu ulitokana na ukosefu wa usalama wa kikazi miongoni mwa wafanyakazi wa bandarini. Kwa sababu kulikuwa na watu wengi waliohitaji kazi, kampuni ya 'African Wharfage' iliyokuwa bandarini Zanzibar iliwafanya wengi vibarua wa siku kwa siku. Wafanyakazi wakagoma. Waajiri nao wakakata kauli kuwaajiri watu wengine. Jambo hili liliufanya mgomo usambae miongoni mwa wafanyakazi wote wa Kiafrika mjini Zanzibar. Aidha, mgomo huu uliungwa mkono na maskwota na mafalahi waliokuwa wakiishi katika mashamba ya karafuu na

LIBRARY

viungani vyake (Jabir 1977:195-196). Mafalahi waligoma kupeleka vyakula katika soko kubwa la Mji wa Mawe. Ushirikiano huu, ambao ni kielelezo cha kukaribiana kimtazamo baina ya wafanyakazi na mafalahi kwa sababu maslahi yao ni sawa, uliendelea hadi mgomo ulipomalizika mnamo 10/9/1948.

Kitendo hiki cha mafalahi hakikuwa cha kisadfa bali kilitokana na ukweli wa kihistoria kwamba hakuna binadamu anayependa idhilali bali daima yuko mbioni kuibadili hali inayomkandamiza ili imfae (Freire 1972:21). Mnamo 1944 kulikuwa kumetokea ugonjwa wa Sotoka, Zanzibar.[9] Matibabu yaliyotolewa na madaktari wa ng'ombe yalisababisha vifo vya ng'ombe thelathini na watatu. Hili lilifuatiwa na ng'ombe wengi kupelekwa majoshoni dhidi ya maradhi ya dingana na magonjwa yaletwayo na kupe. Mafalahi walilazimishwa kulipa ada ya majosho. Kwa sababu ya tajiriba ya hapo awali, waliona kana kwamba hii ni jitihada ya kuwafanya masikini zaidi kwa kuwamaliza ng'ombe wao (Jabir 1977:200).

Mnamo 1951, maradhi ya kimeta yalizuka Kiembe Samaki na kusababisha kile kilichojulikana kama 'Vita vya ng'ombe' (Lofchie 1965:148). Wenye magari ya ng'ombe wakapinga kuchanjwa kwa ng'ombe wao. Hali kadhalika, baadhi ya mafalahi wakakataa kata

kata uchanjaji huo. Wenyeji kumi na tisa waliokaidi amri ya serikali kuhusu chanjo za ng'ombe wakapelekwa kortini kujibu mashtaka. Mnamo siku ya hukumu 30/7/1951 wenyeji wengi wa Kiembe Samaki walienda kortini huku wamebeba marungu na mawe. Wakaizingira mahakama. Baada ya hukumu walivizia gari walimokuwa mahabusu. Wafungwa kumi na mmoja wakaokolewa. Umati huu ukajaribu kuingia Jela kuu ili kuwahurisha wafungwa wengine. Askari wakapiga risasi na watu watano wakauawa papo hapo (Jabir 1977:200-201).

Kwa maoni yetu migogoro hii ndiyo iliyofinyangwa kisanaa ikajitokeza kama Kuli na Dunia Mti Mkavu.

Dunia Mti Mkavu ni riwaya inayoonyesha kinagaubaga mikinzano ya kitabaka iliyoashiria mapinduzi. Mwandishi ametumia tajiriba za ndugu wanne - Fumu, Bakari, Pandu na Kibwana - kusimulia mfumo mzima wa visiwani kabla ya mapinduzi. Aila hii ya Jaku imetawanyika kwa sababu ya ugumu wa maisha. Kutawanyika huku ni jazanda ya ukosefu wa ushikamano katika familia mbalimbali.

Bi Pole na Jaku wanabidika kuigawia dunia watoto wao kwa sababu hawawezi kuwakimu. Hawatengani na watoto wao kwa hiari bali kwa sababu wamevurugwa-vurugwa na ulimwengu na walimwengu wasiojua simile.

Kibwana Jaku ananunuliwa na Bi. Nafisa na kwa namna hiyo anainuliwa kitabaka ili aweze kukinzana na ndugu zake. Nafasi yake mpya inamfanya amfungishe babake huku akijua huyo mzee hana hatia. Baadaye anaamrisha ndugu zake wapigwe risari. Hili latuonyesha kwamba katika mikinzano ya kitabaka udugu wa uzawa hupuuzwa na hulazimika kutii amri za tabaka.

Mikumbano ya Fauz na Fumu ni kielelezo cha kiwango ambacho mafalahi wanaweza kudhiliwa na kuwekwa pembezoni kiuchumi na kijamii na tabaka la mamwinyi (Mazrui 1984:200). Fumu anazuiliwa kulima wala kufaidi kutokana na vipando vyake. Vile vile anakatazwa kulisha mifugo yake katika shamba la babake Fauz. Baadaye Fauz na Makame (babake Masika) wanashirikiana kuchoma mimea ya Fumu. Kisa na mkasa ni kwamba Fauz anamtaka mpenzi wa Fumu, Masika. Migogoro na uhasama baina ya mavulana hawa wawili unachangisha katika kumzindua Fumu apate kuona asili ya maonevu anayofanyiwa.

Hata mzee Gae, ambaye hasa ni nafsi ya mafalahi, amejikuta katika mikinzano ya kitabaka. Mikinzano hii imeanza kitambo na imemfanya aonekane kama mwendawazimu. Hali hii inatokana na ukweli kwamba hawezi kulielekeza tabaka lake katika usuluhishaji

wa mikinzano hiyo. Yake ni matusi na masuto yasiyokuwa na kina cha kinadharia au itikadi ya wazi iwezayo kuzikusanya hasira za muda mrefu na kuzitumia ili kulisukuma mbele tabaka lake.

Mikinzano baina ya mzee Gae na tabaka-tawala inawakilishwa na mikwaruzano yao ya mara kwa mara kabla na baada ya kushirikiana na akina Kumba, Pandu, Fumu, Bakari na kadhalika kuukabili utawala wa kikoloni. Wakati akijaribu kuuamsha urazini wa Fumu, anatwambia:

> Walinivunja kichwa changu kwa nyundo,....... nyundo..... yah nyundo; yah, walinivuruga, walikivuruga kichwa changu.... waliparaganya, hay waliparaganya ubongo wangu, na halafu waliniita mbwa, dog, yah, mimi mbwa. Na mara nyingine waliniita Mswahili mwendawazimu. Walinitesa kama.... he, he, he.... walinitesa kama mnyama. Kwa sababu .... kwa sababu nilithubutu kuwaambia ukweli (uk. 2-3).

Ingawa kwa hakika kichwa cha mzee Gae 'kilivurugwa' na'kuparaganywa', mawazo yake kuhusu utu ni ya kimsingi. Kulingana na mzee Gae binadamu anayestahiki

jina hilo ni yule anayejisaili nafsi yake ili ajielewe. Uwezo wa kujisaili unakuwa uti wa mgongo wa ubinadamu. Hiki ni kipawa kisichomilikiwa na kiumbe mwingine isipokuwa binadamu. Kama vile Jusper wa Betrayal in the city ambaye japo aambiwa ni mwendawazimu anadhihirisha welekevu na busara kubwa, mzee Gae ana falsafa pevu lakini ambayo itapasa ielekezwe ili iwe ya manufaa badala ya kubaki katika kiwango cha dhahania tu. Falsafa hii baadaye inaelekezwa na wafanyakazi wa mijini wakiongozwa na Kumba.

Hali ya mzee Gae ya kiwendawazimu na hasira na ghadhabu za Fumu ni matokeo ya mikinzano ya kitabaka. Lakini wote ni kama kwamba wamehasiwa kwa sababu hawafui dafu dhidi ya uwezo, utajiri na nguvu za mamwinyi. Wamebaki kupiga 'makelele' tu.

Viwandani na bandarini, tunakumbana na mikinzano baina ya wafanyakazi na mabepari. Kazini panakuwa pahala pa kulaani mabwana wa kazi na kuubeza na kuukashifu mfumo wa kazi (uk. 51-52). Panakuwa pahala pa kulia yamini kwamba itabidi mambo yabadilike. Kiwango cha urazini wa kisiasa kinapanda kutokana na mikinzano ya siku kwa siku na vile vile kutokana na juhudi za Kumba.

Kumba, ambaye amepewa jina la majazi lenye maana ya kukabiliana ana kwa ana, ni mfano wa waasisi[10]

wanaoelewa vema kule umma utokako na kule uendako. Hana hamaki za wafanyakazi wenzake wala 'makelele' ya mzee Gae bali ni mpole, mweledi na makini. Ni mwanamapinduzi anayeweza kuwakumba wenzake kwa mawazo yake yenye kina, maki, dhati na hisia; utulivu wake, ukweli wake, mkato wa maneno yake, imani, busara na ubinadamu wake. Kumba anajitahidi kuwaunganisha watu wanaonyanyaswa ili washirikiane katika kuzikabili nguvu za kibepari na kikoloni. Kutokana na hotuba zake anaweza kuonyesha umoja wa mafalahi, wafanyakazi na watamba-na-njia kama jambo muhimu katika kufanikisha mabadiliko ya mfumo wa maisha.

Kiongozi huyu wa wafanyakazi anawapa wenzake matumaini kwa kuufungamanisha mustakabali wao na wa mataifa mengine ya kilimwengu. Anawaambia:

> Pigo la vita na hasara waliopata: nchi moja ya Afrika ya Magharibi iitwayo Gold Coast, inadai uhuru wake, na hapo nyuma mzungu amejifunza vya kutosha alipolazimika kuipa Uhuru Bara Hindi, na isitoshe msukosuko wa Misri na mwamko wa siasa wa nchi nyingi; haya yote, pamoja na ughali wa maisha na upandaji wa bei ya vitu utamfanya Mzungu

> akaze kamba.... Lakini sisi makuli
> hatutoshi kufanya mgomo, lazima
> wachukuzi washirikiane nasi; pia
> wazururaji wasio na kazi.... (uk 52).

Analosema Kumba ni kwamba utawala wa kikoloni unaouhimili umwinyi wa Waarabu unatikisika kutokana na mikinzano ya kilimwengu na ya ndani. Kwa hivyo, wafanyakazi wana jukumu la kuuangusha. Lakini hawawezi kufanya hivyo peke yao. Lazima washirikiane na matabaka mengine yanayonyanyaswa.

Tabaka ambalo ni jepesi kushirikiana na wafanyakazi ni la mafalahi. Katika riwaya hii mkinzano unaoleta ushirika unahusu uchanjaji ng'ombe. Mafalahi wanagoma kupeleka ng'ombe wao wakadungwe sindano kwa hofu kwamba watakufa. Hili haliwashughulishi mabepari wa Kiingereza. Kulingana na 'Mr' Jackob ng'ombe hao lazima wadungwe sindano kwa maslahi ya wazungu. Hawangetaka 'vinyama vyao viambukizwe maradhi.' Mzungu analinda maslahi yake na Mwafrika anatetea maslahi yake. Hali kama hiyo ingeleta mvutano na ingesahilisha muungano wa wafanyakazi na mafalahi.

Mikinzano ya kitabaka inayozungumziwa na mzee Gae na Kumba haiwasibu mafalahi au wafanyakazi kwa <u>ujumla</u> wao tu, bali pia, katika <u>ubinafsi</u> wao. Katika

Dunia Mti Mkavu tuna mikinzano ya Fumu, Fauz na Masika ambayo tumeitaja hapo juu. Masika, kama vile Radhia katika Utubora Mkulima, ni mfano wa mwanamke aliyepevuka kiurazini hivi kwamba anastahabu kuoa fukara mradi pana mapenzi ya dhati. Kupigana na Makame, Hamoud na Shehe ni ishara ya juhudi yake ya kukataa kuungana na tabaka ambalo analiona likidhulumu. Mapambano haya yanafikia kilele Masika anapowaua Fauz na Farouk Hilal.

Mikinzano hii ya kibinafsi ni sehemu ya mikinzano ya kitabaka na inachangisha katika kuyalipua mapinduzi.

Tukiirejelea riwaya ya Kuli tunakumbana na mikinzano kama ya Dunia Mti Mkavu. Riwaya ya Kuli inaeleza kuhusu mikinzano iliyokuwepo bandarini mnamo 1948. Wafanyakazi kama Majaaliwa walivunjwa na kazi na kizazi chao kikaendelea na kazi zao ili kujitarazaki. Wafanyakazi wengine waliumia na kampuni haikuwapeleka hospitalini lakini badala yake ilipendekeza wapelekwe nyumbani. Mwandishi anasema:

> Hii ndiyo mandhari Rashid aliyoikuta bandarini. Hapa ndipo baba yake aliponyonywa uhai wake akafa bila chochote. Unguja bandarini. Mwaka 1948. (uk. 9)

Bandarini, wachukuzi wanapeleka magunia ya karafuu na kuyatia ghalani ndani ya mabanda ya CGA. Wengine wanapakia na kupakua meli za kutoka mataifa mbalimbali. Bandari hii inadhihirisha Zanzibar kama kituo muhimu cha ubepari wa kilimwengu na wafanyakazi wanajikuta katika makucha ya mfumo wenye pupa ya kupata rasilmali na malighafi mbalimbali kutoka 'Ulimwengu wa Tatu.' Adam Shafi anatwambia kwamba meli zilitoka Uholanzi, Ugiriki, na Dar-es-Salaam.

> Zuberi anamwambia mzee Tindo
> 'Si umeiona ile meli ya Holland
> iliyoko nje kabisa?'
> 'Ipi? Ile iliyoko karibu na meli
> ya mafuta ya Kigiriki?
> 'Ndiyo! Basi Wallahi tunapakia
> mapipa ya nazi mpaka hivi sasa....
> ... Nimemsikia yule afisa aliyekuwa
> akitusimamia akisema wana safari
> ya Dar-Salama kwenda kupakia mkonge.
> (uk. 42)

Katika hali kama hiyo ya ufanyakazi, mabepari watawaponza wfanyakazi kusudi wapate thamani ya ziada kubwa iwezekanavyo. Wafanyakazi wanafanya kazi inayowapa tija kubwa mabepari lakini wanapewa mshahara mdogo 'wa kuwaweka hai hadi siku ya pili.'

Si ajabu kwamba Rashidi na wenzake wanalihisi jambo hili. Rashidi anasema:

> Mnajua nyie?.... mie nahisi
> hawa matajiri tunaowafanyia
> kazi wanapata faida kubwa
> na sisi wanatulipa pesa
> kidogo kweli kweli (uk. 44)

Hisia za Rashidi zina ukweli. Gharama ya jasho la mfanyakazi ni sawa na wakati unaohitajika ili kumpa mfanyakazi na aila yake bidhaa za msingi wa uhai wao ili aendelee kuzalisha mali zaidi (Anderson 1974:20). Mapato ya juu yanamfaidi mwajiri.

Mbali na nyongeza ya mishahara, wafanyakazi wanadai wapewe nguo za kazi na wawe na dhamana kamili juu ya maisha yao kwa sababu ya ajali za bandarini. Badala ya kuzingatia madai haya, mabepari wanaendelea na dhuluma na vitimbi vyao. George anazidisha masuto, laana na upiganaji makofi.

Wafanyakazi kama manafi wanaendelea kufa wakiwa kazini.

Kwa upande mwingine wafanyakazi wanazidi kupevuka kiurazini. Jambo hili linamfanya Rashidi aone uhusiano wa mabepari wote. Analipuka:

> Bepari ni bepari tu, akiwa
> Mhindi, Mzungu au kabila lolote
> lile (uk. 68)

Vipi watakuwa tofauti ilhali mkabala wao kuhusu maisha ni mmoja? Wote wana lengo moja: kujitajirisha upesi iwezekanavyo na kwa njia yoyote ile. Ukweli huu ndio unaolipua mikinzano iliyoko katika Kuli.

Polisi na mahakama; kama taasisi za utawala, zinatumiwa kuwaua na kuwafunga viongozi wa migomo. Katika kufanya hivyo, taasisi hizi zinaungana mkono na umwinyi na ukoloni wa Kiingereza kuhalalisha dhuluma kwa wafanyakazi.

Kwa hivyo, katika Kuli, Adam Shafi anatuonyesha wafanyakazi wakiongozana katika kujiandaa kukabiliana na waajiri wao. Baadhi yao kama Bakari, Faraji na Rashidi wanajitolea kwa moyo wa dhati ilhali wengine kama mzee Tindo 'wananunuliwa'. Usaliti wa wafanyakazi si jambo geni katika fasihi ya Kiswahili kwa mfano katika Kilio cha Haki, Tereki anaruka upande wa pili na anashirikiana na Delamon dhidi ya Lanina na wafanyakazi wale wengine. Usaliti ni jambo la kawaida mikinzano ya kitabaka inapochacha lakini kama tunavyoonyeshwa katika Kilio cha Haki, Kuli, Dunia Mti Mkavu na Mukwava wa Uhehe, wasaliti hurudisha nyuma jitihada za ukombozi.

Ingawa mikinzano ya Kuli hailipui mapinduzi, inaubabaisha utawala wa kikoloni ukishirikiana na umwinyi wa Waarabu na inaashiria harakati kali zinazofikia

upeo wake miaka kumi na mitano baadaye.

Katika Kasri ya Mwinyi Fuad hatima ya mikinzano ya kitabaka inawakilishwa na jazanda ya uhusiano baina ya Boby na Fuad. Fuad anamtumia Boby kama chombo cha kujifunzia ubwana kwa kumwamrisha amletee vitu mbalimbali. Siku nyingine Boby hukaidi amri na hapo hupigwa vibao. Lakini siku moja stahamala zinamwisha Boby na anamfukuza Fuad.

Jazanda hii inaonyesha uwezekano wa tabaka linalokandamizwa kukaidi amri na kukinzana moja kwa moja na tabaka linalokandamiza. Maimuna anamwonya mwanaye:

> Siku zote n'akwambia! Usimpige
> Mbwa huyu, atakutafuna siku
> moja (uk. 11)

Uwezekano wa kuvunjika kwa tabaka lake baada ya mikinzano ya kitabaka ndio unaomzidishia ugonjwa wa moyo Bw. Malik na muda mfupi baadaye anafariki.

Yapasa kifo cha Malik kichukuliwe kama kushindwa kwa umwinyi kustahimili mikinzano ya kitabaka. Mamwinyi wale wengine kama Zuberi na Amina katika Asali Chungu, Fuad na Adila katika Nyota ya Rehema, Mwinyi katika Kiu na Hamoud na Fuad katika Dunia Mti Mkavu wanafariki. Vifo vyao ni ishara kwamba

wameshindwa kusuluhisha mikinzano waliyoisababisha wao wenyewe.

Uhusiano wa wanawake na mwamwinyi katika Kasri ya Mwinyi Fuad hautofautiana na wa riwaya hizo zingine. Fuad anajaribu kumbusu Mariam kwa lazima. Aidha, anajaribu kumvamia mkongwe, mjukuu wa mzee Sharwani. Hawa ni wafanyakazi wake. Ni bayana kufikia sasa kwamba mwanamke katika mfumo wa kimwinyi ananyanyaswa maradufu. Ananyanyaswa kama mfanyakazi kwa sababu jasho lake linatumiwa kutengenezea thamani ya ziada kwa manufaa ya mtu mwingine. Tena, anadhulumiwa kama mwanamke kwa sababu anavuliwa utu kwa kutumiwa kama chombo cha kuzimulia ashiki. Visa vya Masika, Semeni, Mariam; Mkongwe na Rehema vinatuthibitishia jambo hili.

Kwa hivyo, mikinzano baina ya wanaume na wanawake haina budi kuchunguzwa katika muktadha wa kiuchumi na kijamii. Nao ukombozi wa wanawake ni sehemu muhimu ya ukombozi wa taifa zima.[11]

Kasri ya Mwinyi Fuad (uk. 18) inatwambia:

> Umasikini ulikuwa umejaa nchini na unyonge umewazonga wananchi. Hata hivyo, au kutokana na dhiki hizo wafanyakazi hawakwisha kufanya migomo, maandamano na mikutano ya hadhara na

LIBRARY

> ya siri ya kupinga mabepari na
> makabaila na kudai uhuru kutoka
> kwa wakoloni.

Kulingana na Adam Shafi, mikinzano ya kitabaka inayojitokeza kama migomo, maandamano na mikutano ya siri ililenga katika ukombozi wa kudumu. Jambo hili linatokana na umaskini na unyonge unaowazonga wananchi katika Kasri ya Mwinyi Fuad.

Kielelezo cha unyonge huo ni Kijakazi ambaye maisha yake ni ya kinyama. Hawezi kamwe kuyaelewa mazingira yake wala kuwa na matumaini kwamba maisha yake yanaweza kubadilika. Furaha yake kubwa ni kusifiwa kwamba ni mfanyakazi hodari na mwenye juhudi. Anamwambia Mkongwe:

> Mimi, shoga yangu, nitamaliza
> maisha yangu hapa hapa. Hapa
> ndipo nilipoanzia na hapa ndipo
> nitakapomalizikia (uk 28)

Yaani katika uhai wake, kijakazi hatarajii kupiga hatua yoyote kuyaboresha maisha yake. Hajui wala hajali juhudi zinazofanywa kusuluhisha mivutano ya kitabaka kwa njia ya mapinduzi. Anadhamiria kuuendeleza utumwa kwa kuchukulia hali yake kwamba ni jambo la majaaliwa asiloweza kujiepusha nalo. Kwa upande mwingine, anachukulia utukufu wa akina Fuad

kuwa unatokana na kudura za Mungu na kattu hauwezi kufutika. Fikra hizi finyu zinatokana na imani za kidini na, vile vile, kutokana na maisha ya kukatisha tamaa iliyokuwepo visiwani.

Kwa kawaida, kadri mivutano ya kitabaka inavyokuwa mikali ndivyo tabaka linalokandamiza linavyozidisha dhuluma na chuki. Hii ndiyo hali tuionayo katika Kasri ya Mwinyi Fuad. Mafalahi wengi wanafukuzwa kazini. Wakati wa usiku wanafanya mikutano ya mara kwa mara Kijangwani ili kutafuta njia za kujipa afueni. Huku wakishirikiana na wafanyakazi wa mijini wanafanya mipango kununuliwe shamba la Dambwe ili yeyote afukuzwaye kazi apate makazi. Shamba hili vile vile lingetumiwa kama kituo cha kuwaandalia wanamapinduzi.

Kununuliwa kwa shamba, Zanzibar, kabla ya mapinduzi ni jambo lenye uhalisi wa kihistoria. Chama cha ASP ambacho kiliwakilisha maslahi ya wanyonge kilifanya jitihada mbalimbali dhidi ya mamwinyi. Chama kilinunua shamba Kilombero na kuwahamisha Waafrika wote waliofukuzwa mashamba ya mamwinyi. Pia waliwahimiza wasusie mabasi na maduka ya Waarabu.

Mikinzano ya kitabaka inapofikia kilele chake, matabaka hujiandaa ili kukabiliana. Kwa hivyo, hatua ya kujiandaa kwa kununua shamba la siri licha ya kuwa

na uhalisi wa kihistoria, ni ishara kwamba Shafi Adam Shafi anafahamu umuhimu wa maandalizi kabla ya kulipuka kwa mapinduzi.

Ingawa tunakumbana na mikinzano katika Asali Chungu, Kiu, na Nyota ya Rehema hatuonyeshwi maandalizi ya kifikra na ki-zana kama sehemu muhimu ya kuelekeza vuguvugu la kisiasa. Dunia Mti Mkavu inatuonyesha maandalizi kwa kadri inavyosimulia jitihada za matabaka kuungana ili kutoa pigo kama nguvu moja. Kuli inatusimulia kuhusu umoja wa wafanyakazi ndani na nje ya nchi na nafasi ya chama chao katika kuwahimiza na kuwashajiisha.

Mikinzano katika Kiu inajitokeza kuhusiana na kiu mbalimbali za wahusika wake. Kila mhusika ana jambo analolitamani kiasi cha kumpofusha asione upande wa pili wa jambo hilo. Mwinyi anamtamani Bahati lakini tamaa hii haikujikita katika udhati wa mapenzi. Mwinyi ni tajiri mkubwa mwenye Benzi, shamba na nyumba kubwa yenye 'zulia zuri ambalo thamani yake ingetosha kumfariji maskini kwa siku na miezi' (uk.1) Ingawa ana umri wa miaka 62, Mwinyi anaamini kwamba maadam 'Mkurufunzi ni pesa' anaweza kupendwa na msichana mbichi kama Bahati. Kama vile mamwinyi wale wengine kama Fuad, Fauz na Zuberi, Mwinyi hawezi kutafakari kwamba anaweza kukataliwa na msichana wa

tabaka la chini. Amezoea kumiliki vitu na watu na kwa hivyo hawezi kuhimili pigo la kukataliwa na Bahati.

Ingawa mwandishi wa Kiu anatusimulia kuhusu mikinzano ya kitabaka kabla ya mapinduzi analikatisha tamaa tabaka linalonyanyaswa kwa sababu haonyeshi matumaini yao ya kuyasuluhisha matatizo yao. Tunakubaliana na Senkoro (1982:15) kwamba mikinzano ya Kiu haisuluhishwi.
Senkoro anasema:

> Amepuuza ukweli wa wazi kwamba Bahati, mamake, na hata Idi wote wana kiu ambayo kiini chake kinapatikana katika uhusiano wa uzalishaji mali katika jamii yenye matabaka ambayo inawatajirisha wachache na kuwafanya wengi maskini. Riwaya hii imepuuza vipengele vya matabaka ya kijamii, na kwa hivyo imeonyesha kimakosa hali ya maisha visiwani kama yenye kukatisha tamaa, yenye kukanganya na yenye tajiriba ya kutamausha ambayo inawaonya watu kama Bahati wasipambane hata kidogo.

'Kiu' yote haimwelekezi mtu katika maangamizi kwani kuna 'Kiu' nyingine ambayo ikielekezwa vema, yaweza

kuleta ukombozi.

Katika Nyota ya Rehema tunamwona Sulubu akivutana na mamwinyi wenye mashamba. Inaonekana kwamba Sulubu anafahamu ukorofi wa mamwinyi na kwa hivyo anahamahama kutoka shamba moja hadi jingine ili kuepukana na kulipa kodi au kudhulumiwa kwa namna nyingine.

Sulubu ni mhusika mwenye utu na huruma katika ulimwengu wenye uroho na ubinafsi mwingi. Hajachafuliwa na mazingira yake kama vile wahusika wale wengine wanavyochafuliwa bali anajitahidi kuyamiliki na kuyabadili kwa kuyafanyia kazi. Lugha yake ya kishamba inatuonyesha kuwa amejiepusha na taathira za mji na upotovu wake na kwamba asili yake ni bara. Ingawa anapata nafasi nzuri ya kumvua Rehema heshima yake wakati wakiwa porini peke yao, hafanyi hivyo. Anamtibu na kumlisha. Binadamu huyu mpole na mwenye utu anajikuta akikizana na pupa ya akina Karim.

Karim, mudiri wa mjini, anashirikiana na watu wa tabaka lake kama Mudiri wa Ramwe, kuharamisha urithi wa Rehema wa shamba la Ramwe. Hatua ya kwanza ni kuonyesha kuwa Fuad hakuacha zaidi ya watoto wawili: Samir na Salma. Wanatoa ithibati ya cheti cha tabaka kuonyesha kuwa Rehema alizaliwa nje ya ndoa na kwa hivyo si mrithi wa mali ya Fuad. Sulubu

na Rehema wananyang'anywa shamba la Ramwe ..

Mvutano unaosababisha kifo cha Karim unatokea pale Karim anapotaka kulichukua shamba la Pakani. Anamwambia mkewe:

> Leo darling, ntakufundisha sheria kidogo. Mtu yeyote akichuma mali kwa kutumia mali isiyokuwa yake, basi mali hiyo aliyoichuma pia si yake.... sheria hii ipo, na sisi tutaitumia kupata pesa kidogo, angalau kulipalipa madeni. Unajua kuwa wale watu waliokuwa wakikaa katika shamba lako la Ramwe walighili katika shamba jingine huko upande wa Pakani? Raha yenyewe Pakani imo katika jimbo la sahibu yangu mmoja! (uk. 164)

Kwa hivyo, Karim na kundi lake wanajiandaa kutumia sheria na mabavu kusudi wawaumize kiuchumi Rehema na Sulubu. Lakini kila stahamala ina kikomo chake. Karim anauawa na Sulubu. Mauaji ya Karim ni kilele cha miaka mingi ya mivutano ya kitabaka. Ni ishara kuwa binadamu hufikwa na wakati akaacha 'kuhamahama' bali akafanya KITENDO kitakachosaidia kukomesha idhilali. Kitendo hiki kinatuonyesha kuwa udhalimu

wa mamwinyi umevuka mipaka.

Karim amewadhulumu watu wengi kwa sababu ana ulinzi wa mfumo wa uzalishaji mali. Ana masahibuze wenye vyeo na wanaompa nguvu. Ana elimu, uwezo, cheo na utajiri. Lakini uzoevu wake wa kula mali ya watu unabidi ukomeshwe na mmojawapo wa wanyonge: Sulubu. Hali hii yapasa ichukuliwe kama kielelezo cha kilele cha mikinzano baina ya matabaka yenye uhasama.

Mwandishi anatwambia:

> Kesi ya Sulubu kumwua
> Karim ilitia vuguvugu nchini na
> kulipua mwamko wa kisiasa.
> Sauti za wanyonge, moja ikiamsha
> nyingine zilivuma na kuhanikiza
> (uk. 168)

Mvumo huu wa sauti zilizowiana katika ujumbe wake kuhusu idhilali na maonevu dhidi ya wanyonge, uliwaunganisha wanamapinduzi katika kuiondoa serikali ya kisultani.

Ushirika baina ya Rehema na Sulubu ni kielelezo cha ushirika wa wanyonge wenye maslahi sawa. Mvutano baina ya Aziza na Rehema, kwa upande mmoja, na Fuad na Adila, kwa upande mwingine, una misingi ya kitabaka na umefangamana na ubaguzi wa rangi. Aziza

ni kizazi cha Waafrika maskini wenyeji wa visiwani. Wazazi wake walikuwa wasimamizi wa shamba la Ramwe. Anapomzaa msichana anayemlanda nyanyaye, anatengwa. Fuad anamwoa Adila, karani wa Bwana D.M. Patel. Tunaambiwa rangi ya Adila ni ya hudhurungi na "nywele zake nyeusi, laini zilikuwa zikianguka kwa mawimbi juu ya mabega yake yaliyoinuka" (uk. 11). Yamkini dharau ya Adila kwa Rehema haitokani na umama - wa - kambo tu bali pia na tofauti zao za rangi. Kwa hivyo, kutaradadi kwa Rehema mjini hakutokani na majaaliwa lakini kunatokana na kubaguliwa kwake. Aidha, anajikuta amenaswa na makucha ya mapapa wa mjini kama akina Mansuri ambao wanamhadaa kwa raha na mavazi na kwa jinsi hii wanambingirisha katika uoza mkubwa wa kijamii. Tunaambiwa:

> Muda si mrefu, alikuwa keshaingia na kutoka katika hoteli zenye kutambulikana, kesha garagara katika mchanga, wa pwani zenye kuvutia, keshaegemea makochi ya gari za fahari, keshaingia na kutoka katika nyumba za watu wenye kujipata (uk. 75)

Katika mahangaiko na mikinzano yake na mazingira yake, Rehema hakumbani na kiumbe mwenye utu

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

isipokuwa Sulubu. Wengi wa wale wanaomsaidia wanafanya hivyo huku wakitarajia msaada wake - tangu Mansuri, Idrisa na marafiki wengine wa kiume na kike. Binadamu ana uwezo wa kughairi mwendo wake na hulka zake. Rehema anayakinai maisha ya fujo za mijini na anakata kauli kushirikiana na Sulubu katika kuyakabili mawimbi ya mazingira. Wanyonge wawili wanaungana kuyapanga maisha yao lakini muungano huu unazidisha mikinzano ya kitabaka inayoiva na kulipuka.

Kwa hivyo, basi, Mohamed Suleiman Mohamed katika Nyota ya Rehema anaonekana kuamini kwamba kufurutu kwa mikinzano ya kitabaka ndiko kunakoyalipua mapinduzi.

Fikra hizi hazikutofautiana na za Said Ahmed katika Asali Chungu. Katika pembe zote mbili za maisha yake kama mtawala na mwinyi, Zuberi anakinzana na watu wa tabaka la chini. Akiwa mkuu wa wilaya, Zuberi hana nafasi ya kuonana na wateja bali anapoteza wakati wake afisini akifanya mapenzi na wasichana. Katika maisha yake ya umwinyi, Zuberi anautumia 'utukufu' wake kuwanyanyasa wengine. Wanyama wake wanakula muhogo na migomba ya majirani, wafanyakazi wake wanachoma mikarafuu ya jirani na anatumia hiana kuwapata wasichana wabichi kama Semeni na Mboga.

Aidha, anadai thuluthi mbili ya mazao kutoka kwa wale waliokodi vikataa shambani mwake. Al'muradi maisha ya Zuberi, ambaye anawakilisha tabaka la mamwinyi lililokuwa vile vile likiongoza, yanakinzana moja kwa moja na ya watu wa tabaka la chini.

Said Ahmed ameeleza mkinzano huu kwa maneno yanayoteka hisia za wasomaji asemapo:

> Mtu huzaliwa katika nchi yake ambayo angalihisi ni mama mzalia, na kutaraji kwamba yeye alikuwa mwananchi wa kustahili haki sawa na wengine. Leo anatafuta angalau pahala pa kuchomeka ubeu wa muhogo hapapati; ati kwa sababu ni pa Bwana Fulani. Mtu kwao hana haki ya kupanda na kuvuna, na bado anashikilia 'hapa kwetu, hapa kwetu....' Uzito mkubwa ulikuwa umewaelemea watu kama mzee Omari; uzito ambao ulionekana kutokuwa na mwisho (uk. 23)

Uzito huu ulitokana na tofauti kubwa ya kiuchumi baina ya kundi dogo na umma kwa jumla.

Uzito huu ndio unaowafanya wahusika kama Biti Daudi wawasaidie mamwinyi katika njama zao kusudi wajifaidi. Biti Daudi anawasaidia Zuberi na Amina

wapate vijana kama vile Makame anavyowasaidia Hamoud na Fauz katika Dunia Mti Mkavu. Wahusika hawa ni maskini lakini wanajinasibisha na mamwinyi kusudi wajifaidi.

Maisha ya umaskini ndiyo yanayomwelekeza Pili, mke wa Shaabani Supu, afanye uasherati na matajiri. Ingawa katika hulka ya Pili huenda kuna udhaifu wa kibinafsi, nafasi ya shida za kiuchumi haiwezi kupuuzwa. Pili anafanya mapenzi na Bwana wa Bopa, Mwarabu tajiri wa Machungwani. Vile vile anafanya mapenzi na Mapute na Bori.

Tabia ya Pili inamfanya Shaabani Supu ahisi kwamba wanawake ni watu wasioaminika na wasioweza kuwa na mapenzi ya dhati bali huongozwa na uhitaji na mtaji. Lakini katika Dunia Mti Mkavu, na Utubora Mkulima tunakumbana na wahusika kama Masika na Radhia wanaoongozwa na mapenzi ya dhati na kupuuza utajiri. Masika anamfuata Fumu na Radhia anamchagua Utubora badala ya Makuu. Kwa hivyo, kauli ya Shaabani Supu kwamba unyonge ndio usababishao maonevu (uk 41) ina mashiko zaidi kuliko ile ya kijumla kwamba wanawake wote ni wabaya.

Mivutano ya kimapenzi baina ya matajiri na maskini yapasa ichukuliwe kama sehemu ya mivutano ya kiuchumi kwa kadri inavyohusu matabaka yaliyotofautiana.

Hata mvutano wa Amina na Baya kwa ajili ya Dude ni sehemu ya mvutano wa kitabaka. Amina anamparamia Dude kwa sababu yeye ana fedha nyingi na angetaka astareheshwe. Dude anamfuata kwa sababu anapata raha na starehe; kwa sababu anainuliwa kitabaka; anapewa nguo mpya, gari jipya la Vauxhall na jina jipya la Karim. Anapewa nafsi mpya.

Uhusiano wa Dude na Baya umejikita katika dhati ya mapenzi. Mwandishi anatwambia:

> Dhati ya mapenzi ilimweza; mapenzi
> ya udugu na mazowea yakamchachafya
> Haikuwa hawaa; haikuwa ubataani
> bali mapenzi - mapenzi halisi
> yasiyoweza kufutika japo
> yakielemewa na ukiwa wa miaka (uk 147 )

Kwa hivyo, katika mvutano baina ya Baya na Amina, Dude anajiunga na Baya ambaye wana asili moja ya kitabaka. Dude anapoizungumzia picha ya Amina baada ya utengano, anajitahidi kujitanzua kisaikolojia kutokana na sumaku ya mapenzi ya Amina yaliyojikita katika hawaa na mtaji. Hii ni jitihada ya Dude ya kumiliki mazingira yake kuliko kuyaacha mazingira yamwendeshe. Kwa namna hii anajaribu kuurejelea utu aliokuwa ameuweka pembeni. Hili ndilo linalomfanya Dude akatae kununuliwa kwa shilingi elfu kumi kusudi

amwache Shemsa. Dude anamwambia Amina:

> Pesa hizo nd'o zinunuwe mapenzi
> yetu mimi na Shemsa? Pesa hizi
> zivunje ahadi na ukweli wetu?
> Au pengine ziwe mashaka ya mmoja
> wetu, pengine mimi, au wewe au
> Shemsa au Bwana Zuberi? Mimi sina
> haja na ..... (uk. 181)

Ingawa wakati mwingine Dude anafanya matendo ambayo ni kinyume na matakwa ya utu, kama kufanya mapenzi na Latifa, kuna nyakati nyingine anakumbwa na hisia za kiutu. Kama mwandishi asemavyo (uk. 192-193) kupotoka kwake kwaweza kupatikana katika msingi wa asili yake, malezi yake na athari ya mazingira.

Hii ni baadhi tu ya mikinzano baina ya matabaka inayopatikana katika riwaya za visiwani, Zanzibar. Mikinzano hii husaidia katika ubingirishaji wa gurudumu la mapinduzi hasa endapo wahusika wamepevuka kiurazini. Urazini wa kitabaka ni hali muhimu sana katika kuyatayarisha na kuyaelekeza mapinduzi. Hali hii haina budi kuchunguzwa katika riwaya tunazozihakiki.

## 3.4. URAZINI WA KITABAKA

class consciousness.

Lukacs (1971:73) amesema kwamba urazini wa kitabaka ni hisia, ni ufahamu wa dhima ya kihistoria.

ya tabaka. Yaani watu wa tabaka moja kuweza kufanya juhudi za pamoja ili waweze kujihami dhidi ya nguvu za tabaka jingine. Mills[12] ametoa mifano ya hali zinazohitajika katika urazini wa kitabaka. Kwanza, watu wafahamu mantiki ya tabaka lao na wajinasibishe na matakwa ya tabaka hilo. Pili, wafahamu na wayachukulie mahitaji ya tabaka lingine kama kwamba si halali. Tatu, wafahamu na wawe tayari kuchukua hatua ya pamoja ya kisiasa ili kufikia lengo la kisiasa la kijumla na lenye manufaa kwao.

Kitu cha muhimu katika urazini wa kitabaka ni kwamba watu wa tabaka moja hushirikiana dhidi ya tabaka jingine kwa sababu maslahi yao ni mamoja. Lengo la tabaka lenye urazini ni kujiimarisha na kujihifadhi dhidi ya tabaka linalokinzana nalo.

Kabla ya tabaka kupata urazini, watu wa tabaka hilo huvutana wenyewe kwa wenyewe hasa kwa ajili ya mashindano au ukosefu wa ufahamu kamili wa adui wao.[13] Wanachukulia, kwa mfano, kuwa hali yao imesababishwa na baadhi ya watu wa tabaka lao. Kwa hivyo, wanaibiana na wanauana. Aidha, wanatafuta suluhu za kibinafsi. Urazini uingiapo ndipo mivutano katika tabaka moja inapoelekezwa dhidi ya tabaka linalokinzana nalo.

Urazini wa kitabaka hautokei kwa sadfa tu bali unatokana na mikinzano mikali ya kitabaka, taathira

za kutoka nje, na jitihada za waasisi wanaoelewa mfumo wa uzalishaji mali, mikinzano yake na njia zinazoweza kutumiwa ili ukombozi ufaulu. Urazini wa kitabaka ni kipengee muhimu sana katika mabadiliko ya kijamii na katika ufanikishaji wa mapinduzi. Kabla mapinduzi ya kijamii hayajatokea inatarajiwa kwamba matabaka yanayohusika yatadhihirisha urazini wa kisiasa na hapo ndipo nguvu za kila tabaka zitashikamana. Tendo la mapinduzi ya kijamii, basi, litakuwa kilele cha mikinzano ya kitabaka iliyoelekezwa kiurazini.

Katika Dunia Mti Mkavu wahusika waliopewa dhima ya kuwaamsha wenzao kiurazini ni kama vile mzee Gae na Kumba. Mzee Gae anawahimiza mafalahi wenzake wazidadisi nafsi zao ili wamaizi kitovu cha idhilali iliyowakusa. Anawashauri wajiulize maswali ya kimsingi kuhusu maisha yao na uhusiano wao na mamwinyi. Urazini wa mzee Gae unatokana hasa na mikinzano yake ya mara kwa mara na utawala, safari zake za nchi za nje, na vita vya mpakani.

Licha ya maswali anayowauliza mafalahi wenzake, mzee Gae anadhihirisha urazini wa kitabaka pale anapomzuia Fumu baada ya Fauz na Makame kuchoma mimea ya Fumu. Fumu anafikwa ukingoni na dhuluma za Fauz. Kwa hivyo, anachukua mndu na kumkabili Fauz.

Mwandishi anatwambia:

> Nani asiyejua kwamba mbele ya bunduki mndu hausimami? Lakini huu ulikuwa wakati ambao kwamba maovu yalifika ukingoni na unyonge ukamshajiisha mwanadamu ayasukume maovu yaporomoke na kutokomea moja kwa moja - ingawaje yanatisha. Kama kuishi kuchungu, kifo huwa ni kitamu (uk. 95)

Lakini hili ni suluhisho la kibinafsi lisiloweza kulifikisha popote tabaka la Fumu.

Mzee Gae anamkumbusha dhima yake usiku huo watakapokutana na wafanyakazi wa mjini. Hii ni kumtanabahisha kuhusu umuhimu wa suluhisho la kudumu. Yaani mateso ya kibinafsi yanapasa yamshajiishe mtu katika kutafuta suluhisho lenye kina na maki.

Jazanda ya chura na nyoka inayotolewa na Mzee Gae mahakamani ni ithibati nyingine kwamba huyu mzee amepevuka kiurazini. Jazanda hii ni ishara kwamba ingawa tabaka linalonyanyaswa huenda likakoseshwa uwezo, wakati mwingine linaweza kutumia maarifa kulibaka na kuliangamiza tabaka-nyonyaji. Mzee Gae anamtahadharisha hakimu:

> ... nyoka anapozibwa pumzi na chura hachukui dakika nyingi, atanyooka mkavu.

> Na hii huthibitisha kwamba ijapokuwa kila siku nyoka humwinda chura iko siku japo moja, chura humwinda nyoka kwa ajili ya kujihami... chura humwua nyoka bwana, usikatae... usikatae.. (uk. 114)

Jazanda hii inawapa matumaini mafalahi na wafanyakazi kwamba japo jitihada za kujikomboa zinazofanywa katika Dunia Mti Mkavu na Kuli hazifaulu, pana matumaini makubwa kwamba zitafaulu hapo baadaye. Jazanda hii inatiliwa nguvu na mvua inayoteremsha mikondo ya damu ya akina Fumu, Pandu, Bakari, Kumba na Masika.

Ama kwa hakika, hatua yoyote inayotetemesha nguvu za kitawala ni hatua ya kimaendeleo. Baada ya mauaji ya In the Fog of the Seasons End kuna mvua inayochanganyikana na damu ya wale waliojitoa mhanga. Said Ahmed na Alex la Guma wanawahimiza wanyonge wasikate tamaa kwa sababu damu iliyomwaika katika mivutano ya kitabaka haikupotea bure bali itaipa uhai na upevu miche ya kimapinduzi. Kwa hivyo, yapasa migomo katika riwaya hizi ichukuliwe kama hatua ya kimaendeleo. Fikra hizi zinakubaliaka hasa kwa mujibu wa uyakinifu wa kijamii ambapo 'kushindwa' na 'kushinda' huchukuliwa kama hali zilizofungamana.

Wakati mzee Gae akiwaamsha mafalahi, Kumba anawaamsha wafanyakazi na watamba-na-njia. Kama vile mzee Gae anavyomzuia Fumu asimkabili Fauz kwa mndu, Kumba anamzuia Bakari asipigane na Mbwana. Vita vya kibinafsi vinapigwa kumbo na kuonyeshwa kwamba havina manufaa kwa umma.

Katika riwaya hii, kama vile katika Kasri ya Mwinyi Fuad na Kuli, uongozi wa juhudi za ukombozi unapewa wafanyakazi wa mijini ambao 'wametayarishwa' na mfumo wa kibepari kutekeleza jukumu hilo ( Lenin 1975:255; Marx katika Turok 1980:37).

Said Ahmed ameonyesha uwezekano wa watamba-na-njia, wanaowakilishwa na Pandu katika Dunia Mti Mkavu kupevuka upesi kiurazini na kushiriki katika mapinduzi. Jambo hili linatiliwa shaka na Mazrui (1984:202-204). Tajiriba ya harakati za mapinduzi inatuonyesha kwamba tabaka hili kwa kawaida'hujikuta' katika mkondo wa kimapinduzi na ni nadra sana kwao kushiriki moja kwa moja katika harakati za ukombozi. Ni tabaka lisilokuwa na msimamo madhubuti na aghalabu 'hujikuta' katika mkondo wa harakati wasisozijua mwanzo wala mwisho wake (Turok 1980:378; Cabral 1969: 51; Woddis 1972 (b): 79-84). Cabral (1969:51) amesema kwamba tabaka hili mara nyingi 'hununuliwa' kwa wepesi ili kupinga juhudi za mapinduzi.

Mhusika Pandu anaweza kuchukuliwa kama 'mhusika binafsi' au mhusika anayewakilisha tabaka fulani la kijamii. Kama 'mhusika binafsi' twaweza kukubali uwezekano wa yeye kujiunga na harakati za ukombozi kwa wepesi lakini kama mhusika mwakilishi' inatuwia vigumu kuikubali nafasi aliyopewa. Anapevuka kiurahisi mno. Aidha, hatuna ithibati yoyote ya kihistoria tuijuayo inayolipa tabaka la watamba-na-njia nafasi muhimu katika mapinduzi ya visiwani. Tunakubaliana na Woddis (1972(b):62) kwamba ingawa 'watu binafsi' miongoni mwa watamba-na-njia wanaweza kushiriki kidhati katika kuyafanikisha mapinduzi, aghalabu tabaka hili haliwezi kushirikiana kwa pamoja na kwa dhati na matabaka hayo mengine tena kwa urahisi kama afanyavyo Pandu.

Ushirikiano wa watamba-na-njia, wafanyakazi, na mafalahi katika riwaya hii unaweza kunasibishwa na ushirikiano wa Farouk Hilal na Subhash dhidi ya Mwanaali. Farouk Hilal na Subhash wanaziunganisha nguvu zao kusudi kumkabili Mwanaali. Hii ni kwa sababu kitabaka wana maslahi sawa yasiyooana na ya Mwanaali.

Kinachouleta ushirikiano huu ni urazini wa kitabaka. Shomari anatupigia muhtasari wa yale yawezayo kutokea nje ya urazini. Anasema:

> Unapoonewa na mtu usiyemuweza, ukipata mnyonge wa Mungu, utataka kumtupia unyonge wako wote; na kumbe kama utaweza utampa sehemu moja tu ya madhila yako (uk. 44)

Vita vya Bi. Mtumwa na mumewe Mashaka ni mfano wa jambo hili. Wote wameonewa na mfumo wa uzalishaji mali Bi. Mtumwa anauza pombe naye mumewe anamwibia viakiba vyake kusudi aende kulewa ajisetiri na uhalisi wa maisha. Bi. Mtumwa akigundua wizi huo anampiga mumewe. Bi. Mtumwa anazimwaya dhiki zake zilizotokana na hali ya maisha kwa mumewe huku akichukulia kwamba umaskini wake unasababishwa na 'ukupe' wa mumewe.

Bi. Staghafiru anamwokoa Pandu aliyekuwa akipigwa na watu kwa ajili ya wizi. Watu wanaompiga Pandu wanafikiri kwamba ndiye anayesababisha unyonge wao. Wanasahau kwamba mfumo wa uzalishaji mali uliomzaa Pandu ndio huo huo unaowafanya wawe wanyonge kiuchumi. Kumwua Pandu au Siwa hakuwezi kuyabadilisha maisha kwa jumla. Hawa ni wezi maskini ambao aghalabu wanabainisha chembechembe cha utu. Said Ahmed anasisitiza kwamba kipengee hicho chenye utu yapasa kikuzwe na kipanuliwe ili nao washiriki katika kuyabadilisha maisha ya jamii.

Uhasama katika tabaka - nyonyaji unaweza kuonekana katika uhusiano wa Bw. Suleiman na Mhindi-sonara Lalji. Wote hawa ni 'mapwagu' lakini wanakinzana kwa ajili ya mashindano baina yao.

Katika muktadha wa Kihistoria, uhasama katika tabaka moja unaweza kubainika wakati wa tatizo la uwiwaji. Tatizo hili liliwafanya Waarabu na Wahindi wakinzane japo kimsingi walikuwa wa tabaka moja. Mashamba ya Waarabu yalitwaliwa na Wahindi, Waarabu waliposhindwa kulipa mikopo (Mrina na Mattoke 19 0: 40; Lofchie 1965: 100-108; Jabir 1977: 39-45).

Riwaya ya Dunia Mti Mkavu, kwa hivyo, imetuonyesha kwamba mikinzano ya kitabaka ina chimbuko lake katika mfumo wa uzalishaji mali. Aidha, imeonyesha umuhimu wa urazini wa kitabaka na maandalizi mazuri katika kuyafanikisha mapinduzi.

Kielelezo cha urazini wa kitabaka katika Kuli ni Bakari. Mhusika huyu anaweza kuwekwa sambamba na Bakayoko wa God's Bits of Wood, Kumba wa Dunia Mti Mkavu, Tekwane wa In the Fog of the Season's End na Gicaamba wa Nitaolewa Nikipenda. Wahusika hawa wanazipa nafsi kazi hizi kwa sababu wote wana urazini wa kitabaka. Wanajua wasimame wapi na wafanye nini ili wakabiliane na adui.

Bakari anashirikiana na Faraji katika kuwaelimisha wafanyakazi na kuandaa mgomo kama vile

Bakayoko anavyoshirikiana na Lahbib. Mipango inafanywa ili wafanyakazi wajue kusoma na kuandika. Urazini wao unaamshwa kwa makaratasi yanayoelezea hali zao na dhiki zao. Wakati wa mgomo, chama cha wafanyakazi bandarini kinashirikiana na wafanyakazi wa Tanganyika kuzisaidia aila zilizoelemewa sana. Ushirikiano wa wafanyakazi nje ya mipaka ya taifa ni kielelezo cha umoja wa maslahi ya wafanyakazi wote ulimwenguni. Shafi anaonekana kusisitiza nafasi ya umoja huo ili kuyaleta mabadiliko yenye maana katika mataifa yenye dhuluma. Lakini umoja huu utawezekana kupitia kwa vyama vyenye viongozi kama Bakari ambao wamepevuka kiurazini bali si kutokana na viongozi kama mzee Tindo wanaozifikiria nafsi zao tu. Mzee Tindo ni mfano wa viongozi wasiopevuka kiurazini na wanaojipendekeza kusudi wapate makombo kutoka kwa waajiri wao. Ingawa wanajua kwamba wananyonywa, hawawezi kuchukua hatua madhubuti kujikomboa kwa sababu wanajiona afueni kuliko wenzao.

Katika riwaya ya Kuli, Shafi anasema kwamba mfanyakazi mwenye urazini wa kitabaka hujikuta wakati mwingine akikinzana na aila yake kwa sababu aila hiyo inaona kama kwamba inapuuzwa. Shafi anaonekana kushauri kwamba panapotokea mvutano baina ya masuala ya kibinafsi na ya umma, basi yale ya kibinafsi yafaa

yapuuzwe. Ndoa ya Amina na Rashidi inatokea wakati Rashid amepevuka kiurazini na yuko mbioni kushirikiana na wafanyakazi wenzake katika kukabiliana na mfumo wa kibepari. Hii inamlazimu ahudhurie mikutano ya usiku mara kwa mara. Amina anachukizwa na jambo hili kwa sababu anachukulia kwamba anapuuzwa. Hata hivyo, anapevuka baadaye na kuuona ukweli. Hili linatupa matumaini kwamba ijapokuwa Rashidi amefungwa, amemwacha mkewe akiwa na mwamko na matumaini kuwa madhila hayo yataisha.

Nafasi ya urazini wa kitabaka katika kufanikisha mapinduzi umegusiwa tena katika Kasri ya Mwinyi Fuad. Baada ya vifo vya Bwana Malik na Bi. Maimuna, Fuad analelewa na Bwana Zein. Tunaambiwa hivi:

> Kwa muda wa miaka kumi aliishi chini ya maongozi ya Bwana Zein aliyemfundisha mbinu zote za kulinda utajiri na utukufu wake na katika kipindi hicho alifanya majaribu mazuri ya kutuma watwana na mafukara walio chini ya amri yake (uk.15)

Kwa hivyo anafunzwa kunga za kulihami tabaka lake kama vile Kumba na Bakari wanavyowafunza wafanyakazi njia za kujilinda.

Baadaye, Fuad anaposhangazwa na mwamko wa kisiasa miongoni mwa wafanyakazi wake anamwendea Bwana

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

Marjebi kusudi ahakikishiwe kwamba tabaka lao liko imara. Ushirikiano wa Fuad, Zein na Marjebi katika kulikosesha matumaini tabaka la wafanyakazi na mafalahi ni ithibati kwamba ni watu wenye urazini wa kitabaka. Wanaharamisha jitihada na matumaini ya tabaka la chini. Dhana yao ni kwamba wafanyakazi 'wamejaaliwa' kuwatumikia mamwinyi na mabepari. Marjebi anamhakikishia Fuad hivi:

> Wa moja havai mbili. Wao washajaaliwa kuwa nyuma maisha yao.... uchaguzi tutawashinda; uhuru tutautia mkononi tarehe tisa desemba; usitie wasiwasi wowote - chama cha Rait el Sultani kiko imara hapana khof. (uk. 56)

Tabaka hili linajiimarisha kwa kusaidiana, kuhakikishiana na kuelekezana. Linaeneza fikra na imani zake ili kujipa matumaini ya kuendelea kufaidi kutokana na nguvu za wengine.

Imesemekana kwamba dhana za tabaka tawala ndizo zinazotawala.[14] Kwa hivyo ili tabaka linalodhulumiwa lijikomboe, halina budi kujitakasa kutokana na imani hizo. Katika Kasri ya Mwinyi Fuad, mikutano ya kijangwani inayoandaliwa na Marjani inasaidia katika kuwatanabahisha wafanyakazi na mafalahi kwamba hali yao haikutokana na majaaliwa kama walivyozoea

kufunzwa. Mikutano hii inasaidia kuwaamsha kisiasa ili waone matumaini ya kujikomboa.

Watu binafsi vile vile wanajaribu kuwaamsha wenzao kiurazini. Kwa mfano, Mkongwe anajaribu kumfunza Kijakazi kuwa hali yake haitokani na kudura ya Mungu. Hata hivyo, inamchukua Kijakazi muda mrefu kutanabahi kuwa hali yake ya maisha inaweza kubadilika. Hata baada ya mapinduzi wakati ambapo Fuad hana uwezo tena, Kijakazi angali anamsujudia. Ugumu wa Kijakazi kuamka kiurazini unatokana na kukolea akilini mwake kwa mafunzo na dhana za utukufu wa mamwinyi. Dhana hizi zimempofusha hata haoni mazingira yake yakibadilika.

Kwa hivyo, Dunia Mti Mkavu, Kuli na Kasri ya Mwinyi Fuad zimeupa urazini wa kitabaka nafasi kubwa katika ufanikishaji wa mapinduzi. Nyota ya Rehema, Asali Chungu na Kiu hazikusisitiza nafasi ya urazini katika mapinduzi. Katika Nyota ya Rehema na Asali Chungu, mikinzano na mikutano ya kisadfa ndiyo iliyopewa nafasi kubwa. Hatuoni jitihada za pamoja za wahusika kujaribu kuleta mabadiliko ya kiuchumi. Aidha, katika riwaya hizi hatuna kundi la waasisi ambao wanawaongoza wenzao kifikra waweze kuubadilisha mfumo. Hata hivyo, waandishi wanaonyesha mapinduzi kama njia ya pekee ya kuleta mabadiliko ya kijamii

na ya kudumu ingawa mapinduzi hayo hayakupewa msingi mzuri bali yamechopekwa ghafla.

Ingawa katika Asali Chungu tunaambiwa hisia za kiutu zilimpata Dude mara kwa mara, hisia hizi hazichujwi kama za Pandu katika Dunia Mti Mkavu. Japo Dude angekuwa mwepesi kupevuka kinadharia kuliko pandu hisia zake hazipewi mwelekeo wa kisiasa. Hata Shaabani Supu ambaye yuko mstari wa mbele kuyafanikisha mapinduzi hatushawishi hasa kuhusiana na kushirikiana na wanawake katika jitihada ya kujikomboa.

Katika riwaya ya Kiu wahusika hawaonyeshi matumaini ya kuweza kuzibadilisha hali zao. Mhusika ambaye angeamka kiurazini ni Bahati lakini amepumbazwa na mapenzi ya Idi. Hata baada ya talaka ya Idi ambayo ingempa fursa ya kujiopoa kutokana na ghilba za maisha, Bahati hazindukani. Anamfuata Idi azimue kiu yake nyingine. Kiu ya mali. Hatimaye, riwaya ya Kiu inaishia katika kutuonyesha kiu zipatikanazo katika mfumo wa kimwinyi. Mwandishi haonyeshi njia zinazoweza kutumiwa kuzizimua kiu hizo kwa sababu anaamini zimeumbwa pamoja na binadamu na zitaendelea kuwepo daima dawamu.

## 3.5. TAASISI ZA KITAWALA

Taasisi za kitawala kama dini, polisi na mahakama zinatumiwa ili kuzima juhudi za wanyonge kutetea maslahi yao. Hili si jambo geni hata kidogo kwa sababu tawala aghalabu hujinasibisha na tabaka lenye nguvu za kiuchumi. Visiwani Zanzibar, utawala wa Kiingereza ulishirikiana moja kwa moja na Waarabu pamoja na mabepari wenye viwanda. Askari wa utawala wa Kiingereza wakatumiwa kuzima migomo na maandamano.

Katika Kasri ya Mwinyi Fuad (uk. 18) tunaambiwa:

> Kila wafanyakazi walipochukua hatua za kudai haki zao walitwa maaskari wa kikoloni ambao walitumia silaha zao za virungu, mavungu ya kuumiza machozi na bunduki kuwatawanya. Baadhi ya viongozi wao na wafanyakazi jasiri walitiwa vifungoni ambako waliteswa na kufanyiwa ukatili wa kila aina.

Wafanyakazi wanapokutana baada ya kifo cha Manafi katika Kuli, askari wa kikoloni wanatumiwa ili kuwatawanyatawanya. Lengo la Inspekta wa kizungu ni kuchukua mkoba wa Bakari ili afichue siri za wafanyakazi na kwa jinsi hiyo aweze kuwamaliza nguvu.

Katika Dunia Mti Mkavu Inspekta Farouk Hilal anatumiwa na utawala wa Kiingereza kuzima mgomo wa mafalahi na wafanyakazi. Farouk anapewa amri kamili:

> Polisi pamoja na CID wanatakiwa wafanye uchunguzi wa kutosha na wawakamate wote wanaoelekea watawashawishi wenziwao kufanya ghasia.... MIMI NAKUPA DHAMANA HII, TUMIA AMRI KALI ILI KAZI YA KUPIGA SINDANO IKIANZA KUSIWE NA TATIZO (uk. 89).

Kwa hivyo, askari wanatumia mabavu kutekeleza maslahi ya mamwinyi na mabepari. Taasisi hii inachukua nafasi maalum katika mikinzano ya kitabaka.

Nafasi hii haitofautiani na ile ya mahakama. Mahakama katika Kuli na Dunia Mti Mkavu inatumiwa kwa manufaa ya wale wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Watetesi wa haki za wanyonge wanafungwa kwa mujibu wa sheria zilizotungwa kulinda maslahi ya mamwinyi na mabepari. Mzee Gae anaiambia mahakama:

> Nyoka tokea lini kumpa chura nafasi ajitetee? Ni udanganyifu tu; sisi tuko hapa, na nyinyi mko huko, tumezeni kama mlivyozoea kumeza, tumezeni, tumezeni, sisi tumo kinywani mwenu. Maneno

> hayatasaidia kitu; hayatasaidia kuzuia uchu wenu. Tumezeni; hamna haja kutuuliza mtumeze vipi. (uk. 113)

Kwa hivyo, Mzee Gae anaona uhusiano wa dhati baina ya mahakama, utawala na wale wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Kupelekwa kwa viongozi wa wanyonge mahakamani ni njia ya kuhalalisha hatua iliyokubaliwa.

Katika Kuli ushahidi wa upande wa mashtaka unapwaya kwa sababu si wa haki. Hata hivyo, Rashidi anafungwa 'miaka mitatu kazi ngumu.' Mahakama inatekeleza jukumu lake katika ulinzi wa mamwinyi na mabepari. Jukumu la mahakama katika Kuli linawiana na la Dunia Mti Mkavu wakati viongozi wa mafalahi na wafanyakazi wanapofungwa. Aidha, kifungo cha Jaku katika Dunia Mti Mkavu baada ya mauaji ya Hamoud ni ishara ya nafasi ya mahakama katika mivutano ya kitabaka. Hata katika Nyota ya Rehema tunaona kwamba Karim anafahamiana na Jaji Mkuu na, kwa hivyo, hasiti kubatilisha sheria kwa sababu ajua ana ulinzi.

Dini hali kadhalika hutumiwa kwa maslahi ya tabaka maalum (Fanon 1967:52). Katika riwaya za visiwani dhana ya majaaliwa inajitokeza mara kwa mara. Kijakazi katika Kasri ya Mwinyi Fuad anaamini kwamba maisha yake ya kitumwa ndiyo majaaliwa yake na kattu

hawezi kujiokoa kutokana nayo. Anamwambia Mkongwe:

> Sikiliza Mkongwe mwanangu, hayo ndiyo majaaliwa yangu. Kuna wengine Bwana Mungu amewajaalia na kuwatukuza mabwana wakubwa na wengine amewajaalia umaskini Lazima ufahamu Mkongwe kama kila mtu na majaaliwa yake. Hivi ndivyo ulivyo ulimwengu (uk. 111)

Hata Fumu katika Dunia Mti Mkavu anayachukulia maisha yake ya kinyonge kama kwamba ndiyo majaaliwa yake - mpaka hapo anapopata urazini wa kisiasa.

Dhana ya majaaliwa imejikita katika dini iliyokuwa imeenea visiwani - dini ya Kiislamu. Dhana hii inawafanya wahusika fulani 'watosheke' na maisha yao kama yalivyo. 'Utoshekaji' huu una manufaa kwa tabaka linalotawala kwa sababu huhalalisha na kuimarisha itikadi za kinyonyaji.

Kwa hivyo katika mikinzano ya kitabaka visiwani, taasisi mbalimbali za kitawala zinachukua nafasi maalum. Zinatumiwa aghalabu kuenezea imani za tabaka dogo linalotawala na kuwakatisha tamaa wanyonge kuhusu matumaini yao ya kubadilisha maisha yao.

## 3.6 HITIMISHO

Katika sura hii tumejaribu kuonyesha kwamba kuna uhusiano mkubwa baina ya mikinzano ya kitabaka na mapinduzi. Tumesema kuwa mikinzano hiyo huwa na athari kubwa endapo itaelekezwa na endapo wanachama wa matabaka watakuwa na urazini wa kitabaka. Urazini utalisaidia tabaka kuyatetea maslahi yake na kujiimarisha dhidi ya tabaka linalokinzana nalo. Baadhi ya riwaya za visiwani hazikuzingatia kipengee cha urazini wa kitabaka katika masimulizi ya mikinzano iliyokuwepo visiwani. Hata hivyo, riwaya fulani zimeonyesha umuhimu wa urazini katika jitihada za ukombozi. Urazini huwezesha na huimarisha ushirikiano wa kitabaka ambao ni muhimu katika kujihami kwa tabaka.

## 3.7 TANBIHI

1. Johnson, Chalmers (1968) Revolutionary Change University of London Press uk. 166

2. Hatua fulani zikichukuliwa kuzuia mikinzano huenda zikashindwa na zikasukuma mbele uwezekano wa mapinduzi.

3. Turok, B. (1980) Revolutionary Thought in the 20th Century. Zed Press London. uk. 4

4. Mkabala huu unachukulia mapinduzi kama kilele cha mikinzano ya kitabaka Tazama, kwa mfano, 'The Communist Manifesto' katika Turok, B. (1980) uk. 30-53.

5. Mikinzano mara huibuka ikadhihiri na mara huzama ikajisetiri. Mara hubadili kasi.

6. Tazama Anderson, H.A. (1974) The Political Economy of Social Class. Prentice Hall. New Jersey uk. 49

7. Woddis, J. (1972(b) New Theories of Revolution International Publishers. New York. uk. 18

8. Jabir, H.H. (1977) Plantation Economy during the Protectorate Period in Zanzibar (1890-1964). Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu, Dar-es-Salaam. uk. 195-196.

9. Wachungaji wengi waliwategemea mifugo kwa maisha yao. Migogoro iliyotokana na siasa za ng'ombe bila shaka iliwaathiri sana kama idhihirikavyo katika Dunia Mti Mkavu.

10. Hawa ni watu wanaoelewa matatizo ya tabaka lao na huwa katika mstari wa mbele kuyatetea maslahi hayo. Huwa kundi dogo lililoimarika kiitikadi na kinadharia.

11. Tazama makala ya Samora Machel 'Women's Liberation is Essential for the Revolution' katika Turok, B. (1980) kama hapo juu uk. 157-167.

12. Fikra za C. Wright Mills zimejadiliwa na Anderson, C.H. (1974) The Political Economy of Social Class. Prentice Hall. New Jersey. uk. 135-136.

13. Tazama Fanon, F. (1967) The Wretched of the Earth Penguin Books. Middlesex, sura iitwayo 'concerning violence'

14. Tabaka linalotawala huwa lina dhana fulani kuhusu maisha na mazingira kwa jumla. Dhana hizo huenezwa miongoni mwa tabaka linalotawaliwa ili kuliteka kifikra.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

## SURA YA NNE

## 4.0 MAPINDUZI NA BAADAYE

### 4.1 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita tumejaribu kuonyesha kwamba riwaya za visiwani zimeipa mikinzano ya kitabaka nafasi kubwa katika masimulizi yake kuhusu maisha visiwani kabla ya mapinduzi. Mikinzano hii, kama ilivyo mikinzano kwa jumla, iliamsha urazini wa kitabaka miongoni mwa mamwinyi na mabepari na vile vile miongoni mwa wafanyakazi na mafalahi.

Hisia hizi za 'umoja' wa kitabaka zilijibainisha katika siasa za vyama. Katika sura hii tutajadili mambo matatu. Kwanza, tutajadili siasa za vyama, Zanzibar kwa mkabala wa kihistoria. Lengo letu ni kuonyesha kwamba vyama vya kisiasa na vya wafanyakazi vina nafasi muhimu katika maandalizi ya mapinduzi kwa sababu hutumiwa kama jukwaa la kutetea, kufunzia, na kuelekezea sera, nadharia na itikadi ya wafuasi wake.

Pili, tutajadili vile kulipuka kwa mapinduzi kulivyosawiriwa katika riwaya hizi. Tutaonyesha kwamba matumizi ya mabavu yamehalalishwa na waandishi wa visiwani.

Hatimaye tutajadili uimarishaje wa mapinduzi hasa kama unavyojibainisha katika <u>Kasri ya Mwinyi Fuad</u>

na Utengano. Hebu sasa tuchunguze siasa za vyama visiwani.

## 4.2 SIASA ZA VYAMA

Mikinzano ya kitabaka tuliyoijadili katika sura iliyopita ilizusha aina mbili za vyama: vyama vya kisiasa na vyama vya wafanyakazi. Ijapokuwa vyama vya wafanyakazi vilikuwa na lengo la kutetea masuala ya muda kama dhamana kazini na mishahara, viliunga mkono vyama vya kisiasa katika kudai uhuru kutoka kwa mkoloni. Kwa namna hii vilichangisha katika kulisukuma mbele gurudumu la mapinduzi.[1]

Siasa za vyama vya kisiasa na vya wafanyakazi zilipamba moto mnamo miaka ya 1950 wakati mapambano ya kitabaka yalipokuwa yameshika kasi. Chama cha kisiasa cha Waarabu kilijulikana kama 'Hizbu el Watan li raiyati Sultani' yaani chama cha raia wa Sultani. Hiki ndicho chama kinachotajwa na Marjebi katika Kasri ya Mwinyi Fuad anapomwambia Fuad:

> Uhuru tutautia mikononi desemba tisa.... chama cha rait el Sultani kiko imara hapana khof. (uk. 56)

Lakini kwa vile jina la chama hiki lilionyesha ubaguzi mno lilibadilishwa na kuwa 'Zanzibar National Party' (ZNP). Msimamo wa ZNP chini ya Ali Muhsin ulikuwa

kwamba Uingereza itoe Uhuru kwa Waarabu kwa sababu hadhi na heshima ya Sultani vilikuwa vimedhalilishwa na utawala wa Kiingereza.

Kwa upande mwingine, Waafrika walikuwa wameanzisha chama kitakacholinda maslahi yao. Serikali mwanzoni ikakataa kukiandikisha chama hiki kwa sababu muungano wa Waafrika ungekuwa kitovu cha hofu kwa wakoloni na vibaraka wake. Serikali ikatumia sera ya Lord Lugard ya 'Kugawa na kutawala'[2] ili kuvunja umoja huo. Wakasema chama cha Waafrika ni cha Wakristo na kingehatarisha maslahi ya Waislamu. Isitoshe, waliwagawanya Waafrika katika matapo mawili: tapo moja likiwa Waafrika wa Bara, na tapo la pili likawa la Waafrika wenye asili ya visiwani (Mrina na Mattoke 1980:49). Waafrika wenye asili ya visiwani na ambao wengi wao walikuwa Waislamu wakajinasibisha na Chama cha Washirazi. Hata hivyo, utengano ulioanzishwa na kuchochewa na utawala wa kikoloni haukudumu. Mnamo 5/2/1957 Chama cha Waafrika cha Zanzibar kiliungana na Chama cha Washirazi. Muungano huu ukaibusha chama cha Afro-Shirazi (ASP) ambacho kingeweza kukabiliana na ZNP katika uchaguzi.

Baada ya uchaguzi wa 1957, ilibainika kwamba Chama cha ASP kilikuwa na nguvu sana kilinganishwapo

na ZNP. Watawala wakajaribu kukigawanya. Mnamo Desemba, 1959 wakulima matajiri wa Pemba na baadhi ya maulama waliokuwa wafuasi wa chama cha Shirazi, walikata alaka na ASP na wakaanzisha chama cha 'Zanzibar and Pemba Peoples' Party' (ZPPP). Chama hiki baadaye kilijidhihirisha kwamba kinawakilisha maslahi ya wenyeji wa visiwani wenye mashamba makubwa. ZPPP kilishirikiana na ZNP kwa sababu maslahi yao yalikuwa sawa. Jambo hili linatilia mkazo kauli yetu kwamba mapinduzi ya 1984 yalikuwa na misingi ya kitabaka kwa sababu vyama vilivyokuwa na maslahi sawa vilitiliana nguvu. Yaliyotokea nyakati za uchaguzi yanatubainishia jambo hili vema.

Uchaguzi wa Januari, 1961 ulikuwa na matokeo yafuatayo:

| CHAMA: | ASP | ZNP | ZPPP |
|---|---|---|---|
| KURA: | 36,698 | 32,724 | 15,541 |
| VITI: | 10 | 9 | 3 |

Kama inavyoonekana kutokana na tarakimu hizi ASP kilishinda. Kulingana na mapendekezo ya Sir Hilary Blood (1960) chama hiki kilipaswa kuunda serikali. Lakini,wajumbe wawili wa ZPPP walikipa ZNP viti vyao na mmoja akajiunga na ASP; ASP na ZNP zikawa sare. Kwa hivyo, hakuna chama ambacho kingeunda serikali kama alivyopendekeza Hilary Blood.

Mnamo Juni 1, 1961 serikali iliongeza majimbo ya uchaguzi hadi ishirini na matatu badala ya ishirini na mawili ili kusitokee vyama viwili vyenye nguvu sawa. Ingawa ZPPP kilikuwa kimejiunga na ZNP baada ya uchaguzi wa Januari, kilijitenga kwa minajili ya uchaguzi wa Juni. Matokeo ya uchaguzi huo yalikuwa kama ifuatavyo:

| Chama: | Zanzibar: | Pemba: | Jumla: |
|---|---|---|---|
| ASP | 8 | 2 | 10 |
| ZNP | 5 | 5 | 10 |
| ZPPP | 0 | 3 | 3 |
| Jumla | 13 | 10 | 23 |

(Mrina na Mattoke 1980:77; Ayany 1970:86)

Baada ya uchaguzi ikaonekana kwamba chama cha ASP kilikuwa kimeshinda lakini ili kuzuia serikali isitwaliwe na chama kilichowakilisha maslahi ya wanyonge, ZPPP kilijiunga tena na ZNP. ASP ikiwa na viti kumi na ZNP viti kumi na vitatu. Serikali ya mseto ikawa si serikali ya walio wengi.

Vyama vya wafanyakazi vilikuwa navyo vikishamiri. Nguvu za kisiasa za vyama hivi zilibainika hasa baada ya vyama hivi kuungana na kuunda shirikisho la vyama

vya Wafanyakazi (Federation of Trade Unions - FPTU) na muungano la vyama vya Wafanyakazi wa Pemba na Unguja (Zanzibar and Pemba Federation of Labour - ZPFL). Aidha, ni wakati huu ambapo Abdulrahman Babu alijiondoa kutoka kwa ZNP. Babu alikuwa kiongozi wa kikundi kilichokuwa na fikra na mtazamo wa kimapinduzi ndani ya ZNP. Kikundi hiki kilipinga umwinyi na ubaguzi wa rangi na kikapendekeza serikali iliyofuata mfumo wa kijamaa badala ya ile iliyojikita katika uislamu (Lofchie 1965:258). Baadaye, Babu aliunda chama cha UMMA. Chama hiki kilifuata itikadi ya ujamaa kisayansi.

Kujitoa kwa Babu kulidhoofisha chama cha ZNP. Shirikisho la vyama vya wafanyakazi (FPTU) likaanza kukiunga chama cha UMMA mkono. Ng'ambo ya pili, muungano wa vyama vya wafanyakazi wa Pemba na Unguja (ZPFL) liliunga mkono chama cha Afro-Shirazi. Babu vile vile aliunda Umoja wa Waandishi wa Habari ('All Zanzibar Journalists' Organisation - AZJO). ZNP kilianzisha chama cha Umoja wa Vyama vya Wafanyakazi ('Zanzibar Trade Union Congress' - ZTUC) ili kukinzana na vyama hivyo vingine.

Kwa hivyo, kabla ya mlipuko wa mapinduzi, vyama vya kisiasa na vya wafanyakazi vilikuwa vinawaandaa kidogo wananchi kiitikadi na kinadharia. Kwa sababu

mkabala wa UMMA ulikuwa umeegemea mno katika 'mrengo wa kushoto' utawala wa kikoloni ulikipiga marufuku na, kwa hivyo, hakikushiriki katika uchaguzi wa Julai, 1963. Matokeo ya uchaguzi huo yalikuwa kama ifuatavyo:

| CHAMA | KURA | | | VITI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ZANZIBAR | PEMBA | JUMLA | ZANZIBAR | PEMBA | JUMLA |
| ASP | 53,232 | 33,853 | 87,085 | 11 | 2 | 13 |
| ZNP | 26,572 | 21,378 | 45,950 | 6 | 6 | 12 |
| ZPPP | 4,572 | 21,037 | 25,609 | 0 | 6 | 6 |

(Mrina na Mattoke 1980:87; Ayany 1970:112)

Ingawa ASP ndicho chama kilichoibuka na ushindi hakingeweza kuunda serikali kwa sababu, kwa mara nyingine tena, ZPPP kilijiunga na ZNP na kwa hivyo kukipa ZNP viti kumi na vinane. Muungano huu ukaunda serikali. Mohamed Shamte akatangaza serikali mnamo Julai 17, 1963. 'Uhuru' ulipotangazwa mnamo Desemba 10, 1963 bendera hazikupeperushwa katika sehemu nyingi za Waafrika. 'Uhuru' huu uliitwa 'Uhuru wa Waarabu'[3]

Waafrika waliona kwamba njia za amani hazingeweza kuwafikisha mbali. Siasa za vyama zilikuwa na mchango, hata hivyo, katika kuleta mabadiliko yaliyoanza kuandaliwa zamani. Tunakubaliana na Abdulrahman Babu

asemapo:

> Mabadiliko ya kijamii kama vile
> mabadiliko ya maumbile ya binadamu
> huja polepole na bila kubainika mpaka
> yanapopevuka na kujibainisha kwa kishindo.[4]

Kishindo hiki, visiwani Zanzibar, kiliharakishwa na utawala wa kiimla wa Mohamed Shamte. Serikali yake ilifanya haraka kujenga upya jeshi la polisi. Ikawaondoa Waingereza na Waafrika waliokuwa na asili ya Bara. Nafasi za polisi, utumishi wa Serikali na matawi mengine muhimu ya utawala yakapewa Waarabu waliokuwa waaminifu kwa Sultani. Mapinduzi yakawa njia ya pekee iliyosalia kwa Waafrika waliotaka kujiokoa na madhila ya miaka mingi.

Hata hivyo, visiwani hakukuwa na Chama cha waasisi ambacho kiliimarika sana kinadharia na kiitikadi na ambacho kingeweza kuyaandaa mapinduzi kisayansi. Chama cha ASP kilikuwa maarufu kwa umma lakini viongozi wake hawakusoma sana wala kuelewa vema nadharia ya mapinduzi ya kijamaa. Chama cha UMMA kilikuwa na nadharia ambayo ingeielekeza Zanzibar katika mfumo wa ujamaa wa kisayansi lakini hakikuwa kimejiimarisha sana miongoni mwa umma. Kilikuwa ni kichanga mno.

Lofchie (1965:274) na Okello (1967) wanasema mapinduzi ya visiwani yaliongozwa na John Okello. Si lengo letu kujadili nafasi ya Okello katika mapinduzi hayo lakini huku tukizingatia ushirika uliokuwepo baina ya ASP na UMMA na tukikumbuka kwamba vyama hivi viliungwa mkono na vyama vya wafanyakazi, yumkinika vyama vya kisiasa na vya wafanyakazi vilikuwa na jukumu kubwa katika maandalizi ya mapinduzi.

Walakini, katika riwaya za visiwani, vyama hivi havikupewa nafasi kubwa katika maandalizi na ulipuaji wa mapinduzi. Huenda hili ndilo linalomfanya Senkoro aseme yafuatayo kuhusu Kasri ya Mwinyi Fuad:

> Nafasi ya jukumu la chama(ASP) katika mapinduzi hayo.... pia hatuioni kiukamilifu kwani mwandishi kaitaja mara moja au mbili tu kama kwamba chama hicho hakikuwa na nafasi kubwa ya uongozi wa hayo mapinduzi.[5]

Vyama vya kisiasa ni muhimu katika harakati za ukombozi kwa sababu huunganisha hisia na fikra za wanachama wake ili kuimarisha sera, nadharia na itikadi yao. Tumeona kwamba vyama vya kisiasa na vya wafanyakazi vilikuwa na nafasi katika siasa za visiwani kabla ya mapinduzi. Waandishi wa visiwani

hawaonekani kulizingatia jambo hili na anayoyasema Senkoro hapo juu yanaweza kusemwa kuhusu Asali Chungu, Kiu na Nyota ya Rehema. Katika Kasri ya Mwinyi Fuad 'tunahisi' kuna 'chama' kinachoandaa hotuba Kijangwani na ukusanyaji wa silaha katika shamba la Dambwe. Juhudi za Marjani, Vuai na Kondo ni za pamoja. Katika Kuli vyama vya wafanyakazi, Zanzibar na vyama vya wafanyakazi, Tanganyika vinashirikiana kugongana na ubepari. Tunamwona Bakari akisafiri katika nchi zote mbili. Tena, aila zinazoelemewa wakati wa mgomo zinasaidiwa. Katika Dunia Mti Mkavu, hisia na fikra za wafanyakazi zinaelekezwa na chama. Vyama hivi vinatekeleza jukumu la vyama vya kisiasa.

Kwa hivyo, katika baadhi ya riwaya za visiwani vyama hivi vinapewa nafasi vinazostahiki. Vinashirikishwa katika maandalizi ya mapinduzi. Hata hivyo, riwaya nyingine hazikuvipa vyama hivi nafasi yoyote.

## 4. 3 KULIPUKA KWA MAPINDUZI:

Mapinduzi ya kijamii yanapofaulu hubadilisha muundo wa kimsingi wa kiuchumi na vile vile wa kitawala. Mapinduzi ya kijamii yanajitenga na migogoro na mabadiliko mengine ya kijamii kwa sababu ya 'Sadfa' mbili:'Sadfa' ya mabadiliko ya muundo wa

jamii ambapo nafasi za matabaka katika jamii zinabadilishwa; na 'sadfa' ya muundo wa siasa na muundo wa jamii (Skocpol 1979:4-5; Woddis 1972 (b): 17).

Mapinduzi ya kisiasa yanabadilisha muundo wa kisiasa lakini hayabadilishi muundo wa kijamii wala si lazima yawe yametokana na mikinzano mikali ya kitabaka. Hali nyingine kama 'Mapinduzi ya Viwanda' zinaweza kubadilisha muundo wa jamii bila kusababisha au kusababishwa na mabadiliko ya muundo wa siasa.

Kwa hivyo, jambo la kimsingi na la kipekee katika mapinduzi ya kijamii ni kwamba yanapofaulu huleta mabadiliko muhimu na ya kudumu katika muundo wa jamii na muundo wa siasa. Aidha, mabadiliko haya huenda sambamba na huongezana nguvu.

Tumeona kwamba, kwa kawaida, utawala ni chombo cha tabaka lenye nguvu za kiuchumi na hutumiwa na tabaka moja katika ukandamizaji wa tabaka jingine. Kwa hivyo, ukombozi wa kweli wenye misingi ya kitabaka hauna budi kuteka taasisi za utawala (Lenin 1975:255). Tena, humo katika dhana ya mapinduzi ya kijamii mna fikra ya kitendo cha tabaka moja lisilomiliki nyenzo za uzalishaji mali, kuchukua madaraka ya kiuchumi na kisiasa kwa nguvu kutoka kwa tabaka tawala.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

Mapinduzi tunayokumbana nayo katika riwaya za visiwani yamelenga katika mambo hayo. Katika riwaya za visiwani, matumizi ya nguvu yanahalalishwa kama njia ya pekee ya kuliondoa tabaka la kimwinyi linaloungwa mkono na mabepari wa Kiingereza. Ugunduzi wa 'uchafu' mwingi ulioenezwa na Zuberi baada ya kumnajisi Semeni katika Asali Chungu unasadifiana na kutekwa kwa serikali kwa mabavu. Amina, Zuberi na Biti Daudi waliokuwa watu wazandiki na wanafiki waliotawaliwa na pupa, wanauawa. Udhalimu wao unaondolewa na nguvu za pamoja za umma ukiongezwa na akina Shaaban Supu. Wananchi wanaenda wakiimba:

> Tunataka haki zetu.... Ardhi mali
> ya taifa.... mabepari leo ndio
> mwisho wao... Tumechoka na unyonge..
> .... Nchi lazima iwe huru (uk. 216).

Itabainika kwamba katika Asali Chungu, mapinduzi hayaonyeshwi yakiandaliwa na kundi la waasisi walioimarika kinadharia[6] wala hakuna nguvu za chama zinazobainika wazi wazi katika kuyaelekeza.

Katika Nyota ya Rehema tunaambiwa kwamba kesi ya Sulubu kumwua Karim ndiyo iliyotia vuguvugu nchini na kulipua mwamko wa kisiasa. Vizazi vya wanyonge waliokuwa jeshini, vikafanya mapinduzi yaliyofanikiwa muda mfupi kabla wakati wa Sulubu kuuawa haujafika.

(uk. 168). Kwa hivyo, kulingana na Mohamed Suleiman Mohamed mafalahi wanaowakilishwa na Sulubu wamepewa nafasi kubwa katika ulipuaji wa mapinduzi. Ni kutokana na idhilali iliyowakusa ambapo tunapata kitendo cha kumwua Karim kikiwachochea wanajeshi wachukue hatamu za uongozi wa nchi. Jambo linalojitokeza hapa ni kwamba tabaka la wanyonge ndilo linalochukua uongozi wa kisiasa kwa mabavu. Mwanajeshi anasikika akiwatuliza wananchi:

> Poeni wananchi! Poeni wananchi!
> Dhuluma imeshapinduliwa! Haki tupu!
> Haki tupu! Uhuru na haki! (uk. 168).

Riwaya ya Nyota ya Rehema, kama vile ya Asali Chungu haitoi fununu yoyote kuhusu dhima ya vyama katika ulipuaji wa mapinduzi. Hata hivyo, inaonyesha matumizi ya mabavu kama njia ya pekee ya wanyonge kujitanzua kutokana na dhuluma za mamwinyi na mabepari.

Katika Kasri ya Mwinyi Fuad tunawaona mafalahi na wafanyakazi wakijiandaa Dambwe kwa kukusanya silaha. Katika maandalizi haya, ushirika unabainika baina ya mafalahi wa Koani na mashamba mengine na wafanyakazi wanaoongoza mikutano ya Kijangwani. Wafanyakazi wa mjini wakiongozwa na Marijani wanajitokeza kama waasisi wa matabaka hayo mengine. Kwa hivyo, Shafi Adam Shafi

analipa tabaka la wafanyakazi dhima maalum ya kuyaongoza mapinduzi. Kondo anawaambia wenzake:

> Salamu zenu nyingi kutoka kijangwani
> Wanasema wakati umekaribia na siku
> haiko mbali. Mamao yote madhubuti
> na maboma yote mawili tutayakamata
> siku moja (uk. 69)

Dhima wanayopewa wafanyakazi wa mjini ya kulipua mapinduzi katika Kasri ya Mwinyi Fuad inawiana na urazini wa kitabaka miongoni mwa watu wa tabaka hili unaotubainikia katika Kuli na Dunia Mti Mkavu. Jambo hili lina uhalisi wa kihistoria kwa sababu, kama tulivyoonyesha, vyama vya wafanyakazi visiwani Zanzibar kama vile Shirikisho la vyama vya wafanyakazi, muungano wa vyama vya wafanyakazi wa Pemba na Unguja na Umoja wa Waandishi wa Habari vilishiriki kwa dhati katika siasa za visiwani. Uhalisi huu wa kihistoria unatokana na maisha ya wafanyakazi yanayowatayarisha wafanye mambo mbali mbali: wakaribiane kihisia na kimtazamo na waanzishe vyama vyao vyenye ushikamano. Wafanyakazi huwa wametangamana kijiografia na maisha yao yana nidhamu maalum ya kazi na uhusiano. Aidha, maisha yao makali yanawajasurisha na kuwafanya waweze kustahamili mambo magumu na yanayoogofya.[7]

Kwa hivyo, katika ulipuaji wa mapinduzi, Shafi Adam Shafi amewapa wafanyakazi jukumu linalopendekezwa na Lenin (1981:17) asemapo:

> Ni tabaka maalum tu, yaani wafanyakazi wa mjini na wafanyakazi wa viwandani kwa jumla...... ndiyo inayoweza kuuongoza umma wote wa watu wafanyao kazi na wanyonywao katika mapambano ya kuuondoa utumwa wa rasilmali, katika kuyatekeleza hasa, katika mapambano ya kuuhifadhi na kuimarisha ushindi, katika kazi ya kuunda mfumo mpya wa kijamii wa kisoshalisti na katika mapambano yote ya kuania uondoshaji kamili wa tabaka.

Wafanyakazi wanachukua mstari wa mbele katika ulipuaji wa mapinduzi. Muungano wao na mafalahi unateka maboma ya askari wa serikali Mtoni, Ziwani, na Malindi. Kituo cha redio vile vile kinatekwa. John Okello (1967:140-146) ametueleza kwamba Bomani, Ziwani, Malindi na kituo cha redio cha Raha Leo vilitwaliwa kwa muda mfupi.

Senkoro (1984:36) anasema mapinduzi katika Kasri ya Mwinyi Fuad yanatokea kiurahisi mno.

Tunakubaliana naye kwa sababu hisia tunazopewa ni kwamba upande wa kitawala ulikuwa hauna nguvu za kujihami. Hisia hizi vile vile zinaonekana katika Asali Chungu na Nyota ya Rehema. Katika riwaya hizi tunaonyeshwa ushindi wa ghafla wa wanyonge lakini hatuonyeshwi maandalizi ya kituo wala mapambano makali wakati wa utekaji wa taasisi za utawala.

4.4. UIMARISHAJI WA MAPINDUZI:

Riwaya tunazozihakiki zinazotusimulia, kwa kiasi fulani, juhudi za uimarishaji na uendelezaji wa mapinduzi ni Kasri ya Mwinyi Fuad na Utengano.

Katika Kasri ya Mwinyi Fuad, ardhi iliyokuwa chini ya milki ya mamwinyi kama Khalfan, Swelum, Khator, na Fuad inataifishwa na inakuwa mali ya umma. Kwa hivyo, mfumo wa uzalishaji mali unabadilishwa. Nyenzo kuu za uzalishaji mali ambazo hapo mwanzoni zilikuwa zinamilikiwa na mamwinyi, zinatwaliwa na kugawanywa kwa mujibu wa siasa mpya ya ujamaa. Juhudi hizi zinatekelezwa na Idara mpya ya Ugawaji wa Ardhi. Fuad anaambiwa:

> Kila mkulima anayeishi katika eneo hili atagawiwa ardhi na baada ya hapo kuna mipango ya kuanzisha ukulima wa kijamaa, yaani kuanzisha mashamba ya

> ushirika. Maana yake ni kwamba shamba lako itabidi ligawiwe (sic) na wewe mwenyewe utapewa sehemu yako ili nawe, uwe na kitu cha kuendeshea maisha (uk. 88)

Mahali na starehe zilizokuwa zimetengewa tabaka la kimwinyi zinafunguliwa kwa umma. Kwa mfano, Karimjee Club inageuzwa jina na kuitwa People's Club.

Mfumo mpya wa uzalishaji mali unatarajia wananchi wote washiriki katika juhudi za uzalishaji mali. Hata hivyo, Fuad anawatarajia baadhi ya watumishi wake waendelee kumtumikia na kumhudumia kama yalivyokuwa mazoea. Anatumia unafiki na kiburi kumpumbaza Kijakazi asifahamu yanayojiri katika taifa lake hasa Fuad anapogundua kwamba 'amesalitiwa' na wafanyakazi wake aliowaona watiifu kabla ya mapinduzi. Kwa upande wake, Kijakazi amechakazwa na maisha ya kitumwa yenye mateso, matusi, usumbufu, masimango na mughna. Ametengwa na mazingira yake asijue kuwa pametokea mabadiliko ya mfumo wa kisiasa. Anafanya kazi huku akififikiri kuwa Fuad angali na nguvu za 'Ki-ungu.'

Lakini, kila binadamu ana uwezo wa kuamka kiurazini akamaizi hali yake na akachukue hatua ya kuibadili hali hiyo. Kijakazi polepole anaanza kuamka

hasa anapoona mafanikio ya shamba la ushirika. Anapopata urazini kamili anamkabili Fuad kwa ukali na ghamidha:

> Sikiliza Fuad! Nakwambia wazi, baada ya leo, sitokubali kukutumikia utumwa wa aina yoyote! Mimi nimejichokea! (uk.150)

Kijakazi anaasi na anakaribishwa na Machano, Mkongwe na Vuai katika shamba la ushirika.

Mwamko wa Kijakazi baada ya mlipuko wa mapinduzi ni taashira ya wananchi kuikubali itikadi ya kijamaa. Mfumo huu mpya unasawiriwa katika Kasri ya Mwinyi Fuad kama mfumo unaoweza kuwafaidi wananchi kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kijakazi ni mfano wa wananchi ambao wamenyanyaswa kiasi cha kufanywa wanyama lakini wawezao kutanabahi baadaye kuwa hawana budi kushirikiana na wanyonge wenzao kusudi watarazaki.

Mabadiliko ya kifikra, kijamii, kiuchumi na kisiasa yanaletwa na 'uimla' wa wafanyakazi na wanawafanya mamwinyi watoroke kwa sababu hawawezi kustahimili nafasi yao duni wanayopewa na mfumo mpya wa uzalishaji mali. Kwa mfano, katika Kasri ya Mwinyi Fuad, Fuad anakosa stahamala na anatoroka kwa njia ya kichinichini.

Shafi Adam Shafi anatuonyesha kwamba mapinduzi haya ya kijamii yatafaulu hasa kwa sababu tabaka la kimwinyi limekata tamaa na umma uko mbioni kujiimarisha na kuujenga upya mkondo wa maisha yao.

Baada ya mlipuko wa mapinduzi katika Nyota ya Rehema, haki inaanza kutekelezwa. Shamba la pakani linawarejelea wastahiki wake, Sulubu na Rehema. Kwa upande mwingine, Salma, kama vile Fuad katika Kasri ya Mwinyi Fuad, anahama na anaenda Ulaya kujiunga na nduguye, Samir. Kuondoka huku, kama vile vifo vya mamwinyi wale wengine, ni ishara kwamba ameshindwa kuwiana na mfumo mpya. Katika harakati hizi za mapinduzi, Rehema anamzaa 'Fuad'. Jambo hili linaweza kuchukuliwa kama ithibati ya kimaumbile kuwa Rehema alikuwa mtoto wa halali wa Fuad.

Riwaya ya Utengano imezama katika kubainisha shida za uimarishaji wa mapinduzi. Shida hizi zinajitokeza katika pembe mbili: usaliti miongoni mwa viongozi na nafasi ya mwanamke katika taifa jipya.

Usaliti miongoni mwa viongozi unawakilishwa na Maksuudi Kambe. Maksuudi ni mwakilishi wa viongozi mabarakala na wazandiki baada ya mapinduzi. Anatokana na ukoo wa Wafanyakazi na wakulima. Kabla ya uhuru alikuwa mtetezi wa haki za umma. Tunaambiwa:

> Yeye ndiye aliyekuwa miongoni mwa waasisi wa chama cha Mwafrika. Naye alijitolea kwa nia, mvua na jua.... uhuru ukapatikana, mkoloni akatoweka. (Lakini) Maksuudi aligombania uhuru wa nchi yake kwa tamaa kwamba wakitoka wale watu weupe, yeye atakuwa mmojawapo atakayekamata nafasi zao. (uk. 17).

Maksuudi ni kielelezo cha wasomi wanaojifunga-manisha na umma wakati wa jitihada za ukombozi ili baadaye wajifaidishe. Katika tamthilia ya Mashetani, Ebrahim Hussein ametuonyesha kwamba baada ya kutimuliwa akina Juma kutoka uongozini kisiasa na kiuchumi nafasi yao ilijazwa na akina Kitaru ambao walianza kujilundikizia magari na rasilmali nyingi. Kikundi hiki ndicho kinachosimuliwa na Said Ahmed katika Kina cha Maisha asemapo:

> Alikuwa mtu duni, alizongwa na shakawa
> Hana alichoauni, wala alichoambuwa
> Walikimwita mhuni, na thamani kumtowa
> Utamwonea imani, jinsi ya alivyokuwa
> Mwepesi wa kusahau.
>
> .......

Leo kawa Sultani, mwingine kattu hajawa
Hatamani na haoni, nyuma aliyochukuwa
Anga kwake limeguni, gubi amegubiliwa
Mwanadamu maluuni, hakika ukichunguwa
Mwepesi wa kusahau.[8]

Maksuudi anatumia elimu yake ya kidini na kitaaluma kuficha utashi wake na dhamira yake ya muda mrefu. Baada ya mapinduzi, anapewa wadhifa wa kuwa Mkuu wa Wilaya. Kama vile mwenzake Zuberi katika Asali Chungu, kabla ya mapinduzi, Maksuudi ni fisadi mkubwa. Kwa mfano, 'anakula' shilingi mia mbili za mke wa Japu, aliyetaka kiwanja cha kujenga nyumba, ili akubali kutia sahihi katika ombi lake. Lakini kwa vile zimwi likujualo halikuli likakwisha, Maksuudi anafanywa Mkurugenzi wa Shirika la Bima la Taifa. Hata hivyo, habadilishi mwendo wake bali anashughulika na magendo. Anawapa akina Smith haki ingawa ajua hawaistahiki (uk. 72). Tena, Maksuudi anatumia cheo chake kumhini Mwanasururu mali yake na kisha anamtaliki. Mwanasururu anatumbukia katika uoza wa kijamii kama vile alivyofanya Semeni katika Asali Chungu.

Kwa upande mwingine, kuna baadhi ya wananchi wanaojitahidi kuyaimarisha mapinduzi. Mfano wa

wananchi hawa ni Siwa na Fadhili. Siwa ni kijana mwanasiasa ambaye, ingawa tajiriba zake hazikuelezwa, umaarufu wake miongoni mwa umma unatufanya tumchukulie kama mmoja wao. Fadhili ni ndugu wa uzawa wa Maksuudi. Uhusiano wa ndugu hawa unaweza kumithilishwa na wa Farouk Hilal, Bakari, Fumu na Pandu katika Dunia Mti Mkavu. Fadhili ni mzalendo halisi ambaye amejitwika jukumu la kuyaimarisha mapinduzi. Mkabala wake kuhusu maisha unatofautiana na wa Maksuudi na hili linasababisha mgogoro baina yao. Maksuudi angetaka asaidiwe na Inspekta Fadhili kusudi ajinufaishe binafsi ilhali Fadhili yuko mbioni kuzuia mambo yoyote ambayo yangehatarisha mapinduzi. Fadhili anayaweka maslahi ya umma mbele ya uzawa. Kama vile katika Dunia Mti Mkavu, tunaona kwamba maslahi ya tabaka yanainuliwa dhidi ya uzawa katika mahusiano ya watu wenye urazini wa kitabaka.

Katika Utengano, tunabainishiwa dhima ya askari katika taifa lililojikomboa dhidi ya ukoloni. Askari wanapewa jukumu la kusaidia kuendeleza na kuimarisha mapinduzi ilhali kabla ya mapinduzi, kama tulivyoona, wanatumiwa kuzuia mabadiliko.

Jitihada za Maksuudi kumshawishi Fadhili adidimize kesi ya magendo hazifai dafu. Aidha, Maksuudi anajikuta amevunjwavunjwa kiuchumi na kijamii

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

kwa sababu ya tamaa yake inayomwelekeza katika uzinzi na magendo, udhalimu wake na unafiki wake. Haya yanamfanya atengwe na aila yake.

Said Ahmed anatuonyesha kwamba ingawa kwa namna fulani, mapinduzi ya Januari, 1964 yaliondoa utumwa, kwa upande mwingine kuna utumwa uliosalia. Huu ni utumwa na wanawake. Katika kurasa zilizotangulia, tumeonyesha kwamba mfumo wa uzalishaji mali uliokuwapo kabla ya mapinduzi, haukumpa mwanamke hadhi anayoistahiki. Aghalabu alichukuliwa kama chombo cha kumfurahisha mwanamme au cha kuzalishia mali. Hali hii haikubadilika sana baada ya mapinduzi.

Said Ahmed anatwambia kwamba jumba la Maksuudi ingefaa liitwe 'Kasri la Watawa' (uk. 19); kutokana na kimo chake, heba na uzuri ulioListahiki. Litakuwa la 'Watawa' kwa sababu Bi. Tamima, mkewe, na Maimuna, bintiye, 'wanatawishwa'. Hawaruhusiwi kutoka nje bila ruhusa yake wala kumkaribisha mtu humo bila idhini yake. Wanawake hawa hawapewi nafasi ya kutoa mchango wao katika maendeleo ya jamii mpya. Wanatengwa na mazingira yao. Juhudi za Maimuna za kutafuta uhuru zinamzamisha katika uchafu wa kimaisha na kitabia kama vile Rehema wa Nyota ya Rehema alivyobobea katika ukahaba kwa kutengwa na aila yake.

Ni katika hali hii ya kumdhalilisha mwanamke

ambapo Maksuudi anamdhulumu mkewe, Mwanasururu. Mwanasururu alikuwa amerithi ng'ombe, kijishamba kidogo, vyombo vya dhahabu na fedha. Maksuudi akamvamia akamtawisha, akamfisidi rasilmali yake yote na kisha akamwacha. Mamake Mwanasururu (Bi. Farashuu) akaapa kulipiza kisasi na kutokana na hali hii Maimuna anabadilishwa kuwa kitatange na Bi. Tamima anatalikiana na Mumewe.

Maimuna anatumiwa na mama Jeni kama chombo cha kunasia mtaji kutoka kwa wanaume. Tena, katika hoteli Rumbalola anakuwa 'gwiji' wa nataki na nyimbo na, kwa hivyo, sauti yake nzuri na tambo lake la kupendeza, vinatumiwa kuvutia wateja. Al'muradi kokote Maimuna aendako anakuwa kiumbe wa kufyonzwa na ulimwengu mpaka pale anapoelekezwa na 'Sadfa' mikononi mwa Kabi. Kabi, kama vile Sulubu katika Nyota ya Rehema, ni kiumbe mwenye utu kamili. Kabi na Sulubu wanawakilisha binadamu ambao hawakuchafuliwa na mazingira yao. Ingawa Maimuna na Rehema wana historia ya ukahaba, wanakubaliwa na wahusika hawa kwa sababu wameweza kujiopoa kutokana na hali hiyo iliyosababishwa na mfumo wa uzalishaji mali uliowaweka pembezoni. Kabi anamhakikishia Maimuna:

> Binadamu anaweza kuwa mnyama
> lakini baadaye akaurejelea ubinadamu

wake. (uk. 162)

Suala la ukombozi wa wanawake katika enzi ya mapinduzi ni la kimsingi lakini silaha anayopewa Bi. Farashuu ya kulipiza kisasi dhidi ya Maksuudi kwa kumtenganisha na aila yake, ina udhaifu. Kisasi hakiwezi kuleta suluhisho la kudumu wala hakiwezi kuchangisha katika uimarishaji wa mapinduzi. Kazija anasababisha utengano wa Maksuudi na mwanawe Mussa na kisha anamfedhehesha Maksuudi wakati wa uchaguzi. Yote haya anayafanya kwa niaba ya Bi. Farashuu. Biti Kocho anasababisha utengano wa Maimuna na wazazi wake na Tamima na mumewe. Wahusika hawa wanafahamu kuwa wanawake wananyanyaswa hata baada ya mapinduzi lakini wanashindwa kuiona hali hii kama urithi utokanao na mfumo wa kimwinyi na ambao unapasa kuangamizwa kutokana na harakati za pamoja.

Ujasiri na juhudi za Kazija, Farashuu na Biti Kocho za kuwatetea wanawake, zimetengana na hazina ushikamano unaoweza kuleta ukombozi kamili.

Serikali ya kimapinduzi inaonekana kufahamu kwamba ukombozi wa wanawake ni jambo la kimsingi katika uimarishaji wa mapinduzi. Tunaambiwa:

> Serikali itafanya kampeni kubwa
> kuwaelimisha wanawake vijijini...
> kunatakikana maendeleo ya haraka

> vijijini na maendeleo ya wanawake ni maendeleo ya jamii nzima, na ukombozi wa wanawake ni ukombozi wa jamii nzima (uk. 173)

Ukombozi wa wanawake katika harakati za kimapinduzi ni suala muhimu. Samora Machel katika makala yake[9] amelirejelea jambo hili. Machel (katika Turok 1980:157) amesema kwamba dhamira ya mapinduzi ni kutupilia mbali mfumo wa ukandamizaji. Hili hutoa nafasi kwa ujenzi wa jamii mpya ambayo inahurisha na kushajiisha juhudi za binadamu wote. Kwa hivyo, juhudi za binadamu, nguvu za uzalishaji mali na maumbile huungana katika kuibadilisha dunia imfaidi binadamu kwa jumla. Ili mapinduzi yasemekane kuwa yamefaulu watu <u>wote</u> wanaokandamizwa hawana budi kukombolewa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kisaikolojia. Wanawake hawapaswi kutengwa pembezoni katika harakati za mapinduzi bali wanapaswa kushiriki tangu mwanzo katika ukombozi wao na ukombozi wa umma kwa jumla.

Aidha, ukombozi wa wanawake haupaswi kutazamwa katika ufinyu wake bali katika upana wa ukombozi kwa jumla. Mapinduzi ya kijamii ndiyo yanayoweza kuwapa nafasi wanayoistahiki katika shughuli za uzalishaji mali. Ujumbe huu unasisitizwa katika <u>Dunia Mti Mkavu</u>,

Kasri ya Mwinyi Fuad, Kuli na Utengano. Riwaya hizi zinaufungamarisha ukombozi wa wanawake na ukombozi wa umma.

Kwa hivyo, katika kiwango cha uimarishaji wa mapinduzi kama hatua ya kuuendeleza mfumo wa kimapinduzi, baadhi ya waandishi wa visiwani wanatuonyesha juhudi zinazofanywa katika viwango vya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kisaikolojia. Juhudi hizi zinafaulu lakini kwa kiasi kingine zinatingwa na matatizo. Kuwepo kwa viongozi kama Maksuudi na Zanga ambao wanazijali nafsi zao na wanaendeleza kasumba zilizokuwepo wakati wa enzi ya umwinyi, kunahatarisha mapinduzi na huenda kukayafanya yasifaulu. Hata hivyo, kutokana na juhudi za watu kama Fadhili, Siwa, Vuai na Marijani kuna matumaini kwamba harakati za kuyafanikisha mapinduzi hazitakoma bali zitaendelea kuuwasha mshumaa hadi kuche. Kwani, mapinduzi si kitendo kimoja tu bali ni mfumo unaochukua muda kupevuka na kuimarika.[10] Harakati tunazoziona katika riwaya hizi kuyatekeleza na kuyaimarisha mapinduzi ni sehemu tu ya mfumo huo.

## 4.5 HITIMISHO

Katika sura hii tumesema kwamba vyama vya kisiasa na vya wafanyakazi vilishiriki katika harakati za siasa Zanzibar. Hata hivyo, hakukuwa na Chama cha

Waasisi ambacho kingetayarisha sera, nadharia na itikadi kwa makini na kisayani ili kuyafanikisha mapinduzi. ASP kilikuwa chama cha umma lakini si cha waasisi. Viongozi wake hawakusoma sana nadharia ya mapinduzi wala ya ujenzi wa ujamaa wa kisayansi.[11] Baadhi yao waliibuka kama wasaliti na mabarakala waliotumia mapinduzi kutosheleza utashi wao. Mfano wa viongozi hao ni Maksuudi katika Utengano. Kwa upande mwingine, chama cha UMMA, ingawa kilikuwa kimeimarika kiitikadi na kinadharia, hakikuwa na misingi mikubwa miongoni mwa wananchi, kwa sababu kilikuwa kichanga. Aidha, baada ya mapinduzi viongozi wake walishikwa na chama kikapigwa marufuku. Waandishi wa riwaya visiwani hawakuvipa vyama hivi nafasi kubwa katika kazi zao.

Tumeona kwamba mapinduzi ya kijamii yanapofaulu hubadilisha msingi wa muundo wa kiuchumi na wa kisiasa ilhali mapinduzi ya kisiasa hubadili msingi wa muundo wa siasa. Utekaji wa taasisi za kitawala kwa njia ya nguvu pamoja na juhudi za utaifishaji wa mashamba na uamshaji wa umma kisiasa ni hatua zinazobainika katika riwaya za visiwani. Matumizi ya mabavu yanasawiriwa na waandishi wote kama njia ya pekee ya kuleta mabadiliko muhimu miongoni mwa wananchi.

Ukombozi wa wanawake umeonekana kufungamana na ukombozi wa kisiasa na kiuchumi na kwa hivyo wanawake hawana budi kushiriki katika harakati za mapinduzi. Ukweli huu unabainika katika takriban riwaya zote za visiwani.

## 4.6 TANBIHI

1. Kuhusu umuhimu wa vyama vya wafanyakazi katika mapinduzi tazama Dridzo, S.A. (1976) Marx and the Trade Unions. Greenwood Press, Connecticut

2. Sera hii inawatenga watu wenye maslahi sawa ili kuwadhoofisha wasiweze kutumia nguvu zao kwa pamoja. Kujikita kwa utengano kunasahilisha kumilikiwa kwao.

3. Tazama Sanger, C. (1967) katika Okello, J. Revolution in Zanzibar. East African Publishing House. Nairobi. Utangulizi.

4. Babu, A.M. (1982) katika Tandon, Y. (mhariri) Debate on Class, State and Imperialism. Tanzania Publishing House. Dar-es-Salaam (uk. 1)

5. Senkoro, F.E.M.K. (1984): Uhakiki wake wa Kasri ya Mwinyi Fuad katika Mulika na 16 Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu, Dar-es-Salaam. (uk 36)

6. Cabral, A (1969) Revolution in Guinea: An African People's Struggle. Stage I London (uk. 75) anasisitiza sana nafasi ya nadharia katika mapinduzi.

7. Tazama Draper, H. (1978) Marx's Theory of Revolution Vol. 2 Monthly Review Press. New York (uk. 40-48)

8. Mohamed, S.A. (1984) <u>Kina cha Maisha</u> Longman. Nairobi. (uk.1)

9. Machel, S. (1980) 'Women's Liberation is Essential for the Revolution' katika Turok, B. <u>Revolutionary Thought in the 20th Century</u>. Zed Press. London (uk. 157-167). Tazama vile vile hotuba za Fidel Castro na makala ya Linda Jenness katika <u>Women and the Cuban Revolution</u> (1970). Amerit Pamphlet. New York.

10. Kwa mfano mapinduzi ya Cuba hayakuanza na kumalizika 1959. Kitovu chake kitaonekana katika enzi ya John Quincy Adams, Karne iliyopita. Mapinduzi hayo yangali yanaendelea.

11. Fikra hizi zinatokana na mjadala wangu na Said Ahmed Mohamed tarehe 9/5/1987, Mjini Nairobi.

# SURA YA TANO

# 5.0 HITIMISHO

## 5.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tutagusia machache kuhusu kazi tuliyoifanya kwa jumla huku tukionyesha mambo yaliyojitokeza katika utafiti wetu. Pili, tutasema machache kuhusu matatizo tuliyokumbana nayo na mafanikio ya kazi yetu. Kisha tutaongea kuhusu ilhamu itokanayo na waandishi wa visiwani na vile vile mapendekezo kuhusu utafiti unaoweza kufanywa kuwahusu waandishi hawa wa visiwani.

## 5.2 KAZI KWA JUMLA

Kazi hii imejishughulisha na maudhui ya mapinduzi kama yanavyojitokeza katika riwaya za visiwani, Zanzibar. Kutokana na riwaya hizi ni bayana kwamba kitovu cha mapinduzi kinapatikana katika mfumo wa uzalishaji mali.

Mfumo wa uzalishaji mali wenye muundo wa kitabaka husababisha mikinzano mikali katika uhusiano wa watu ambayo, ikielekezwa kiurazini, huleta mabadiliko ya mfumo mzima wa kiuchumi. Tumeona kwamba wakati mikinzano inapochacha, tabaka lenye nguvu za kiuchumi huungwa mkono na taasisi za kitawala (Marx na Engels 1979:259)

Katika muktadha wa visiwani, Zanzibar kabla ya mapinduzi rangi ya mtu na tabaka viliandamana. Hii ni kwa sababu nafasi za elimu na kazi za kitaaluma ziliachiwa watu wachache waliomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Hawa walikuwa Waarabu, Wahindi na Wazungu. Waafrika wengi wakaachwa wauze nguvu na siha yao katika kazi za dharubu na sulubu.

Riwaya hizi zimetuonyesha uoza wa kijamii na pupa iliyotangulia mapinduzi. Tumetoa mifano kubainisha pupa ya mali na mwili hasa miongoni mwa tabaka tawala. Wanyonge wananyang'anywa vikataa vyao na wengine wanalazimishwa kuingia ndoa wasizozitaka.

Tumesema kwamba mikinzano ya kitabaka inaleta urazini wa kitabaka. Baadhi ya waandishi wa visiwani kama Said Ahmed katika Dunia Mti Mkavu na Shafi Adam katika Kasri ya Mwinyi Fuad na Kuli wamelipa tabaka la wafanyakazi dhima ya kuyaongoza matabaka hayo mengine katika usuluhishaji wa mikinzano. Tumetoa kauli kwamba japo nyakati nyingine nguvu za wanyonge zinaonekana kushindwa, waandishi hawa, isipokuwa Mohamed Suleiman katika Kiu, wanatupa matumaini kwamba juhudi zao huenda zikafaulu baadaye.

Cabral (1969:75) amesema kuwa nadharia ya kimapinduzi ni muhimu sana katika kuyafanikisha mapinduzi. Aghalabu nadharia hii huenezwa na Chama

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

cha waasisi ambao wamepevuka kiurazini na wana mizizi imara miongoni mwa umma. Katika sura ya nne, tumeona kwamba hakuna nafasi iliyopewa chama cha waasisi katika riwaya za visiwani. Jambo hili linawiana na historia ya visiwani. Huenda shida zinazobainika katika Utengano kuhusu utekelezaji wa mapinduzi zina msingi wake katika jambo hili.

Matumizi ya nguvu kama jambo la lazima katika mapinduzi yametanda katika kazi za waandishi hawa wa visiwani. Ni bayana kwamba vifo vya mamwinyi ni jazanda ya kushindwa kwao kustahimili mikinzano mikali ya kitabaka. Hili linaonyesha uwezekano wa tabaka hili kuvunjwavunjwa. Lakini katika mkumbano huu, watu wa tabaka la chini wanabidika kujitoa mhanga. Ndiposa Bakari katika Kuli na Kumba katika Dunia Mti Mkavu wanafariki.

Jambo jingine linalojitokeza katika riwaya hizi ni kwamba harakati za mapinduzi hazina budi kuwashiririkisha wanawake. Kwa hivyo, ukombozi wa mwanamke unafungamanishwa na ukombozi wa umma kiuchumi, kisiasa, kijamii na kisaikolojia.

Katika kiwango cha uimarishaji wa mapinduzi tumeona kwamba Shafi Adam Shafi katika Kasri ya Mwinyi Fuad anachukulia utaifishaji wa nyenzo za uzalishaji mali kama hatua muhimu na ya kimsingi. Tena, haja

ya ukombozi wa kisaikolojia inasisitizwa kwa sababu fikra za kitumwa kama za Kijakazi zinaweza kurudisha nyuma juhudi za ukombozi.

Sehemu hii vile vile imeonyesha ugumu wa uimarishaji wa mapinduzi kama unavyojidhihirisha katika Utengano. Said Ahmed amebainisha haja ya viongozi mabarakala kufichuliwa na kutokomezwa. Hizi ndizo juhudi zinazotekelezwa na Fadhili na Siwa.

Kwa jumla basi, kazi hii imetazama maudhui ya mapinduzi katika viwango vitatu: muundo wa mfumo wa uzalishaji mali, nafasi ya mikinzano ya kitabaka na mapinduzi na baadaye.

## 5.3 ILHAMU

Waandishi hawa wametiana ilhamu na kushajiishiana kwa sababu wanajihusisha na masuala yanayofanana. Huenda jambo hili ndilo lililomfanya Kitsao (1982;117-118) atoe kauli kwamba kazi za Said Ahmed 'zimepata mfano wake katika Nyota ya Rehema' Kazi za Said Ahmed Mohamed zinachukuliwa kama 'miigo' ya Nyota ya Rehema. Fikra hizi zinatokana na mshabaha mkubwa ulioko baina ya Asali Chungu, Utengano na Nyota ya Rehema. Nafasi ya 'Sadfa' katika maisha ya wahusika ni kubwa sana. Tena, uoza wa kijamii unaomkumba Rehema mjini na ule wa Maimuna umefanana kwa kiasi kikubwa. Aidha, Maimuna 'anakumbana' na

Kabi ambaye ni kiumbe mwenye utu japo ni kiguru na katika kufanya hivyo anajiopoa kutokana na ghilba za ulimwengu, kama vile Rehema 'anavyokumbana' na Sulubu na anaukabili utu asiopata kuuona katika ulimwengu wenye maonevu. Isitoshe, mapinduzi ya mabavu yanatukia katika Asali Chungu na Nyota ya Rehema.

Kwa maoni yetu, ingawa kuna mshabaha katika baadhi ya kazi za Said Ahmed na Nyota ya Rehema, hii ni kwa sababu kitovu cha ilhamu yao ya kuandika ni kimoja. Wamelelewa na kukulia katika mfumo mmoja wa uzalishaji mali na kwa hivyo tajiriba zao zimefanana. Yumkini, Said Ahmed amepata ilhamu ya kuandika Asali Chungu na Utengano kutokana na Nyota ya Rehema baada ya 'kuathiriwa' kihisia na riwaya hii kama vile Ngugi wa Thiong'o alivyoathiriwa na riwaya ya Conrad ya Under Western Eyes. Katika Dunia Mti Mkavu Said Ahmed anajitenga na 'taathira' hizo na anayasawiri maudhui ya mapinduzi huku akiyafungamanisha na historia ya visiwani. Anahifadhi kisanaa migomo ya 1948 na 1951 kama vile Shafi Adam anavyohifadhi mgomo wa 1948.

Waandishi hawa wanahamasishana na kuathiriana. Bila shaka kazi zao zitawatia ilhamu waandishi wengine wa fasihi ya Kiswahili.

5.4 MATATIZO NA MAFANIKIO

Tulidhamiria kuonyesha kwamba fasihi na jamii ni vitu vilivyofungamana. Kutokana na uhakiki wa maudhui ya visiwani, uhusiano huo umejibainisha. Aidha, tumefanikiwa kuonyesha kuwa waandishi wanaweza kusimulia kuhusu tukio moja kwa namna tofauti kutegemea mkabala wao wa maisha unaowasaidia katika upembuzi.

Tulipoanza utafiti huu tulitarajia mapinduzi yatakuwa yamewiana na historia ya visiwani. Tulifahamu nafasi ya ubunifu katika fasihi lakini katika kiwango cha uyakinifu wa kihistoria tumeona waandishi hawa wakiyasimulia kitofauti. Kwa mfano Nyota ya Rehema inawapa mafalahi na jeshi nafasi kubwa kinyume na Kasri ya Mwinyi Fuad. Mpaka hivi sasa, hatujui kazi yoyote ya kihistoria inayotueleza wazi wazi nafasi za matabaka mbalimbali katika mapinduzi ya visiwani. Kile tulichokifanya ni kuyadhihirisha matabaka hayo katika riwaya za visiwani na katika kufanya hivyo tukaongozwa na nadharia ya Ki-Marx tuliyoitumia katika uhakiki wetu.

5.5 MAPENDEKEZO

Ijapokuwa katika kazi hii tumezihakiki riwaya za Shafi Adam Shafi, Mohamed Suleiman Mohamed na Said Ahmed Mohamed kwa mujibu wa maudhui ya mapinduzi

kuna mambo mengine yanayohusiana na kazi hizi ambayo hatukuyashughulikia kwa sababu ya upeo wa utafiti wetu. Mambo haya yanaweza kuchunguzwa na watafiti wengine baadaye.

Kwa mfano, Herbert Marcuse (1979) amesema kuwa itikadi ya kimapinduzi inaathiri ubunifu wa kisanaa. Kauli kama hivyo inaweza kuchunguzwa kwa kulinganisha riwaya za Said Ahmed Mohamed na Shafi Adam Shafi kimaudhui na kifani. Utafiti kama huo huenda ukatufaa katika kubainisha kama kuna uhusiano baina ya fikra za kimapinduzi na udhaifu wa kisanaa.

Utafiti mwingine unaoweza kufanywa ni kuhusu usawiri wa wahusika wa kimwinyi katika riwaya za visiwani. Riwaya hizi zinatuchorea taswira maalum ya mamwinyi kabla na baada ya mapinduzi. Taswira hii inaweza kulinganishwa na ile ya wanyonge.

Aidha, uchunguzi unaweza kufanywa kuhusu taswira na jazanda katika riwaya za visiwani. Uchunguzi kama huo utatuonyesha ujumi wa waandishi hawa na huenda ukabainisha mshabaha katika uchaguzi wa taswira na jazanda zao.

Tumewachunguza waandishi watatu wa riwaya za visiwani. Uchunguzi wa baadaye unaweza kuzama katika maudhui ya mapinduzi katika fasihi ya visiwani, Zanzibar. Utafiti kama huo utamtaka mhakiki achunguze tanzu za riwaya, tamthilia , ushairi na fasihi - simulizi.

MAREJELEO

Abdalla, M.S. (1973) Duniani kuna watu. East African Publishing House: Nairobi.

----------- (1974) Mzimu wa watu wa Kale. East African Literature Bureau: Nairobi.

-----------(1975) Mke Mmoja waume watatu: East African Publishing House: Nairobi.

Ake, C. (1978) Revolutionary Pressures in Africa. Zed Press: London.

Anderson, H.A. (1974) The Political Economy of Social Class. Prentice Hall: New Jersey.

Aristotle, Horace, Longinus (1965) Classical Literary Criticism. Penguin Books: Middlesex.

Arnold, E. (1970) Contemporary Criticism. Stratord Studies: London.

Arnold, R. (1973) 'Swahili Literature and Modern History: A necessary Remark on Literary Criticism' Makala katika Kiswahili Vol 42/2, 43/1 Machi 1973. Jarida la Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili. Dar-es-Salaam.

Arvon, H. (1973) Marxist Esthetics. Cornell University Press: London

Ayany, S.G. (1970) A History of Zanzibar. East African Publishing House: Nairobi.

Babu, A.M. (1981) African Socialism or Socialist Africa. Tanzania Publishing House: Dar-es-Salaam.

Baxandall, L. (Mhariri 1972) Radical Perspective in the Arts. Penguin Book: Middlesex.

Bisztray, G. (1978) Marxist Models of Literary Realism. Columbia University Press: New York.

Brett, E.A. (1972) Colonialism and Underdevelopment in East Africa. Heinemann: London.

Brown, D.M. (1985) *Land, Freedom and Fiction: History and Ideology in Kenya.* Zed Press: London.

Cabral, A. (1969) *Revolution in Guinea: An African People's Struggle:* Stage I: London.

Coser, L.A. (1963) *Sociology through Literature.* Prentice - Hall International: London.

Coupland, R. (1956) *East Africa and Its Invaders.* Oxford University Press: London

----------- (1968) *The Exploitation of East Africa: 1856-1890*: Faber and Faber Ltd: London.

Craig, D. (Mhariri 1975) *Marxists on Literature: An Anthology.* Penguin Books: Middlesex.

Debray, R. (1970) *Strategy for Revolution.* Monthly Review Press: New York.

Draper, H. (1978) *Karl Marx's Theory of Revolution* Monthly Review Press: New York.

Dridzo, S.A. (1976) *Marx and the Trade Unions.* Greenword Press: Connecticut.

Eagleton, T. (1976) *Marxism and Literary Criticism* Methuen: London.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

----------- (1976) *Criticism and Ideology: A study in Marxist Literary Theory:* NLB. London.

Esmond, B.M. (1978) *Zanzibar: Tradition and Revolution*. Hamish Hamilton London.

Fischer, E. (1959) *The Necessity of Art: A Marxist Approach.* Penguin Books: Middlesex.

Freire, P. (1972) *Pedagogy of the Oppressed.* Penguin Books. Middlesex.

---------- (1974) *Education for Critical Consciousness:* Sheen and Ward. London.

Fanon, E. (1967) *The Wretched of the Earth.* Penguin Books. Middlesex.

---------- (1967) *Toward the African Revolution. Monthly Review Press:* London

Farsy, A.S. (1960) *Kurwa na Doto*. East African *Literature Bureau*: Nairobi

Glicksberg, C.I. (1976) *The Literature of Commitment*. Associated University Press: London.

Gorky, M. (1949) *Mother*. Progress Publishers: Moscow.

Gray, J (1962) *The History of Zanzibar from the Middle Ages to 1856*. Oxford University Press: London.

Guevara, E.C. (1968) *Reminiscences of the Cuban Revolutionary War*. Monthly Review Press: London.

Hammond, T.T. (1974) *Lenin: On the Trade Unions and Revolution:* 1893-1917 Greenwood Press: Connecticut.

Hough, G. (1962) *An Essay on Criticism.* Gerald Duckworth and Co. Ltd: London.

Hussein, E. (1969) *Kinjeketile*. Oxford University Press: Nairobi.

----------- (1971) *Mashetani*. Oxford University Press: Nairobi.

----------- (1980) *Arusi*. Oxford University Press: Nairobi.

Hyden, G. (1980) *Beyond Ujamaa in Tanzania: Underdevelopment and an Uncaptured Peasantry*. Heinemann: London.

Imbuga, F. (1976) *Betrayal in the City*. East Africa Publishing House: Nairobi.

Ingrams, W. (1967) Zanzibar: Its History and Its People. Frank Cess and Co. Ltd London.

Irele, A. (1979) Perspectives in African Literature Heinemann: London.

---------- (1981) The African Experience in Literature and Ideology. Heinemann: London.

Jeanes, L (1970) Women and the Cuban Revolution. Amarit Pamphlet. New York.

Jabir, M.H. (1977) The Plantation Economy During The Protectorate Period in Zanzibar ( 1890 - 1964). Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

James, C.V. (1973) Soviel Socialist Realism: Origins and Theory. Macmillan Press: London.

Johnson, C. (1968) Revolutionary Change. University of London Press: London.

Kamunde, M.E. (1983) Kilio cha Wanyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kezilahabi, E. (1978) 'Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar.' Uhakiki katika Mulika na 14. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Dar-es-Salaam.

Kharusi, A.S. (1969) The Agony of Zanzibar: A Victim of the New Colonialism. Foreign Affairs Publishers. Survey, England.

Khatib, M.S. (1975) Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar. Oxford University Press: Nairobi.

--------------(1983) Uhakiki wa Kuli katika Mulika na 15. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Kimani wa Njogu (1986) Mwongozo wa Mukwava wa Uhehe. Heinemann: Nairobi.

Kitsao, J (1982) An Investigation of Themes in Swahili Literature and an Application of Stylostatistics to Chosen Literary Texts. Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Nairobi.

La Guma, A. (1972) In the Fog of the Seasons End. Heinemann: London.

Lang, B na F. Williams (1972) Marxism and Art: Writings in Aesthetics and Criticism. David Mckay Co. Inc. New York.

Laurenson, D. na Swingewood (1972) The Sociology of Literature. Schocken Books. New Jersey.

Lenin, V.I (1939) Imperialism: The Highest Stage of Capitalism: A Popular outline: International Publishers. New York.

----------- (1967) On Literature and Art. Progress Publishers. Moscow.

-----------(1975) Selected Works. Vol. II Progress Publishers. Moscow.

---------- (----) Selected Works. Vol. 9. Progress Publishers. Moscow.

---------- (1981) Mwanzo Mtakatifu. Idara ya Uchapishaji vitabu 'Maendeleo': Moscow.

Lodge, D. (Mhariri 1972) 20th Century Literary Criticism. Longman: London

Lofchie, M. (1965) Zanzibar: Background to the Revolution. Princeton University Press. New Jersey.

Lowenthal, L. (1957) Literature and the Image of Man Beacon Press. Boston.

Lukacs, G. (1963) The Meaning of Contemporary Realism Merlin Press. London.

--------- (1970 Lenin: A study on the Unity of his Thought. NLB. London.

--------- (1971) History and Class Consciouness: Studies in Marxist Dialectics. Merlin Press. London.

---------- (1970) Writer and Critic and other Essays Merlin Press. London.

Marcuse, H. (1979) The Aesthetic Dimension: Toward a Critique of Marxist Aesthetics. Macmillan Press. London.

Marx, K. na F. Engels (1973) On Literature and Art. International General: New York.

-------- (1977) The German Ideology. Lawrence and Wishart: London

-------- (1979) Pre-Capitalist Socio-Economic Formations. Progress Publishers: Moscow.

------- (Tarehe Haikutolewa (a) Selected Works. Vol.I Progress Publishers. Moscow

------- (Tarehe Haikutolewa (b) Capital Vol. III Progress Publishers. Moscow.

Mativo, K. (1983) 'Criteria for the Criticism of African Literature.' Makala katika Ufahamu na I, Fall 1983. Jarida la African Activist Association.

Mazrui, A. (1981) Kilio cha Haki. Longman: Nairobi.

--------- (1984) Uhakiki wa Dunia Mti Mkavu katika Kiswahili Vol 51/1, 51/2. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Mbughuni, P. (1978) 'The theme of a New Society in the Kiswahili Prose Tradition: From Oral to Written Literature' Makala katika Kiswahili Vol. 48/2. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Mlacha, S.A.K (1984) 'Riwaya za Visiwani (1970- 1980) na Ujenzi wa Jamii mpya' katika Mulika na 16. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Mohamed, S.A. (1978) Asali Chungu. Shungwaya: Nairobi

--------- (1980 (a) Dunia Mti Mkavu. Longman: Nairobi.

(1980 (b) Utengano. Longman: Nairobi

(1980 (c) Sikate Tamaa. Longman. Nairobi.

---------- (1983) 'Kupatana na Riwaya Zangu' Makala katika Mwamko na 2 Jarida la Chama cha Kiswahili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

--------- (1984) Kina cha Maisha. Longman; Nairobi

Mohamed, M.S. (1972) Kiu. East African Publishing House: Nairobi.

--------- (1976) Nyota ya Rehema. Oxford University Press. Nairobi.

--------- (1977) Kicheko cha Ushindi: Shungwaya: Nairobi.

Mrina, B.F. na W.T. Mattoke (1980) Mapambano ya Ukombozi wa Zanzibar. Tanzania Publishing House: Dar-es-Salaam.

Mosare, J (1969) 'Background to Revolution in Zanzibar. 'Makala katika Kimambo I.N. na A.J. Temu (Wahariri) A History of Tanzania. East African Publishing House. Nairobi.

Mugambi, P.J.M. (1982) Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za Kikenya zilizochapishwa. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mulokozi, M. (1979) Mukwava wa Uhehe. East African Publishing House. Nairobi.

Ngara, E. (1985) Art and Ideology in the African Novel: A study of the Infuluence of Marxism on African Writing. Heinemann: London.

Ngugi wa Thiong'o (1967) A Grain of Wheat; Heinemann Nairobi.

---------- (1977) Petals of Blood. Heinemann. Nairobi.

.....& M. Mugo (1978) Mzalendo Kimathi. Heinemann. Nairobi.

--------- (1981 (a) Detained. Heinemann: Nairobi

(1981 (b) Writers in Politics. Heinemann. Nairobi.

...... na M. Mirii (1982 (a) Nitaolewa Nikipenda. Heinemann. Nairobi.

........ (1982 (b) Shetani Msalabani. Heinemann. Nairobi.

------------ (1986) Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature. James Currey Ltd. London.

Nyerere, J.K. (1973) Ujamaa ni Imani: Moyo Kabla ya Silaha. East African Publishing House. Dar-es-Salaam.

Okello, J. (1967) The Zanzibar Revolution. East African Publishing House. Nairobi.

Ostrovsky, N (-----) How the Steel was Tempered Progress Publishers. Moscow.

Ousmare, S. (1970) God's Bits of Wood. Heinemann: London.

Plekhanov, G.V. (1957) Art and Social Life: Progress Publishers, Moscow.

Raymond, W. (1977) Marxism and Literature Oxford University Press Oxford.

Robert, S. (1967) *Utubora Mkulima.* Nelson Nairobi.

Rodney, W. (1972) *How Europe Underdeveloped Africa*. Tanzania Publishing House: Dar-es-Salaam.

Senkoro, F.E.M.K. (1982) *The Prostitute in African Literature*: Tanzania Publishing House: Dar-es-Salaam.

Shafi, S.A. (1978) *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Tanzania Publishing House: Dar-es-Salaam.

--------- (1979) *Kuli*. Tanzania Publishing House: Dar-es-Salaam.

Shivji, I.G. (1976) *Class Struggle in Tanzania.* Tanzania Publishing House: Dar-es-Salaam.

Skocpol, T. (1979) *States and Social Revolutions*. Cambridge University Press; Cambridge.

'Soviet Literature' (1968) Sehemu ya I Jarida la chama cha Waandishi wa USSR.

Suchkov, B. (1973) *A History of Realism*. Progress Publishers. Moscow.

Swingewood, A. (1975) *Marx and Modern Social Theory* Macmillan Press London.

Tandon, Y. (Mhariri 1982) Debate on Class, State and Imperialism. Tanzania. Publishing House. Dar-es-Salaam.

Trotskii, L. (1971) Literature and Revolution The University of Michigan Press. U.S.A.

Turok, B. (Mhariri 1980) Revolutionary Thought in the 20th Century. Zed Press London.

Vasquez, A.S. (1973) Art and Society: Essays in Marxist Aesthetics. Monthly Press Review. New York.

Wastberg, P. (1968) The Writer in Modern Africa. The Scandinavian Institute of Studies, Uppsala.

Wellek, R. na A. Warren (1956) Theory of Literature Penguin Books. Harcourt.

Woddis, J. (1972 (a) Introduction to Neo-Colonialism. International Publishers. New York.

---------- (1972 (b) New Theories of Revolution, International Publishers. New York.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY